# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Ishirini - Tarehe 7 Mei, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati Ifuatazo Iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 155

**Kitengo cha Macho – Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe**

**MHE. SULEIMAN S. JAFO (K.n.y. MHE. JOHN Z. CHILIGATI)** aliuliza:-

Kitengo cha Macho katika Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe kimekuwa hakifanyi kazi kutokana kwa vifaa muhimu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaa vitakavyowezesha kitengo hicho kuanza kutoa huduma zake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Kitengo cha macho katika Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe hakifanyi kazi kama inavyotakiwa kutokana na kutokuwepo kwa vifaa muhimu na watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, huduma zinazotakiwa kutolewa katika Kitengo cha macho ni pamoja na uchunguzi, utambuzi wa magonjwa ya macho, uratibu wa shughuli za macho, kutengeneza miwani, upimaji wa macho, upasuaji wa mtoto wa jicho, upasuaji mdogo wa macho, kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje na waliolazwa na kutoa rufaa kwa wagonjwa wanaohitaji kwenda Hospitali ya rufaa kama vile *CCBRT* au Muhimbili.

Huduma zinazotolewa kwa sasa ni pamoja na kupima wagonjwa wa macho wenye matatizo na kupatiwa dawa. Kutambua wagonjwa wenye kuhitaji upasuaji mdogo na mkubwa; kuwapima macho wagonjwa wanaohitaji kuwa na miwani ya kusomea na kutoa rufaa kwa wagonjwa wenye matatizo ya macho yenye kuhitaji daktari bingwa.

Kitengo cha macho ili kiweze kufanya kazi vizuri kinahitaji kiwe na Daktari Msaidizi wa macho *(AMO OPHAMOLOGY 2)* maafisa Wauguzi Wasaidizi 2, *Optometrist* 3, Mhudumu wa Afya 1 na vifaa mbalimbali vya aina 17 vya kutolea huduma hizo.

Kwa sasa kuna aina mbili tu za vifaa hivyo, Aidha kitengo hiki hakina Daktari Bingwa wa macho na kinahudumiwa na Muuguzi Mtaalamu wa macho. Hivyo, ni kweli kuwa kituo hakifanyi kazi kwa ufanisi kutokana na kukosa vifaa muhimu na madaktari bingwa wa macho.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha zaidi huduma za macho katika Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 13 katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa ajili ya kununua vifaa tiba katika Kitengo cha macho Hospitalini hapo.

Aidha, Halmashauri imepatiwa kibali cha kuajiri Daktari wa macho katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 ambaye ataripoti wakati Serikali itakapokuwa inawapanga watumishi wa sekta ya afya wapatao 5,000 katika vituo vya kazi mwishoni mwa mwaka 2012/2013, kama ilivyoelezwa na Waziri wa nchi , Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na mipango hiyo, Halmashauri katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 iliomba maombi maalum ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya upanuzi wa Hospitali na ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya huduma mbalimbali zikiwemo huduma za macho. Kati ya mambo hayo, Serikali imeidhinisha kiasi cha shilingi milioni 300 ambapo sehemu ya fedha hizo zinatumika kununulia vifaa katika kitengo cha macho. *(Makofi)*

**MHE. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya kutia moyo ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja dogo la nyongeza tatizo la Vitengo vya macho ni kubwa katika Hospitali zote hapa nchini. Kwa maana ya kukosa wataam mabingwa na kukosa vifaa vya tiba ya macho. Je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kutatua tatizo hili ambalo ni kubwa sana kwa nchi nzima pamoja na Wilaya ya Manyoni.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika,ni kweli anavyosema Mheshimiwa Chiligati kwamba eneo hili lina matatizo kwa hizi hatua ambazo nimezieleza kwa upande kwa Kisarawe hatua hizihizi tunaendelea kuzichukua kwa ajili ya Halmashauri zingine nchini. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali la msingi linahusu Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe kukosa vifaa maalum ninaomba kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa hili tatizo la hospitali za Wilaya kutokuwa na vifaa maalum ni tatizo la karibu Hospitali za Wilaya zote Tanzania. Mfano Hospitali ya Wilaya ya Same ina hali mbaya haina vifaa vingi na ina beba wananchi wa Majimbo mawili yaani Same Mashariki na Same magharibi.

Je, Serikali ya Chama cha Mapinduzi leo inaweza kikatuambia nini kutokana na hali hii ya Hospitali zetu ambayo kila wakati tunapata majibu ambayo ni nadharia na hatupati *solution* ya kudumu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya hospitali za Wilaya zina mapungufu ya vifaa lakini jitihada za Serikali zimekuwa kubwa hasa katika kuwezesha upatikaji wa vifaa vya kisasa katika maeneo mengi, kuna maeneo ya kipaumbele eneo moja la kipaumbele ni kuwepo kwa huduma na vifaa. Kwa mfano katika huduma za uzazi vifaa vimewezesha kupatikana katika maeneo mengi katika huduma kama hiyo.

Huduma ya macho ambayo tunaizungumzia katika Swali la msingi huduma hii kwa sasa vifaa vimeboreshwa katika Hospitali zote za Mikoa na nia ni kuelekea katika Hospitali za Wilaya lakini hospitali za Wilaya unaweza kuweka vifaa vya kisasa zaidi au vile vya kibingwa pale kutakapokuwa na uwezo wa kuweka madaktari bingwa katika Hospitali hizo za Wilaya.

Mheshimiwa Spika,kabla hatujafika hapo ni lazima tuendelee kwanza katika kuongeza nguvu za ufundishaji na uwepo wa madaktari bingwa ambao kwa sasa tumeendelea na juhudi wa uwepo wa madaktari hao katika nafasi za Hospitali za Mikoa.

Kwa hiyo, tukishakamilisha hilo zoezi tutafika kwenye hospitali za Wilaya kwa sababu tuna vyuo sasa vya kufundisha wataalam katika fani hii ya upimaji wa miwani na wataalam wa ngazi hiyo ya upimaji huduma hizo za macho na vilevile kutoa fursa kwa madaktari bingwa kusomea katika nafasi hiyo ya macho ninaamini tunaweza kutatua tatizo hilo.

**SPIKA:** Tunachukua dakika kumi badala ya tano kwa hiyo tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Muhammad Chomboh, kwa niaba yake Mheshimiwa Rweikiza.

Na. 156

**Huduma Mbalimbali Kwenye Mitaa ya Jiji la Dar es salaam**

**MHE. JASSON RWEIKIZA (K. n.y. MHE. MUHAMMAD A. CHOMBOH):** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la ujenzi wa nyumba za ghorofa katika mitaa mingi katika Jiji la Dar es salaam na kuchukua nafasi ya nyumba ndogo za awali:-

Je, Serikali imejiandaaje katika miundombinu ya maji safi na maji taka, umeme na barabara za mitaa husika ili kuweza kukidhi mahitaji ya lazima kwa wakazi wa Mitaa hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo badala yake amekaa Mheshimiwa Samuel Sitta, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu wa swali la Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kuna ongezeko kubwa la ujenzi wa nyumba za ghorofa katika Jiji la Dar es salaam unaotokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii unapoelekea kuwepo kwa ongezeko la watu lisiloendana na utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii.

Ongezeko hili limeleta changamoto za miundombinu ya majisafi na salama kutokidhi mahitaji, uzalishaji mkubwa wa taka ngumu na maji taka,uzalishaji na usambazaji mdogo wa umeme usiokidhi mahitaji, pamoja na mtandao mkubwa wa barabara ambazo hazijajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto za miundombinu duni isiyoendana na ongezeko la watu na makazi, Serikali imeanza kutekeleza mipango mbalimbali ikiwemo ya uboreshaji wa miundombinu kupitia mradi wa *Dar es salaam Metropolitan Development Project (DMDP)* kwa mkopo wa Dola za Kimarekani *(USD)* milioni 75 kutoka benki ya Dunia.

Mradi wa Mabasi yaendayo haraka Dar es salaam *Dar es salaam (Rapid Speed Transit)* kwa gharama za *USD 281.22* milioni ambazo ni mkopo wa Benki ya Dunia na Mchango wa Serikali Kuu na sekta binafsi; mpango maalum wa kuboresha huduma za maji safi na uondoshaji majitaka utakaogharimu shililingi Trilion 1.09 kupitia ufadhili wa Serikali ya Marekani, Norway, India, Ubelgiji na Mkopo wa Benki ya Dunia.

Mradi wa kupanua na kuimarisha miundombinu na vituo vya kupozea, kusafirisha, na kusambaza umeme unaotekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Ufini (Finiland)kwa gharama za *Euro* milioni 26.5,mradi wa umeme ujulikanao kama *Tanzania Energy Development and Access Project (tedap)* unaotekelezwa kwa mkopo wa *USD* milioni 111.9 kutoka Benki ya Dunia na mradi wa *Electricity V* unaotekelezwa kwa mkopo na *USD* milioni 32 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi hii katika Jiji la Dar es salaam utaongeza upatikanaji wa maji safi kutoka asilimia 68 ya sasa hadi asilimia 90 na uondoshaji majitaka kutoka asilimia 10 ya sasa hadi asilimia 30 ifikapo mwaka 2015, pamoja na kuongeza uzalishaji na usambaji wa huduma ya umeme na kuboresha miundombinu ya barabara. *(Makofi)*

**MHE. JASSO S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, mradi huu wa Jiji la Dar es salaam uko pia katika miji mingine nchini kote na hata vijijini watu wanaongezeka na hivyo mahitaji ya huduma za maji, umeme na barabara upo mahali kote nchini.

Je, Serikali ina mpango gani katika kuboresha huduma hii kwa watu wote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ukisema kuwa unatengeneza mazingira ya Dar es salaam yawe mazuri kama tulivyoeleza hapa na kule kijijini ukaacha hakuna umeme, hakuna barabara watahama wote watakwenda Jijini Dar es salaam na watakuletea tatizo ukosoma mtu anaitwa Amalfudhi ndiye anayesema mambo ya *population.*

Mheshimiwa Spika, anasema majanga yatakavyotokea, watu watakufa na nini sasa hiyo tuiache mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge anachosema hapa na kama miliangalia vizuri progaramu zote ambazo zimeletwa na Serikali zinaangalia pia maendeleo ya hizi huduma nilizozisema hapa kwa maendeleo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba iliyopita ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Bajeti iliyopita hapa iliangalia maeneo mbalimbali ambayo yatakuwa yanafanyiwa kazi na hizi Wizara zingine zinazokuja za Maji. Mheshimiwa Magufuli atakapokuja hapa na watakapokuja wale wengine wote wataonyesha hizo huduma zitakavyotolewa. Kwa hiyo hili ni jambo jema Mbunge anatukumbusha na sisi tutaendelea kufuatilia. *(Makofi)*

**MHE. ENG. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa kuwa swali la msingi linazungumzia maghorofa katika Jiji la Dar es salaam na Miundombinu mingine na kwa kuwa tarehe 29/3/2013 siku ya Ijuma nyumba ya ghorofa 16 ilianguka katikati ya Jiji Mtaa wa Indira Gandhi na likasababisha maafa makubwa.

Kwa kuwa kuna jengo lingine pacha pale Mtaa wa Indira Gandhi ambalo limetengenezwa kwa ajili ya maafa kwa Taifa yaani janga lingine tunasubiri pale lilitakiwa liwe la ghorofa tisa lakini limejengwa ghorofa 17 Waziri wa ardhi ameshatamka kuwa jengo lile livunjwe wakasema kuwa ipo TAMISEMI waziri Mkuu anaweza kutamka lile jengo livunjwe leo *big result now?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, sasa hivi nitatoa tamko hapa la kuvunja.

**SPIKA:** Ninaomba ujibu kwa kifupi hizo habari.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninamwelewa Mheshimiwa Mbatia anachozungumza baada ya haya matatizo yote yaliyotokea tuliachoagiza ni kwamba tunakagua majengo yote sasa mimi hapa kwenye jibu la hili swali la nyongeza nitoe maelekezo kama wavunje mimi ninaomba Mheshimiwa atuamini sisi tutafuatilia hili jengo pacha analolisema hapa tutalifuatilia ili tuone kama kweli sasa hili sasa linatakiwa liondolewe tutafuatilia na tukiona kuwa tumeridhika na vigezo vyote hivyo tutatoa maelekezo lakini sasa hivi ninachelea kusema hivyo.

**SPIKA:** Tungekushangaa ungesema hivyo. Mheshimiwa Dkt. Kamani swali la nyongeza.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza, ujenzi wa majengo ya ghorofa katika miji inapelekea matumizi makubwa na shughuli za kiuchumi katika miji hii ikiwamo Dar es salaam. Inasababisha pia msongamano mkubwa wa magari ambao hauna maeneo ya maegesho. Je, sasa sijui Waziri Mkuu atatuambia kuna mpango gani maalum wa kuweka maeneo ya maegesho katika Jiji la Dar es salaam ahsante?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kamani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kamani anachosema hapa ni cha msingi kwa sasa ni kama wote Msajiri wa Majengo, *National Housing,* Halmashauri na maeneo mbalimbali moja ya masharti ambayo tunawapa ni kwamba anapojenga eneo la chini litengwe kwa ajili ya shughuli za kupaki na mambo mengine kama anavyosema ni tatizo kwa hiyo hili ni jambo ambalo tunaendelea kulifuatilia kuhakikisha kuwa ujenzi wowote ambao unaendelea pale lazima u take *in to account* hiki alichokisema Dkt. Kamani.

Na. 157

**Kampuni ya Wind ya East Africa Ltd Kufua Umeme wa Upepo Singida**

**MHE. KABWE Z. ZITTO (K.n.y. MHE. TUNDU A. M. LISSU)** aliliza:-

*TIC* ilitoa Hati ya vivutio kwa Kampuni ya *Wind East Africa Ltd* kuendeleza mradi wa kufua umeme wa upepo kwenye Vijiji vya Kititimo na Unyambwa katika Manispaa ya Singida tangu tarehe 28 Mei, 2008 badala yake Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Singida ilimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya kutoa watalaam wakatenge na kupima ardhi ya vijiji vya Kinku na Mungaa kwa ajili ya kampuni hiyo kuendeleza mradi wake, huku Kampuni ya *Wind East Africa Ltd* ikiwa imekwishatengeneza ramani inayoonyesha eneo la mradi ikijumuisha Vijiji vya Ugha, Ugha A na B; Unyankumbi A na B, Kisaki, Mungu Maji na Kisasida katika Manispaa ya Singida.

Lakini tarehe 20 Oktoba, 2011 Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida alikanusha kuwepo kwa kampuni hiyo ya kufua umeme kwenye eneo lolote la Maispaa ya Singida:-

(a) Je, Mkuu wa Mkoa ana mamlaka gani ya kisheria ya kubadilisha eneo la mradi ambao ulishatolewa hati?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya Makanganyiko huo wa maeneo halisi ya mradi huo?

(c) Kama mradi huo utatekelezwa kwenye maeneo yaliyotajwa. Je, Serikali ina taarifa za idadi ya wananchi wa maeneo husika na jinsi watakavyoathirika kiuchumi na watafidiwa vipi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hati ya vivutio *certificate of incentives* Na. 120020 ya tarehe 25 Agosti, 2008 iliyotolewa na Tanzania *Investment Centre* kwa kampuni ya *Wind East Africa Ltd* inaonesha eneo la awali la mradi wa kufua umeme wa upepo ni kititimo na Unyambwa. Hii ilitokana na kipimo cha mwendo kasi wa upepeo cha urefu wa mita 30 kilichojengwa eneo la Kititimo.

Hata hivyo, Kampuni ya *Wind East Africa Ltd* iliona ipo haja ya kufanya utafiti wake katika eneo kubwa zaidi kwa kuweka minara minara mirefu zaidi yenye urefu wa mita 60. Kwa kutumia vipimo hivyo na stadi nyingine imebaini maeneo mbalimbali ambayo yanafaa katika kupata umeme kwa kuvuna nguvu za upepo.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni ilitarajiwa kuwa minara ya upepo ingewekwa katika Vijiji vya Kinku na Mungaa lakini baadaye kampuni hiyo iliamua minara yote miwili iwekwe katika Kijiji cha Mungaa kwanza.

Baada ya upimaji wa miezi kadhaa minara ilihamishiwa katika vijiji vya Ughaugha A na Kisaki. Ili kuwezesha utafiti kufanyika Kampuni ya *Wind East Africa Ltd* iliingia Mkataba na Vijiji husika ya ukodishaji wa maeneo ya ukubwa upatao mita za mraba 10,000. Mikataba hii pia inahusisha masuala ya ulinzi.

Katika utekelezaji wa mikataba hii kwenye kipindi cha utafiti Januari Machi, 2012 kampuni imeshalipa jumla ya shilingi milioni 36 kwenye vijiji vya Mungaa, Ughaugha A na Kisaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tundu Mughwai Lissu lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu Na. 17(7) cha sheria ya uwekezaji Na. 26 ya mwaka 1997, mwenye mamlaka ya kubadilisha eneo ni kituo cha uwekezaji Tanzania (*TIC*). Kwa hiyo, Mkuu wa Mkoa kisheria hana mamlaka ya kubadilisha eneo lililotolewa na *TIC,* na kwa kuzingatia hilo hajabadilisha eneo la uwekezaji kama inavyoonekana katika hati ya vivutio Na. 120020 iliyosainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa *TIC* tarehe 25/8/2008 na ambayo inafafanuliwa zaidi na kifungu Na. 17 (7) cha sheria ya uwekezaji Na. 26 ya mwaka 1997.

Hata hivyo, ikumbukwe kwamba Mkuu wa Mkoa ni msimamizi wa shughuli zote za Serikali katika Mkoa. Hivyo, pale ilipoonekana anaingilia kati (*intervention*) ni kwa sababu ya nafasi na dhamana anayobeba kama Mkuu wa Mkoa.

(b) Mheshimiwa Spika, kinachoonekana kama ni mkanganyiko katika suala hili ni pale ambapo hati ya vivutio inaonyesha kuwa kampuni ya *Wind East Africa Ltd* imepewa eneo la Kititimo na Unywambwa huku kampuni hiyo ikiendelea kufanya utafiti katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge.

Hata hivyo, maelezo ya yaliyotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Singida ni kuwa kinachooendelea ni nia tu kufanya utafiti katika eneo hilo ambapo baadaye zitafuata taratibu za kisheria ili *TIC* iwapatie eneo hilo kama litaonekana linafaa kwa uwekezaji.

(c) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelekezwa katika kipengele (b) hapo juu, kampuni ya *Wind East Africa Ltd* bado inaendelea na tafiti mbalimbali zikiwemo kupima mwendokasi wa upepo *wind speed* na uimara wa udongo *soil stability* kuhimili mitambo ya kuzalisha umeme huo itakapofungwa.

Hivyo, eneo linalofaa kuanza uwekezaji litakapojulikana baada ya kukamilika kwa shughuli za utafiti, Serikali itafanya uthamini wa ardhi na mali za wananchi ili kujua idadi ya wananchi wanaohitaji kulipwa fidia kiasi ambacho kinapaswa kulipwa kwa wananchi hao. Aidha, wananchi wote watakaoathirika kwenye eneo la mradi watalipwa fidia kwa mujibu wa sheria zilizopo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ukiona majibu ya Naibu Waziri (a) na (b) yanajikanganya, Waziri anasema kabisa kwamba Mkuu wa Mkoa hana mamlaka yeyote kwa mujibu wa sheria ya *TIC,* lakini pili, Waziri anasema kwamba ni nia tu ya utafiti. Hatuendeshi nchi hii kienyeji, hakuna nia tu ya utafiti ni lazima kuwe na vibali mahsusi ambavyo vinatolewa kwa ajili ya kufanya *exploration*.

Je, Serikali sasa itaielekeza kampuni hii kufanya utafiti wake katika maeneo ambayo inaleseni ili maeneo mengine ambayo hana leseni labda Serikali iyatangaze kwa watu wengine?

Swali la pili, kuna makampuni mengi sana hivi sasa Singida yanayofanyakazi ya miradi ya umeme ya upepo, lakini wananchi wa Singida, Viongozi wa Singida hawahusishwi kwa namna yeyote ile.

Ni lini Serikali itakaa na Viongozi wa Singida na wananchi wa Singida kuweza kuwahusisha ili kuhakikisha kwamba maslahi ya watu wa Singida yanazingatiwa katika miradi hii yote?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) (K.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, utafiti na uendelezaji wa miradi ya umeme wa upepo ni tofauti sana na uchimbaji wa madini au uchimbaji wa gesi au mafuta. Maana unafanya utafiti wa hewa na upepo unapotokea.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nimekwenda mimi tarehe 19 Aprili, Singida na nimefika katika maeneo haya yote. Nimefanya mikutano ya hadhara katika maeneo haya, nimefanya mkutano wa hadhara Kititimo, tunasema Kititimo lakini mradi upo katika Kijiji cha Kisasida.

Pale wanachosema ni kwamba wamemaliza na pale hakuna mgogoro wowote kati ya wananchi na kampuni inayoendeleza mradi wa pale ambayo inaitwa *Geo Wind Tanzania Ltd.* Kampuni ya *Wind East Africa* yenyewe ndiyo ipo, Unyamikumbi siyo kama inavyosemwa.

Nimefanya Mkutano wa hadhara na wananchi, Mkutano ulifunguliwa na Mwenyekiti wa Kijiji, uongozi wa Kata ulikuwepo, uongozi wa Tarafa uliokuwepo, uongozi wa Wilaya ulikuwepo, uongozi wa Mkoa ulikuwepo, sasa huu ushirikishwaji ambao unasemwa haushirikishwi wananchi nadhani siyo sahihi sana. Kwa sababu wananchi hawakuniambia chochote zaidi ya kusema tunahitaji fidia na kwamba tunataka wawekezaji waje haraka waendeleze mradi huu baada ya utafiti kuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, nimeomba nitoe ufafanuzi wa maswali yote mawili kwa pamoja kama nilivyoweza kufanya. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Chilolo najua umetoka huko Singida.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika ahsante. Kwa kuwa, tunaamini Serikali haipuuzi haki za wananchi hata mara moja, na uongozi wa Singida hili wanalijua na wanalisimamia kikamilifu.

Je, ni lini wananchi hawa watafidiwa hizo pesa zilizobakia na umeme huu wa upepo utawaka lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) (K.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, taratibu za uendelezaji wa baadhi ya miradi kwa kweli ni ngumu na hasa miradi kama hii ya upepo na hasa inapokuwa si Serikali ndiyo inayotoa fedha, tunashirikiana na sekta binafsi. Sekta binafsi zina *logistics* zake, fedha lazima watafute kwa *financers* nje ya nchi, watu wenye mitaji mikubwa, kunakuwa kuna mchakato ambao wakati mwingine si lawama kwa Serikali peke yake sisi tunajaribu ku-*facilitate*, tunawalea vizuri.

Mhehsimiwa Spika, juzi nilipomaliza mkutano kwenye majumuisho na wale wawekezaji wa makampuni yote mawili nilisema nahitaji taarifa ya kila wiki ya uendelezaji. Maana wale wanaenda wanahitaji tu *certificate* zetu ili waende kutembea nazo huko kutafuta fedha hawana chochote.

Kwa hiyo tunaendelea kupambana hivyo hivyo ndiyo maana tulipitisha hapa sheria ya kushirikiana na sekta binafsi katika miradi mbalimbali ya uchumi katika nchi yetu ni lazima tuvumiliane lakini kweli dhamira ya Serikali iko wazi na tunasimamia kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa miradi hii ya upepo ya Singida kwa kweli vikwazo vyote vimewekwa vizuri tunaendelea kwa kasi sana.

Na. 158

**Utekelezaji wa Programu ya REA**

**MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. AHMED M. SHABIBY)** aliuliza:-

Utekelezaji wa *REA* awamu ya kwanza ulikusudia kupeleka umeme Chakwale na Rubeho; na awamu ya pili kupeleka umeme kwenda Madege, Idibo, Lyogwe na Kikunde Kijiji kilichoko mpakani mwa Jimbo la Gairo na Kilindi:-

(a) Je, utekelezaji wa kupeleka umeme Chakwale na Rubeho umefikia wapi?

(b) Kwa kuwa kutoka Chakwale kwenda Madege, Idibo, Iyogwe na Kikunde ni km. 27 tu.

Je mradi huo umo katika awamu ya pili ya *REA* kama Waziri wa Nishati na Madini alivyoahidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby Mbunge wa Gairo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme Kijiji cha Chakwale na Rubeho ni kazi za nyongeza zilizoongezwa katika awamu ya kwanza ya miradi ya umeme vijijini Mkoani Morogoro. Mradi huu unaotekelezwa na Mkandarasi aitwaye *Symbion Power LLC* na unahusisha:-

(i) ujenzi wa njia ya usambazaji umeme msongo wa Kv 33 umbali wa Km 22; na

(ii) ujenzi wa njia ya msongo wa voti 400 umbali wa Km15. Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 2.1.

Hatua iliyofikiwa ni upimaji wa njia pamoja na kuweka alama kwenye njia hiyo kwa asilimia 100.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Gairo Vijijini vinavyotarajiwa kupatiwa umeme katika awamu ya pili ya utekelezaji wa miradi ya umeme chini ya ufadhili wa Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) ni pamoja na Mswaki, Mgera, Kwamaligwa, Mtumbatu, Madege, Idibo, Iyogwe na Kikunde. Kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivi itahusisha:-

(i) Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa Kv 33 umbali wa kilomita 70;

(ii) Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 umbali wa km 40; na

(iii) Kufunga mashine umba *(transfoma)* 17 za ukubwa mbalimbali. Zabuni ya kuwapatia wakandarasi wa kazi hizi ilitangazwa mwezi Desemba, 2012 na kufunguliwa mwezi Machi, 2013. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Naomba kumwuliza Naibu Waziri kwamba hizi bilioni 2.1 ni pesa za ndani au ni pesa za nje?

Lakini swali la pili, katika vijiji hivi alivyovitaja kupitia mpango wa *REA* gharama yake ni shilingi ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, fedha hizi bilioni 2.1 ni fedha ambazo zimepangwa kutekeleza miradi hii kutokana na Bajeti iliyotengwa na Bunge hili katika mwaka uliopita wa fedha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba ni shilingi ngapi katika vijiji tulivyovitaja, kwa sababu bado upembuzi yakinifu unafanyika ili tuweze kujua gharama za mradi, wakati tukishakamilisha hiyo ndiyo tutaweza kufahamu gharama halisi za mradi huo.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ahadi za viongozi wa kitaifa ni ahadi ya Serikali. Makamu wa Rais Dokta Bilal alipotembelea Kijiji cha Chipogolo aliahidi Serikali itawapatia umeme haraka iwezekanavyo, ninaomba kujua kwamba ahadi hii ya Makamu wa Rais itatimizwa lini kuwapatia wananchi wa Kijiji cha Chipogolo umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali ambalo Mbunge ameniulizia mwenyewe ili nijibu mwenyewe maana Chipogolo ipo kwenye Jimbo langu na ninamshukuru sana kwa kufanyakazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, ahadi hii itatekelezwa na ipo chini ya mradi wa *backbone* wa lane tunayojenga ya Msongo mkubwa kutoka Iringa hadi Shinyanga.

Katika mradi huu ni kwamba vile Vijiji vyote ambavyo vitakuwa vinapitiwa na msongo huu vyote vitawekewa umeme kwa hiyo kutakuwa na ushushaji wa umeme kwa kila kijiji ambacho kinapitiwa na mradi huu na vijiji hivyo ni vyote vinavyopitiwa na mradi huu kuanzia Iringa hadi Shinyanga. Kijiji hiki cha Chipogolo ni miongoni mwa vijiji hivyo na juzi nilikuwa pale nimefanya mkutano nataka niwahakikishie wananchi wa Chipogolo kwamba umeme watapata chini ya mradi huu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kuniona ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu uliopita wa bajeti mwaka jana tulipunguza bei ya kuunganisha umeme kwa wananchi hususani kwa nguzo kutoka laki nne mpaka laki na sabini na saba. Hadi hivi leo tunavyoongea hizo nguzo hazipatikani, naomba kufahamu ni kwanini hizo nguzo hazipatikani mikoani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli baada ya kupunguza bei kumetokea mwamko na msisimko mkubwa kwa wananchi wengi kuomba wafungiwe umeme, ukiangalia kwa kasi tunayokwenda nayo kwa kweli ni kubwa hailingani na uwezo wetu katika kutafuta hivi vifaa vinavyotakiwa na hasa nguzo, vifaa vingine havina tatizo hasa ni nguzo.

Tunajitahidi sana hivi karibuni tumeingiza nguzo nyingi sana kiasi ambacho tuna uhakika hakutakuwa na malalamiko hayo tena kwa sababu unavyojua nguzo ni za ndani lakini pia tunaagiza zingine nje ya nchi kwa sababu za ndani peke yake hazitoshi, tunaamini sasa tunaweza tukatatua tatizo hilo la nguzo.

Na. 159

**Fidia kwa Wananchi Waliopitisha Nguzo za Umeme - TAIRO**

**MHE. ALLY K. MOHAMED (K.n.y. MHE. ESTER A. BULAYA)** aliuliza:-

Wananchi wa Kijiji cha Tairo walifanyiwa tathmini kwenye makazi yao ili kupitisha nguzo za umeme kuelekea Ukerewe toka mwaka 2009 lakini mpaka sasa hawajalipwa:-

Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi hawa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mhehsimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa tathmini ilifanyika katika Kijiji cha Tairo wakati wa utekelezaji wa mradi huo. Tathmini hiyo ilishirikisha watendaji wote wa Serikali kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya na Mkoa. Serikali kupitia vikao na Watendaji iliwaomba wananchi kuchangia ardhi na kuwafidia wale tu ambao nyumba zao zingebomolewa na wale ambao mazao yao ya kiuchumi yangekatwa kupisha ujenzi wa njia ya umeme.

Mheshimiwa Spika, tathmini ilipelekwa *TANESCO* kwa ajili ya malipo. Malipo hayo yalikwishafanyika kwa wote waliostahili. Aidha, kumejitokeza malalamiko ambayo yanatakiwa kufanyiwa uhakiki kuanzia ngazi ya kijiji, ambapo walalamikaji waliojiorodhesha kwa Mkuu wa Wilaya ya Bunda kuona uhalali wake ili ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Wananchi wa Tairo walitangaziwa na Shirika la Umeme kwamba wamepelekewa 2.5 bilioni kwa ajili ya kulipwa fidia,

kitu cha ajabu Mkurugenzi ametangaza kwamba amepokea shilingi bilioni 1.2. Je, ukweli upo wapi?

Swali la pili, ni lini shirika lako la umeme litasambaza umeme katika Mji wa Namanyere kwa ajili ya wanachi wangu wa Namanyere kule.

**SPIKA:** Wewe siyo mwaminifu hata kidogo, Naibu Waziri majibu, kwanza swali lake la pili ni jipya. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Amesema kuna mkanganyiko kati ya kiwango ambacho wananchi wanakifahamu au kile kinachosemwa na Mkurugenzi ambacho bilioni 1.2. Nadhani hapa tuchukue takwimu iliyotolewa na Kiongozi aliyepo wa Serikali. Kwa sababu kwa masuala ya wananchi kama tukichukulia kwamba ndivyo wanavyofahamu itatupa shida ingawa nataka niahidi hapa mbele ya Bunge lako Tukufu nitajaribu kufuatilia tuone ukweli wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili ni kwamba lini tutasambaza umeme Namanyere. Kwa Mheshimiwa Keissy ana kila sababu ya kuishukuru Serikali kwa sababu hivi tunavyozungumza juzi tumetoka kuwasha umeme kwenye Wilaya yake ya Nkasi. Kwa hiyo ana furaha nyingi lakini anazungumzia usambazaji zaidi. Basi kadri tutakavyopata fedha na katika miradi hii inayokuja ya *REA* hatutakusahau Mheshimiwa Keissy na kwamba baadhi ya miradi ipo kwenye orodha ya miradi yetu tutakayoitekeleza katika kipindi hiki cha Mwaka huu wa fedha.

Na. 160

**Kuhamasisha Kilimo cha Pamba Nchini**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. CYNTHIA H. NGOYE)** aliuliza:-

Zao la Pamba ni moja ya mazao muhimu sana ya kibiashara yanayolimwa nchini:-

Je, Serikali itakuwa yatari kufanya utafiti na kuwahamasisha wananchi wa Wilaya za Mbarali na Chunya kulima pamba ya kutosha kukiuzia kiwanda cha nguo cha Mbeya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisitisha kilimo cha zao la Pamba kwa Mkoa mzima wa Mbeya tangu mwaka 2000 baada ya kugundua kuwa funza mwekundu *(Red Bollworm)* alikuwa ameshaenea katika vijiji vya Mbala, Kanga, Galula, Magamba, Wanzani na Chang'ombe Wilayani Chunya. Aidha, madhumuni ya karantini hiyo ilikuwa ni kuzuia kisumbufu hicho kusambaa hadi maeneo makuu ya uzalishaji wa mazao ya pamba nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafiti uwepo wa kisumbufu katika zao la Pamba hapa nchini ili kudhibiti uenezi wa visumbufu kwa wakulima. Utafiti wa visumbufu hususani vya funza wekundu katika mikoa ya kusini ulianza msimu wa mwaka 2004/2005, na kumalizika msimu wa mwaka 2007/2008. Utafiti huo ulilenga kuthibitisha kuwepo kwa funza mwekundu katika maeneo ya Karantini, kutathmini kuenea kwake, kutathmini madhara ya kiuchumi na ya kulima pamba katika maeneo yaliyoathiriwa na mtazamo na maoni ya wakulima na maeneo yanayohusika na karantini hiyo.

Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa idadi ya visumbufu vya mmea wa pamba hususani Funza wekundu viliongezeka mwaka hadi mwaka wakati wa kipindi chote cha miaka mitatu ya utafiti. Matokeo haya yaliashiria kuwa Pamba ikilimwa maeneo haya vizumbufu hao wataongezeka kwa kiasi kikubwa na kusambaa maeneo mengine yanayolimwa pamba hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo pia yalionyesha kuwa, kilimo cha pamba katika eneo ambalo kuna Funza mwekundu kinaongeza gharama za uzalishaji ikilinganishwa na kilimo hicho katika eneo lisilo na Funza mwekundu kwani mkulima hulazimika kunyunyizia dawa mara kumi ikilinganishwa na mara sita.

Aidha, uwiano wa faida halisi na gharama za uzalishaji *(Cost Benefit Analyisis)* unaoesha kuwa katika eneo lenye funza mwekundu hata mkulima akinyunyizia dawa mara kumi uwiano ni 0.47 wakati uwiano wenye tija katika uzalishaji wa pamba ni kati ya 1.2 hadi 1.5.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya utafiti huo, kilimo cha pamba katika maeneo ya mikoa ya Mbeya na Rukwa hakitakuwa na tija kwa wakulima kwa sasa. Hata hivyo, Serikali inaandaa mkakati wa kilimo cha pamba aina ya *Bt Cotton* ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa kilimo cha pamba hiyo ambayo ina ukinzani mkubwa na haishambuliwi na Funza mwekundu pamoja na kuvumilia ukame.

Baada ya kufanya marekebisho ya Kanuni za Sheria ya mazingira na kukamilika kwa utafiti huo Serikali itaangalia uwezekano kuruhusu kilimo cha pamba katika maeneo ya Chunya, Ruvuma na Mpanda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu lako refu mno.

Mheshimiwa Mwambalaswa, swali la nyongeza?

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, wananchi wa Chunya, wamesitishwa kulima kilimo cha pamba kuanzia mwaka 2000 na hawana zao lingine mbadala la kujipatia kipato.

Je, sasa hiyo pamba mbadala ambayo, inakinzana na huyo funza mwekundu, wataanza lini kulima? Serikali, itamke hapa.

Mheshimiwa Spika, la pili. Serikali, ilipositisha kilimo cha pamba Wilayani Chunya, kuna vyama vya msingi ambavyo vilikuwa havijawalipa wakulima fedha zao na suala hili limekuwa linaingia na kutoka toka mwaka 2000 mpaka sasa.

Je, sasa Serikali, inasemaje, vyama vya msingi ambavyo wakulima hawakulipwa fedha zao watalipwa lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwambalaswa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nitambue kwamba, Mheshimiwa Mwambalaswa, alishauliza swali kama hili, lakini nimweleze tu kwamba, utafiti huu wa *BT Cotton* utachukua muda mrefu. Kwa sababu, kwa sasahivi tuna mchakato wa kubadilisha Kanuni, ili ziweze kuruhusu utafiti wa *BT Cotton* hapa nchini, ambao ni ubadilishaji wa *Gen (GMO)* na utafiti huo baada ya kuwa umeruhusiwa unaweza kuchukua kati ya miaka 6 mpaka 8. Uzoefu tulioupata kule Burkinafaso, utafiti ulichukua miaka 8 mpaka wakaanza kuruhusu ukulima wa *BT Coton* kwa hivyo, utafiti huo utachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyama vya ushirika. Kama lilivyoishajibiwa swali lake ni kwamba, vyama vya ushirika vyote ambavyo vilihusika na kupata hasara, vilielekezwa na Serikali, viweze kutoa mchanganuo.

Kwa taarifa tulizonazo ni kwamba, vyama vingi vilishakuwa vimelipwa, basi kama kuna vyama ambavyo mpaka sasahivi havijapata fidia, naomba niwasiliane na Mheshimiwa Mbunge, ili tuweze kupata *detail* na tuone ni nini kitaweza kufanywa na Serikali.

Na. 161

**Uchakavu wa Nyumba za Polisi Zanzibar**

**MHE. ASHA MOHAMED OMAR (K.n.y. MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID)** aliuliza:-

Je, Serikali, ina mpango gani wa kufanya ukarabati wa nyumba za Askari ambazo zimechakaa sana, maeneo ya Ziwani, Mwera, Bububu, Chakechake na Mkoani Pemba?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali, inatambua uwepo wa nyumba za Askari Polisi ambazo zimechakaa sana katika maeneo ya Ziwani, Mwera, Bububu, Chakechake Mkoani Pemba na maeneo mengine hapa nchini. Ni azma ya Serikali, kuboresha makazi ya watumishi wake wakiwemo Askari Polisi, kazi ambayo inafanywa kwa awamu kwa ushirikiano na wadau mbalimbali chini ya Mradi wa Maboresho wa Jeshi la Polisi na kwa kuzingatia Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nia hii nzuri ya Serikali, hukwamishwa na ukosefu wa rasilimali fedha za kutosha. Mara fedha zikipatikana Serikali, itazifanyia ukarabati nyumba zilizotajwa. *(Makofi)*

**MHE. ASHA MOHAMED OMAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa mujibu wa Bajeti ya Wizara yako, hutaweza kukarabati nyumba hizo. Je, utaweza kuliambia Bunge Tukufu, ni lini nyumba hizo zitakarabatiwa, ili kuondosha usumbufu wanaoupata Askari wetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukarabati wa nyumba, uchakavu wa nyumba, ni kubwa sana. Ni tabu kwa mimi na mwingine kusema kwamba, tarehe ngapi nyumba hizo zitaboreshwa au zitakarabatiwa. Isipokuwa kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba, tatizo hili tunaliona na tunalifanyia kazi. Kila mwaka tunatenga fedha kwa ajili ya kazi hii kwa hiyo, katika miaka isiyozidi mitano, miwili, mmoja, mitatu, nyumba hizi nazo zitapata zamu ya kukarabatiwa, *inshallah.*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, matatizo ya kwamba, fedha hazipo katika Wizara hii yamekuwa ni mengi. Na kwa kuwa, viko Vituo kwa mfano, Kituo cha Polisi Mkanyageni, hiyo fedha iliyopatikana milioni 20 kikajengwa Kijituo, kimejengwa katika hali ya udhaifu na hivi sasa kimeshavurugika pale, Polisi wanapata tabu. Na kwa kuwa, kuna mambo mengi hivi sasa ambayo Wizara hii haipatiwi pesa.

Kwa mfano, masuala ya *Offender Management Information System,* ambayo katika hali ya uhalifu inayoongezeka hivi sasa Wizara hii au Vitengo hivi Miradi hii ingewekwa ipatiwe pesa. Je, Mheshimiwa Waziri, unaonaje Wizara hii nayo tukiizuwia ikafanye kama vile tulivyoizuwia Wizara ya Kilimo, ili nayo itengewe pesa, furaha utaipata Wizara hii?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, bajeti ya Wizara hii haitoshelezi. Na kuna matatizo mengi ambayo pengine tungepata fedha zaidi tungeyatatua kwa haraka kama tunavyokusudia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa upande wa Bajeti, je, kuzuiliwa itakuwa furaha kwangu; kwangu haiwezi kuwa furaha. Na ninachokumbuka ni kwamba, Kamati ya Kudumu ya Bunge hili, ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii na katika mapendekezo yao walisema kwamba, maeneo mbalimbali ya Wizara hii yaongezewe fedha. Hilo litakuwa kati ya Kamati ya Bajeti na Kamati ya Kudumu pamoja na Bunge zima, lakini si ushauri mzuri kuikataa Bajeti.

Na. 162

**Vijiji Kuwekewa Minara ya Simu**

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Vijiji vya Mgungira, Iyumbu, Ufana na Msosa, Tarafa ya Sepuka na Vijiji vya Iglansoni, Muhintiri na Kinyampembee Tarafa ya Ihanja, viliahidiwa kuwekewa minara ya simu muda mrefu na usanifu wa maeneo ulishafanyika:-

Je, minara hiyo itawekwa lini, ili wananchi wapate mawasiliano ya uhakika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *(UCAF),* inaendelea na tathmini ya kina ya kujua mahitaji ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini, ambapo katika Jimbo la Singida

Magharibi, hususan Vijiji vilivyoko katika tarafa za Sepuka na Ihanja, Kata za Mgungira, Muhintiri na Mwaru, vitanufaika kwa kupata huduma ya mawasiliano kufuatia matokeo ya zabuni iliyotangazwa na Mfumo huo, mwezi Oktoba, 2012.

Mheshimiwa Spika, kufuatia matokeo ya zabuni hiyo, tayari kampuni ya simu ya *Airtel* imepewa kazi ya kuweka minara katika Kata ya Mgungira, yenye vijiji 3 na kutengewa ruzuku ya dola za Marekani 166,000; Kata ya Mwaru yenye Vijiji 5 imetengewa ruzuku ya dola za Marekani 178,600. Kwa upande wake, Kampuni ya Simu ya *tiGO,* imepewa kazi ya kuweka minara katika Kata ya Muhintiri yenye Vijiji 6 na kutengewa ruzuku ya dola za Marekani 107,100.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wote zikiwemo kampuni za simu kufanikisha lengo la kufikisha mawasiliano katika maeneo mbalimbali yakiwemo maeneo yaliyoainishwa kama Maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara, ili kuharakisha maendeleo ya uchumi na ya kijamii kupitia huduma za mawasiliano.

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri mwenyewe na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Je, katika awamu ijayo chini ya miradi inayosimamiwa na mfuko wa *UCAF,* ni vijiji gani vitawekewa minara ili waweze kupata mawasiliano ya simu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Vijiji vya Mnang'ana, Mshungua, Irisya, Masutyanga, Kintandaa na Mtunduru, vinapata mawasiliano ya simu, lakini hafifu.

Je, Serikali, itakuwa tayari kuwasiliana na makampuni ya simu yanayohusika, ili kuboresha na kuimarisha mawasiliano haya ya simu, wananchi waweze kufaidika na kazi nzuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohammed Hamisi Missanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nilitaarifu tu Bunge lako Tukufu kwamba, katika awamu ijayo ya *UCAF,* tenda itahusisha Vijiji vyote nchi nzima. Kwa hivyo, sitaweza kutaja vijiji vyote vya nchi nzima, ila Waheshimiwa Wabunge wajue kwamba, tenda itahusisha vijiji vyote nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, jibu la pili katika swali lake la pili, anaulizia kwamba, vijiji ambavyo tayari vina mawasiliano, lakini yanakuwa hafifu; niseme tu kwamba, sehemu zote ambazo zina mawasiliano zinaweza kuwa zinapata mawasiliano hafifu aidha kwa watu kuwa wengi zaidi au kwa mawasiliano hayo kuzidiwa na watu ambao wanapiga simu katika maeneo hayo.

Serikali, kupitia *TCRA,* inasimamia hili na itahakikisha kwamba, maeneo yote yanayopata mawasiliano hafifu wahusika wanahakikisha kwamba, wana-*up grade* kuhakikisha kwamba, mawasiliano yanakuwa si hafifu tena. Kwa hivyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Missanga kwamba, Kanuni zinataka kwamba, mawasiliano yote katika maeneo ambayo ni hafifu yaboreshwe, ili wananchi waweze kupata faida ya mawasiliano.

Na. 163

**Wizi wa Fedha Kwenye Mabenki kwa Njia ya Mtandao**

**MHE. KIDAWA H. SALEH** aliuliza:-

Ukuaji wa teknolojia ya Mawasiliano Ulimwenguni, umeleta faida kubwa kimaendeleo, lakini pia umeleta matatizo yakiwemo wizi wa mabenki kwa njia ya mtandao:-

Je, Serikali, ina mkakati gani wa kupambana na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikakati ambayo Serikali imeweka kupitia Benki Kuu ya Tanzania, ni pamoja na kuzitaka Benki zote kutumia teknolojia ya kisasa ya *Euro Mastercard Visa (EMV Compliant)* ambayo hutumia mfumo wa *Chip Based* na kuachana na mfumo wa kizamani unaotumia *Magnetic Stripe* ambao kwa sasa umepitwa na wakati na ni rahisi kwa wahalifu kuuchezea na kuiba fedha za wateja.

Aidha, hatua nyingine za kukabiliana na tatizo hili ni mabenki kuweka mfumo wa *Anti-Skimming Devices* ambao mfumo huu unazuwia mwizi kugundua namba ya siri ya mteja. Na kwa upande wa Benki ya *NMB* imeamua kusimamisha utaratibu wa *Swapping* uliokuwa unatekelezwa na kampuni ya simu ya *Airtel.* Kupitia mfumo huu *NMB* iligundua kuwa, baadhi ya wafanyakazi wa *NMB* na wale wa *Airtel* ambao sio waaminifu walishirikiana katika kuiba fedha za wateja.

Mheshimiwa Spika, Serikali, kwa upande wa *NMB* ilituarifu kwamba, inatarajia kuanzisha utaratibu wa kutuma ujumbe wa simu kwa wateja wake kupitia simu zao *(Bank Message)* pindi mteja anapofanya muamala, ili yule mwenye akaunti aweze kukubali, kukataa, pamoja na kufahamu kuwa katika kipindi hicho akaunti yake inatoa au inatumika kutoa fedha. Hivyo, basi, hatua zote hizi zinalenga kuzuia wizi unaofanywa kwa njia hii kwa kuwa, akaunti ya mteja itakuwa imeunganishwa moja kwa moja na namba ya simu yake ya mkononi. Aidha, Serikali, imo katika hatua ya kukamilisha Sheria ya Wizi kwa njia ya mtandao *(Cyber Crime Act)* ambayo vilevile itasaidia kupunguza tatizo hili.

**MHE. KIDAWA H. SALEH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu magumu ya ki-mtandao ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Naibu Waziri au Serikali, imekiri kuwa wizi huu hauwezi kufanywa na mtu wa kawaida tu, unafanywa na watu waelewa na mfano uliotolewa ni wafanyakazi wa *NMB* na Shirika la *Airtel* kuwa wanashirkiana kuiba.

Je, ni adhabu gani kali imewekwa kwa wafanyakazi hawa, iwe ni fundisho na katazo kwa wengine wasifanye kosa hili?

Mheshimiwa Spika, la pili. Je, kwa wale wateja ambao wameibiwa pesa zao kupitia kule Mabenki. Mabenki yana utaratibu gani wa kuwarudishia fedha zao zilizoibiwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kidawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, kwa sasa siwezi nikajua adhabu ambayo imechukuliwa, *particularly* kwa *Airtel* pamoja na *NMB.*

Lakini tutakapokamilisha sasa hiyo *Cyber Crime Act,* ndiyo ita-*generalise* adhabu ambazo zitakuwa zinachukuliwa pindi matatizo kama haya yanapotokea kwa *public* nzima. Sasahivi ni *percuiliar* kwa *Airtel* na *NMB* wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini utaratibu wa urudishaji inategemea. Kwa wale ambao waliibiwa fedha zao na wizi wenyewe umetokana na wafanyakazi wa *NMB* pamoja na wafanyakazi wa *Airtel,* hiyo *NMB* inarejesha fedha zake pindi watakapofanya *assessment* yote na kuona kitu gani hasa kilitumika kwa ajili ya hizo fedha kuibiwa, lakini *NMB* inarejesha hizo fedha za wateja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, matumizi ya *new technology* madhumuni yake ni kupunguza matumizi ya rasilimali na kuleta ufanisi katika *productivity.*

Sasa Serikali, inazungumzia nini matumizi haya ya *new technology,* ambayo yaendelee kutumika nchini bila ya kuathiri kwanza ukosefu wa ajira pamoja na ongezeko la *cyber crime?*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kweli, *new technology,* itasaidia sana katika kukuza uchumi wan chi hii, lakini ina athari zake. Na mojawapo ya athari ni kwamba, *technology* mpya ikiingia, basi wafanyakazi au *human resource* nayo inapungua.

Kwa hivyo, hatuwezi kwa kuogopa hili kwamba, tusi-*embrase new technology, new technology* inakuja na lazima tuitumie kwa ajili ya ku-*increase productivity,* lakini vilevile kwa ajili ya ku-*increase productivity,* lakini vilevile kwa ajili ya ku-*increase economy* ya nchi hii. Inakuja, hatuwezi kuizuwia kwa hivyo, lazima iwepo.

Mheshimiwa Spika, lakini pengine vilevile, hii *Cyber Crime Act,* itaelezea jinsi ya kupambana na watu ambao watakuwa wanatumia *new technology* kwa ajili ya kujinufaisha wao binafsi na kuwaumiza wananchi. Kwa hivyo, teknolojia itakuja, hatuwezi ni lazima tui-*embrase* tuitumie katika kukuza uchumi wan chi nchi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 164

**Tatizo la Maji Dar es Salaam**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali imeweka mfumo gani wa kuhakikisha kwamba, mpango maalum 2011 – 2013 wa kuboresha huduma za Maji Safi na uondoaji wa Maji Taka katika Jiji la Dar-es-Salaam uliopitishwa na Baraza la Mawaziri 2011 unatekelezwa kwa wakati na ufanisi kuwezesha mabomba yaliyopo yatoe maji na mtandao usambazwe mpaka maeneo ya pembezoni mwa Jimbo la Ubungo?

(b) Je, ni lini *EWURA* itafanya ukaguzi wa kiufanisi *(Performance Audit)* wa miradi ya Visima vya Maji vilivyochimbwa na Serikali na kukabidhiwa kwa *DAWASCO,* Jumuiya za Wananchi na Taasisi mbalimbali, lakini havitoi huduma inayostahili kwa kadiri ya malengo ya awali?

(c) Je, ni lini Serikali, itawasilisha Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali za Majisafi na Majitaka *(Water Supply and Sanitation Miscellaneous Amendment Bill),* ili kushughulikiwa upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa Sheria zilizopo na kuweka mfumo thabiti wa usimamizi wa sekta ya maji nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, lenye sehemu *(a), (b)* na *(c),* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza mpango maalum wa kuboresha huduma ya maji safi na uondoaji wa maji taka jijini Dar es Salaam kupitia mamlaka ya maji safi na maji taka Dar es Salaam Dawasa.

Katika kutekeleza mpango huo Serikali imeweka utaratibu wa usimamizi na ufuatiliaji wa karibu kwa kuzingatia hadidu za rejea zilizopo kwenye mikataba na ratiba ya kazi. Vikao na ukaguzi wa miradi hufanywa kila mwezi kati ya Wizara, Dawasa, Bodi ya Dawasa, Wakandarasi na Wataalam wa shauri katika maeneo ya miradi ili kudhibiti ubora na kuharakisha utekelezaji.

Mheshimiwa Spika (b), mwezi Desemba 2012 EWURA ilifanya ukaguzi wa kiufanisi yaani *performance audit* wa miradi ya visima vya maji 147 vilivyo chimbwa na Serikali chini ya usimamizi wa Dawasa kati ya visima hivyo visima 80 vilikutwa vinafanya kazi wakati 67 vilionekana kutofanyakazi. Sababu ya visima hivyo kutofanyakazi ni pamoja na ubovu wa *pump*, kuibiwa kwa *pump*, kupungua kwa maji, kukauka kwa visima, kuwepo kwa madeni ya umeme na migogoro ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, (c) katika kutekeleza sheria ya maji Wizara inaendelea kubaini mapungufu yaliyopo kwenye sheria za maji kwa upande wa sheria ya Dawasa mapungufu kadhaa yamebainishwa na sasa yapo katika hatua mbalimbali za kupitishwa kwenye vikao husika baada ya kukamilika mswada wa marekebisho ya sheria hiyo utawasilishwa hapa Bungeni. Kwa sheria ya huduma za maji na usafi wa mazingira mapungufu kadhaa yamebainishwa na tunaendelea kukusanya maoni kutoka kwa wadau ili tuwe na uchambuzi wa kina baada ya kukamilisha hatua hiyo taratibu nyingine zitafuata ili kuwasilisha muswada wa marekebisho ya sheria hapa Bungeni. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu hayo katika sehemu ya jibu imeelezwa kwamba mfumo huo uliowekwa ni kwa ajili ya kuharakisha utekelezaji lakini mpango huu maalum kwa mujibu wa ahadi ya Rais ya mwaka 2011 ulipaswa kuwa umekamilika mwezi Machi mwaka 2013 ambao umekwisha pita na mpango haujakamilika hali ambayo inaashiria kwamba mfumo huo haujaweza bado kuharakisha utekelezaji.

Sasa kwa kuwa Serikali hii hii imeweza kuweka mfumo wa bomba refu kweli la gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam kujengwa kwa miezi 18 peke yake ni kwa nini bomba la maji ambalo ni fupi sana kutoka Ruvu tu mpaka Kimara pale Dar es Salaam ambayo pesa zipo tayari ni kwa nini kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri inataka kuchukua miezi 48 ni kwanini mfumo ule ule wa uharakishwaji uliotumika kwa upande wa bomba la gesi usitumike kwa bomba la maji ili bomba likakamilika kwa haraka zaidi?

Mheshimiwa Spika (b) kwa kuwa umuhimu wa mfumo huu ni kwa ajili ya kudhibiti vile vile ubora na kwa kuwa kulikuwa na kasoro kubwa za ubora kwenye mradi wa mabomba ya wachina na ndiyo maana hali ipo ya matatizo kiasi hiki.

Ni kwa nini Serikali sasa isiheshimu Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge kwa sababu mimi kama Mbunge nimeiandikia Wizara mara kadhaa kupitia Ofisi ya Katibu wa Bunge kupewa nakala za hii mikataba na ratiba ya kazi ili kuweza kushiriki kwenye kusimamia ubora ni kwa nini Serikali isiheshimu hii sheria na kuweka hii mikataba wazi na ratiba ya kazi wazi ili utekelezaji ukafanyika kwa wakati na kwa ubora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa maji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa John John Mnyika kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimuhakikishie kwamba utekelezaji wa mradi wa gesi na maji ni tofauti hata ukiangalia katika masuala ya ufundi katika gesi na upande wa maji ni tofauti kwa hiyo kwa vyovyote vile masuala ya miradi ya maji shughuli zake za ufundi ni pana zaidi kuliko hiyo anayosema ya gesi.

Lakini pili nimwambie kwamba tukubaliane kwanza angekubali kwamba tulipoweka ule mpango mwaka 2011 tulikuwa na mpango na tukaainisha na Bajeti ambayo ilikuwa ni bilioni 653. Sasa kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali kwa kipindi hicho ni kwamba tulikuwa na miradi mingi. Tulikuwa na mradi wa kutoa maji Ruvu chini kwenda Dar es Salaam, kutoa Ruvu juu na ile miradi ya Kimbiji na Mpera ya visima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni miradi ambayo ilikuwa inahitaji fedha nyingi ambazo zisingepatikana kwa wakati mmoja sasa Serikali imefanya kazi kubwa sana. Imepata fedha za mradi wa Ruvu chini ambao tayari unatekelezwa na kama ule mradi ulipangwa kukamilika mwaka 2013 tayari chanzo chake kinakamilika mwezi wa saba mwaka huu.

Lakini ule mradi wa kulaza bomba unakamilika mwezi wa pili mwaka kesho 2014 tofauti kama ya miezi sita tu pale kwa hiyo tutaanza kupata maji ya nyongeza lita milioni 88 kwa mradi tu wa Ruvu chini lakini mradi wa Ruvu juu tayari utekekelezaji wake umeanza na mwezi wa saba unaanza ujenzi na fedha zimepatikana.

Kwa hiyo, kazi kubwa ya kwanza ya Serikali ilikuwa ni kutafuta fedha ambazo tayari zimepatikana na lazima tushukuru hiyo, sasa utekelezaji ule umeshaanza kutekelezwa na mradi wa Ruvu juu utaongeza lita milioni 114.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukichukua mradi wa Ruvu juu ambao unakamilika mwezi wa kumi na mbili mwaka 2014 na ule wa Ruvu chini tayari itatoa lita milioni 502 ambao ni zaidi ya kiwango cha mahitaji ya Dar es Salaam kwa siku ambayo ni milioni 450.

Kwa hiyo mimi nadhani hapa Mheshimiwa Mbunge angeishukuru Serikali kwamba imefanya kazi kubwa ya kutafuta fedha na utekelezaji umeanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, suala la kwamba ule mradi wa mabomba ya kichina una mapungufu mimi sikubaliani kwamba unamapungufu. Kilichotokea ni kwamba wakati ule mtandao uliposambazwa hatukuwa na maji ya kutosha tulitegemea vyanzo vile vile ambavo vilijengwa miaka ya 1974. Kwa hiyo, tuliweka mtandao maji hayapo kwa hiyo, tukishaweka sasa hivi vyanzo vipya tunahakika kwamba yale mabomba ya mchina sasa yataanza kutumika na yatakapoanza kutumika ndipo tutakapojua kwamba kuna mapungufu kwenye mtandao huu.

Mheshimiwa Spika, lakini uniruhusu niwaombe Wabunge wa Dar es Salaam akiwemo Mheshimiwa John John Mnyika tatizo la maji Dar es Salaam siyo tu uchache wa uzalishaji bali ni upotevu wa maji.

Tumeanzisha *operation* mwezi wa pili ambayo mpaka sasa hivi tumebaini watu 100 wanaoiba maji na wakiwemo kwenye jimbo lake la Mheshimiwa John John Mnyika na niwape mfano mmoja katika wale 100 ambao wamepelekwa mahakamani mmoja ambaye anaitwa Jackson Faustine amekutwa ana shamba la mboga mboga, ana shamba la migomba, ana kiwanda cha matofali, ana baa na boza la kuuza maji ambayo anayagema kwenye mabomba ya Dawasco bila idhini kwa kuiba na kwa siku moja anatumia mita za ujazo 50.2 ambazo ni sawa sawa na mapipa 216 mtu mmoja wakati wengine wanataka maji ya kunywa huyu anamwagilia kwa hiyo kwa aina hiyo ukichukua 100 na ukubwa wake utagundua ni maji kiasi gani yanapotea.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Dar es Salaam tuungane na wafanye maandamano ya kukemea vitendo hivi viovu vya kugema maji kwenye miundombinu ya Dawasco ili wananchi wote wapate maji. Maji yaliyopo yakitumika vizuri kwa kujiheshimu yanaweza yakawasaidia Watanzania walio wengi, ahsante sana.

**SPIKA:** Habari ya mikataba, Mheshimiwa Kafulila muda umeisha.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, suala la mikataba mimi nalichukua tutaliangalia nadhani halina matatizo na tuendelee kuwasiliana na Mheshimiwa Mnyika tuone ni wapi alikwama alipokuwa anahitaji mikataba.

**SPIKA:** Waheshimiwa tumemsikiliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu maji ni uhai lakini muda umepita. Naomba nifanye kueleweka jambo moja. Tulipoanza mwaka huu wa bajeti kamati ya kanuni ilikaa na baada ya kubadilisha mfumo mzima wa namna ya kuripoti Bajeti pia utaratibu wa kuomba uchangiaji tulikubaliana hapa ulibadilishwa. Wabunge wote walipewa fomu za kujaza ni Wizara gani angetaka kuchangia ya kwanza, ya pili, ya tatu tena hatukuweka *limit* ya mwisho.

Kwa hiyo mtu ambaye hakujaza zile fomu na siku inayohusika hata kama Wizara ya Mambo ya Ndani kama katika ile *block* ya Wizara ile wewe hukuomba huwezi kuitwa. Taarifa tulizonazo leo naambiwa Filikunjombe na Mheshimiwa Lugola nimewafunga mdomo mimi kuto kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani. Hakuna mahali walipoomba kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani.

Kwa hiyo, naomba tafadhali tuelewe utaratibu uliopo Waheshimiwa Wabunge kama hukuomba katika Wizara inayohusika huwezi kupata nafasi na kama uliomba na *priority* yako ni ya mwisho sana kama kuna wenzio walikuwa na *priority* ya kwanza na ile mtu ameweka ya kwanza mwingine ya 17 atachaguliwa yule wa ya kwanza na kama wale wa kwanza wote wamekwisha hata huyu wa 17 yumo katika ile *package* ya wale wanaoongea katika Wizara ile.

Kwa hiyo naomba ieleweke kwamba Filikunjombe wala Lugola hawakunyimwa, hawakuomba. Kwa hiyo naomba hii ileleweke. Kwa hiyo baada ya kusema hivyo sasa tunaenedelea, Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Mwaka 2013/2014
### Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Shamsi Vuai atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Selasini, atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia. Baada ya Vuai atafuata James Mbatia halafu Selasini.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu inapita katika kipindi kigumu sana. Migogoro hasa ya kisiasa, kidini na kitendo cha ugaidi ambacho tulichokishuhudia juzi katika mji wa Arusha vinaharibu taswira ya Tanzania kama kisiwa cha amani.

Mheshimiwa Spika, ni rahisi sana kwa sisi viongozi kulaumiana na kumtafuta mchawi, lakini viongozi wenye hekima na busara kama tulivyo sisi hawapaswi kuwajadili watu yanapotokea matatizo. Wanatakiwa wajadili tatizo na *agenda* iliyo mbele yao na *agenda* iliyo mbele yetu ni tatizo la kuvurugika kwa amani katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema huu si wakati wa kulaumiana bali ni wakati wa mshikamano ili tujenge mazingira ya kuwasaka na kuwapata wale waliofanya vitendo hivi. Uongozi ni dhamana kubwa na moja katika sifa kubwa ya kiongozi ni kukubali ukweli hata kwa mambo ambayo hatuyapendi. Tuwe majasiri na tukubali ukweli.

Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kwamba kuna mahali sisi viongozi tumekosea. Tumekosea nini? Unaposikiliza mijadala ya Bunge na Wabunge ndani ya Bunge wakati mwingine kauli zetu haziashirii mema na hatuwezi kushangaa kuyaona haya yanayotokea leo.

Mheshimiwa Spika, kiongozi anaposema jambo ni lazima apime athari ya lile analolisema na tuukubali ukweli kwamba Tanzania ni nchi changa. Kuna mataifa ambayo yana takribani umri wa miaka 300 lakini Tanzania ina miaka 50 tu. Watanzania hawa kutokana na uchanga huu, kutokana na kiwango chetu cha elimu, uwezo wetu wa kuweza kuchambua mambo, si mkubwa sana.

Kwa maana hiyo basi tusiseme tu kila jambo ambalo linatujia kwenye mdomo. Tujikumbushe kilichowahi kutokea pale Rwanda mwaka 1994 mgogoro ule kwa kiasi kikubwa ulitokana na kauli kama hizi kwamba kabila fulani ni baya, kabila jingine ni zuri watu walipoondoka wakaondoka na mapanga. Waswahili husema watu makini na wenye hekima na busara hujifunza kutokana na matukio ya watu wengine.

Mheshimiwa Spika, najua ni vigumu sana mwanadamu kubadilika na kuacha mambo ambayo ameyazoea ni jambo gumu sana lakini mwanafalsafa mmoja wa zamani wa China aliwahi kusema maneno yafuatayo, alisema:-

"Mabadiliko ni jambo la lazima sana katika maisha ya watu. Lakini wako watu wa aina mbili ambao kamwe hawatabadilika. Wa kwanza watu wasiokuwa na hekima na busara wataendelea kushikiria misimamo yao ya zamani hata kama haina maslahi na Taifa lao. Kundi la pili watu wenye busara hawa wataendelea kushikilia misimamo yao, misimamo ambayo ina maslahi ya muda mrefu".

Mheshimiwa Spika, mimi ninahakika sote Waheshimiwa Wabunge tuliopo hapa nina hakika tunataka kuwa katika kundi la pili na wala siyo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ninalotaka kulisema Tanzania ni nchi ambayo ina watu wa makabila tofauti, ni nchi ambayo ina watu wenye imani ya dini tofauti, ina watu wenye itikadi ya vyama vya siasa tofauti.

Napendekeza tu tuwakubali watu kwa ubinadamu wao, kwa mchango wao, kwa uzalendo wao. Lakini mwisho tupendane kwa yale tunayokubaliana, tustahamiliane kwa yale tusiyokubaliana na Kiongozi mmoja wa Marekani aliwahi kusema nyumba ambayo imegawanyika haiwezi kusimama. Mheshimiwa Spika naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mbatia halafu Mheshimiwa Joseph Selasini.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Nianze kwa kutoa pole kwa Baba Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo na Kanisa Katoliki, Balozi wa Vatican Askofu Mkuu Francisco Montecillo Padilla, pamoja na Askofu Mkuu wa Jimbo la Arusha Baba Askofu Josephat Lebulu kwa janga lililotokea juzi jumapili tarehe 5 Mei, 2013.

Mheshimiwa Spika, ni mambo ya kusikitisha sana kwa kuwa Taifa letu ni letu sote Watanzania. Janga likitokea kama lililotokea juzi inabidi Watanzania wote bila kujali imani, rangi, wala dini, wala itikadi tuwe kitu kimoja kwa maslahi ya Taifa la Tanzania. Amani, amani inabidi ilindwe kwa gharama yoyote ile hata ukiangalia Bajeti ya Wizara hii napenda niseme ni kidogo sana kwa majukumu ya kulinda amani ya Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimeshiriki sana kujitahidi chini ya *TCD* kuleta maelewano kati ya migongano ya kidini kati ya vyama vya siasa na Serikali kwa pamoja ni kazi ngumu sana.

Chokochoko ambazo zimeshazama mioyoni mwa Watanzania, kwa kauli za baadhi ya Viongozi, kwa kauli za baadhi ya Watanzania mambo mengine yanasikitisha kwa mfano mauaji yanatokea Katiba yetu Ibara ya 19 inaelezea utaratibu wa imani za kidini.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina Dini kila mtu ana imani yake ya dini,Imani ni jambo binafsi lakini leo hii unaweza ukampigia kiongozi simu hata wengine askari wangazi za juu wa Jeshi la Polisi, unampigia askari simu mlio wake ni wa kaswida na imani yake. Mlio wa simu unakuta mimi ni Abdalah nampigia kiongozi mlio wa simu unalia pepo toka, Abdallah toka"! ningeomba *big result now* Mheshimiwa Waziri kuanzia leo milio kwenye simu zetu tukiwepo Wabunge tunaohudumia Watanzania wote tuondoe kwani tunasambaratisha taifa letu la Tanzania kwa mashindano ya Imani za dini zetu.

Imani ya dini ni jambo la binafsi na hasa vyombo vya Dola vya Ulinzi na Usalam. Sisi ni sehemu ya jamii ambayo jamii inatuangalia tuko wapi tunaipeleka wapi. Ukiangalia kumetokea mgogoro sana, tarehe 11 mwezi wa pili mwaka huu siku ya jumatatu aliuwawa mchungaji Mathayo Kachali kule Geita kwa misingi ya imani za kuchinja.

Ukisoma sheria yetu ya mwaka 2008, iliyosainiwa na Rais tarehe 6 mwezi Desemba mwaka 2008 siku ya jumamosi. *The Animal Welfare Act*, No.19, 2008. Kifungu cha 29 na 30 kinaeleza utaratibu wa kuchinja. Sasa tunapata kigugumizi gani? Kwani ukishaweka utaratibu mahali, ukishindwa kufuatilia na kusimamia ule utaratibu, iwe ni kanuni, Katiba hata kanuni za Bunge letu tukufu, haki inazaa amani, ukipindisha tu ni vurugu katika Jamii. (*Makofi*)

Inabidi tukubali kwamba dhamana tuliyopewa na Watanzania, waliotuingiza hapa ndani, mimi nakiri kwamba nilitembelea Nchi za *DRC* na Togo mwaka 2005, kukiwa na vurugu. Wenzetu watu wa Zanzibar ukiangalia hata wanapochangia hapa ni tofauti na Bara, kwa kuwa walisha onja vurugu na wanajua machungu ya mauaji yakoje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa moyo wa dhati kutoka sakafu ya moyo wangu, mihadhara hii ya kidini ambayo imedumu zaidi ya miaka 20 sasa tuseme basi imetosha. *Big results now*! (*Makofi*)

Hatuwezi tukaleana hivi hivi, *State is a forceful organ*, ni chombo cha mabavu! Sasa Serikali mnashindwaje kufanya maamuzi? Mnaruhusu tunachochea sisi wenyewe tunashiriki kwenye makanisa haya, tunashiriki kwenye misikiti kuchochea vurugu hizi. Kuna falsafa ya waislamu inasema, ukiona uovu unatendeka zuia, ukishindwa kuzuia kemea, ukishindwa kukemea onesha hata chuki basi! Tunashindwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi nilikuwa nasoma bibilia takatifu. Ukisoma Zaburi ya 1, inasema, heri mtu asiyekwenda katika shauri la wasio haki, wala kusimama katika njia ya wakosaji wala kuketi barazani pa wenye mizaha. Hili Bunge letu ni baraza, lakini tumelifanya Bunge la matusi! tunapeleka taifa hili wapi?(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mama yetu Tanzania mwenye watoto zaidi ya milioni 45, waliohai kwa sasa, tunataka kulifikisha wapi? Nashauri kwamba, tuwe na utulivu, tutafakari pamoja kuna mambo mengine tunaweza tukayasema hapa hadharani, lakini mengine tunatakiwa tujifungie sote bila media kwa pamoja mfano tulete *CD* za mauaji ili tuelimishane vizuri tuko wapi? tunataka kupeleka wapi Taifa la Tanzania? Hili ni jambo gumu kweli kweli, lakini Serikali inatoa majibu mepesi. (*Makofi*)

Asubuhi ya leo nimeuliza swali kuhusu Jengo la ghorofa 17 katikati ya Jiji la Dar es salaam, tukisubiri likianguka, Jeshi la Zima Moto hawana vifaa. Mfano, Jeshi la Polisi tarehe 29 Mwezi Machi mwaka huu siku ya ijumaa, afande Kova Kamanda wa Polisi, Kanda maalum ya Dar es salaam, walihangaika kwa sababu hawana vifaa.

Badala ya kuwawezesha kwa vifaa, Waziri wa Ardhi ameshasema, lakini wao wanasema wanasubiri TAMISEMI. Serikali haina majibu. Kwa nini tunasita wakati tunasema *big result now*! kwa nini tunashindwa kufanya maamuzi? Tuna tatizo gani?

Yaani tusubiri mauaji yatokee! Mauaji ya raia mmoja wa Tanzania hayana thamani, huwezi ukanunua uhai wa Binadamu. Tarehe 29 mwezi wa tatu walikufa zaidi ya watu 36, wengine zaidi ya 20 walijeruhiwa vibaya sana. Kwa nini hatufanyi maamuzi na ni kwa gharama ya nani?

Nawaomba Watanzania na nawatia moyo kwamba viongozi tukae pamoja, vyama vyenye uwakilishi Bungeni, Serikali, Viongozi wa Dini pande zote waislamu na wakristo na tusiwe wepesi wa kunyosheana vidole. Hapana! Mauaji ya tarehe 17 Aprili mwaka huu 2013 ya *Padre* Evarist Mushi, nilishiriki kwenye maziko yake, viongozi wamekata tamaa! Unapoona Baba Askofu anasema hapana, huu siyo mpango wa Mungu, sasa inatosha basi! Wafanye nini?

Tusiwaruhusu viongozi wetu watupeleke huko, unapoona kwamba hali inazidi kuwa mbaya na sisi tunashabikia, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wa pande zote, ndimi zetu, kauli zetu zitaliangamiaza taifa la Tanzania. Tusije tukashangaa miaka mitano/kumi ijayo tunapelekwa *the* Hague kwa kauli zetu za uchochozi wa mauaji ndani ya Taifa la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumefika mahali tuseme makosa yetu ya jana japo yasikitisha sana ni mafundisho yetu ya leo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA**: Ahsante, kengele ya pili hiyo!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ni kengele ya kwanza!

**SPIKA**: Ni ya pili!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi uliyonipatia. (*Makofi*)

**SPIKA**: Ahsante, afadhali tupelekwe *the* Hague lakini tutakwenda motoni! Mheshimiwa Joseph R. Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Nassib S. Omar, halafu Mheshimiwa Shibuda!

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nichukue nafasi hii kutoa salamu za pole kwa baba askofu Josephat Lebulu, Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo kuu la Arusha na waumini wote wa Kanisa Katoliki Jimbo kuu la Arusha kwa ajali au msiba uliotokea Jumapili iliyopita.

Pia, nichukue nafasi hii kutoa pole kwa wakazi wa Dar es salaam, Balozi wa baba Mtakatifu nchini pamoja na Rais wa Baraza la Maaskofu katoliki Tanzania, baba Akofu Tarcisiuus Ngalekumutwa na Baba *Cardinal Polycarp* Pengo kwa msiba huu na tafrani hii iliyotokea.

Mheshimiwa Spika, tukio la Arusha limeishitua nchi yetu na bila shaka limeishitua Dunia. Kilichotokea Arusha siyo utamaduni, siyo desturi, siyo jambo ambalo limezoeleka na Watanzania. Kwa sababu hiyo, naomba nitoe wito kwanza kwetu sisi Wabunge lakini pia kwa Watanzania wote, kwamba huu siyo wakati wa kutupiana lawama, hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili lazima tuhakikishe kwamba tunashirikiana kurejesha utulivu katika Jiji la Arusha na katika nchi yetu pia. Ni lazima tuchunge ndimi zetu, wote kabisa. Viongozi pamoja na sisi wananchi naomba tuanzie hapa Bungeni lazima tuchunge ndimi zetu kwa sababu tunayo zamana kubwa ambayo tumepewa na Watanzania. Hakuna sababu ya kuanza kunyosheana vidole, hakuna sababu ya kuanza kupiga ramli, kwamba jambo hili ni la kisiasa au ni la dini.

Ninatoa wito kwa yeyote anayejua kwamba jambo hili ni la kisiasa ashirikiane na wanaofanya uchunguzi kupata ukweli wa jambo hili. Yule anayejua kwamba suala hili ni la kidini afanye hivyo. Vinginevyo natoa wito kwa Serikali na nimekuwa nikiwasema hapa kwa muda mrefu. Sheria tumetunga lakini kuna uwoga wa kuzitekeleza sheria zilizopo.

Kama mtu anasema waziwazi kwamba jambo hili ni la kidini, kwa nini asiisaidie polisi ili atoe ushahidi kwamba ni la kidini katika marefu na mapana yapi. Kama mtu anasema kwamba ni la kisiasa, kwa nini asiisaidie polisi hata kama ni kiongozi ili akaeleza ni la kisiasa katika marefu na mapana yapi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo jambo hili linatufundisha kwamba hatuko salama. Tanzania haiko salama tena! Jambo hili linatufundisha kwamba Watanzania tumegawanyika na kwa sababu hiyo ni rahisi kutumiwa na adui.

Mimi nina bahati ya kuchanganyika na Wabunge wa pande zote. Kila mmoja ukisikia kuna mahali anatupia lawama, chini chini siyo wazi. Wengine baadhi yetu tunasema jambo hili limesababishwa na kundi la watu fulani ambao ni sisi viongozi. Mimi nasema hatuko salama, hiyo ni imani yangu mpaka dakika hii. Hakuna mashehe waliokaa mahali wakatengeneza kikundi cha waislamu kuwatukana wakristo, wala hakuna maaskofi waliokaa mahali wakatengeneza kikundi cha wakristo kuwatukana waislamu.

Ninachoamini wapo wahuni kutoka pande zote mbili na hao ndiyo maadui zetu wanaofanya kazi hii ya kutugombanisha. Hapo ndipo nataka kuwa mkali kawa jeshi la Polisi, kwa sababu wahuni hao wanafahamika, na kwa sababu gani hawakatwi? Tunaogopa nini?

Hizi lugha za kuligawa Taifa hazijaanza leo, hizi lugha zimeanza zaidi ya miaka 20 iliyopita na ninyi polisi ndiyo mnaotowa vibali vya mikutano hii ya kutukana watu. Mtu anasimama hadharani na anasema Serikali hii inaongozwa kwa mfumo Kristo. Hivi ni kweli Rais Jakaya Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anaongoza nchi hii kwa mfumo kristo? Polisi hamsikii?

Serikali haisikii? Kwa nini watu hawa hawakamatwi wakaeleza nchi hii inaongozwa vip kwa mfumo Kristo?

Tumesikia miaka karibu kumi au kumi na tano iliyopita, watu wanasimama Jukwaani wanasema Chama hiki ni cha Waislamu na Chama hiki ni cha wakristo. Huu ni uchochezi, kwa nini watu hawa wasichukuliwe hatua kama wachochezi wengine. Tunawaogopa nini halafu leo tunakaa tunalia kwamba maafa yametokea Arusha.

Mheshimiwa Spika, mimi nachoiomba Serikali sasa ionyeshe kwamba ipo, na ionyeshe weledi wake. Kwanza naitaka Serikali ikamilishe upelelezi wa mauaji yaliyokwisha kutokea. Kwanza kesi ya Shehe Soronga, pili kujeruhiwa kwa *Padre* Mkenda, tatu Mauaji ya *Padre* Mushi na hili la Arusha. Haitoshi tu kusema kwamba tutafanya kazi, lazima ionekane kwamba kazi inafanyika.

Mwisho, ningeitaka Serikali katika hili itunge sheria za kudhibiti lugha za uchochezi hadharani, kwenye majukwaa hata ndani ya Bunge. kama sheria zilizopo hazitoshi, iletwe sheria ya kudhibiti watu wanaloligawa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kuna Wabunge fulani walisimama hapa, wakasema Msingwa huyu anayeongea Mchungaji wa Nguruwe au mchungaji wa Mbwa! Kama nai mchungaji anakundi analoongoza. Hivi anayesema namna hiyo, hafikiri kwamba anawaita wale waumini nguruwe au mbwa! Tunaligawa Taifa sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, mimi kama Mkatoliki, tena najisifu kwa ukatoliki wangu, nataka kuwaambia wakatoliki wenzangu, Askofu Lebulu amesema, jana amesema na leo kasema. Kwamba kwanza tusamehe, lakini pili tuwaombee wanaohusika, tatu tushirikiane na Serikali waharifu wapatikane.

Hivyo ndivyo wakatoliki wote tunapaswa kufanya na mnajua wakisema viongozi wetu wa dini *Roma locuta causa finite* huna sababu ya kuendelea tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoka hapo, nataka niseme kwamba, hakuna mtu anayehoji uwepo wa Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi ni la muhimu kabisa na wala hakuna mtu anayebeza kazi inayofanywa na makamanda na askari ya Jeshi la Polisi.

Tunachosema Jeshi lijitahidi kadiri linavyoweza kujiondoa katika kufanya shughuli zake kibaguzi, hususani katika siasa. Hicho ndiyo kinachosemwa!

Mheshimiwa Spika, kitu kingine tunachosema ni kwamba, mafao ya Polisi yaangaliwe na hili tumelisema muda mrefu sana. Polisi wa ngazi za chini haki zao ziangaliwe, malipo yao, vyeo na posho zao viangaliwe, ndiyo hili tunalolisema. Ingawaje ndani ya Jeshi la Polisi kuna kazi nzuri inayofanywa na kamanda Mwema na wenzake. Sasa hivi wana *SACCOS* ambayo ina uwezo wa zaidi ya bilioni 4 ambayo Polisi wana uwezo wa kwenda kukopa huko.

Sasa hivi wana bima inayoweza kuwapa matibabu wakiwa kazini na wakistaafu. Hayo ni mambo mazuri ambayo yanafanyika na pengine itawasaidia huko baadaye, wale askari wa ngazi za chini waende wakanufaike na mambo haya.

Mheshimiwa spika, kuhusu uhamiaji, ilisemwa jana kuhusu mpaka mrefu wa Jimbo langu Rombo kati ya Tanzania na Kenya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA**: Ahsante sana, sasa nimwite Mheshimiwa Nassib Suleman Omar atafatiwa na Mheshimiwa Shibuda halafu Mheshimiwa Paul Lwanji.

**MHE. NASSIB S. OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru na pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake nyingi juu yetu. Mimi naanza kwanza kwa kutoa pole kwa ndugu na jamaa na wazee wale waliofariki na waliojeruhiwa katika tukio la bomu lililolipuka katika kanisa Katoliki huko Arusha. Mungu atawajalia waliojeruhiwa wapone haraka na waliokufa Mungu awalaze mahala pema.

Kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Selasini tunaitegemea sana Serikali kulifuatilia suala hili ili kuhakikisha wote hawa waliofanya suala hili wanakamatwa na wana adhibiwa vikali. Hatua za mwanzo za Polisi za kuwakamata wale waliohusika zinatia moyo na hivyo waendelee ili waliobakia wote wakamatwe na waadhibiwe.

Pili naunga mkono hatua za Serikali za kukemea vurugu, fujo na uvunjifu wa amani. Vyama vyote vishirikiane ili kujiepusha na kufanya maandamano yasiyokuwa na tija. Kwa sababu mengi ya maandamano haya husababisha fujo.

Mheshimiwa Spika, hatuna budi kuwapongeza jeshi la polisi kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Wamekuwa wakikabilina na maandamano, majambazi kwa kweli mara nyingi wanaumia na mara nyingine wanakufa. Kwa kweli hii ni kazi ya kujitolea na sisi lazima tuwapongeze na kuwapa nguvu ili waendelee.

Pia, tunampongeza Mheshimiwa Rais na nawapongeza wote ambao wamepata nishani kwa kazi nzuri ambayo wamefanya. Nampongeza *IGP,* kamanda Kova na Askari wengine ambao Rais amewatunukia nishani kwa kufanya kazi nzuri katika jeshi la polisi.

Mheshimiwa Spika, polisi pia imeanzisha Polisi Jamii ambayo imesaidia sana katika kuondoa uvunjaji wa amani na uhalifu. Serikali itie nguvu ili hili Jeshi Jamii liendelee kuleta usalama katika vijiji na vitongoji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naingia kwenye matatizo ya Polisi. Bajeti ya mwaka jana, nilizungumzia kuhusiana na nafasi tupu ambazo ziko Polisi, *Head Office,* Zanzibar kuna nafasi ya *Deputy Commissioner* toka mwaka 2004 mpaka hii leo bado haijajazwa. Kadhalika, Tanzania nzima kuna nafasi 540 za *Assistant Commissioners* ambazo bado hawajapandishwa vyeo mpaka hii leo, labda tumwulize Mheshimiwa Waziri anangojea nini? Kazi nzuri wanayofanya Polisi haioni? Atakapowapandisha vyeo na wao ndiyo watapata nguvu ya kufanya kazi zaidi. *(Makofi)*

Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze kwa nini nafasi hizi mpaka leo ziko tupu?

Mheshimiwa Spika, tatizo la Makazi ya Polisi, mimi sitaki kuingia sana katika hili, lakini nitaeleza athari ambazo zimetokezea kwa Askari aliyekufa Bububu, baada ya kumaliza kazi saa sita usiku, Askari huyu alitoka kuelekea nyumbani na njiani aliwakuta wahalifu wakamuua. Laiti ingekuwa Askari hawa wana nyumba, basi tatizo hili lisingetokea. Zaidi ya hayo, kwa nini basi Askari ambao wanapomaliza zamu usiku hawarudishwi majumbani mwao au wapewe silaha waweze kujilinda?

Mheshimiwa Spika, kama hatuna nyumba za kutosha hivi sasa lazima tuhakikishe kwamba, Askari wetu ambao wanatoka zamu usiku tunachukua hatua za kuwalinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la Wastaafu. Mwaka jana pia nilizungumzia suala hili. Kuna Wastaafu wengi sana, wasiopungua 200, ambao sasa hivi haki zao hawajazipata, baadhi yao wamekufa na hapa kwa mfano nina *list* ya Askari 46 wa Zanzibar ambao wameshakufa, wengine toka mwaka 2000. Mimi binafsi nimelifuatilia suala hili *Head Office* ya Polisi kule Dar es Salaam, lakini inaonekana mpaka mafaili yao hayapo. Sasa tumesema mara nyingi kuhusiana na suala hili, wengi wao hawa wana watoto, wana wajane, maisha yao magumu sana ukienda vijijini. Jeshi na Wizara hawachukui hatua zozote kuhakikisha haki zao wanazipata,

kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie kinagaubaga namna gani atalishughulikia suala hili la mafao ya Askari ambao wengine wameshakufa.

Pendekezo langu ni kwamba, aunde Tume ndogo hukohuko Wizarani, ifuatilie masuala haya, ije na *solution* ya kuweza kupata haki zao. Wengi wanakaa Mikoani, wengi wako Zanzibar, inabidi wasafiri kutoka Mikoani mpaka Dar es Salaam, hawana fedha, hawana chochote, kweli itawezekana mtu atoke Mkoani kwenda Dar es Salaam kufuatilia mafao?

Hawa Askari wengi wao wanafanya kazi vizuri, wanategemea baada ya kustaafu watapata haki zao wapumzike na familia zao. Leo wakiona Askari wenzao wamefariki bila kupata haki zao watakuwa na imani ya kufanya kazi kweli? Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja hapa suala hili alipe kipaumbele na atueleze hatua atakazochukua. Tumekubaliana na wenzangu hapa kwamba, Tanzania Bara na Zanzibar tunalisikiliza suala hili vizuri na tutazuia shilingi kipindi hicho utakapokuwa hujajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Askari wetu na Jeshi letu limekwenda Darfur, limefanya kazi vizuri, limerudi, Jeshi letu na Askari Polisi wamekwenda Comoro, wote pamoja wamekwenda kufanya kazi, bado sasa hivi wanaendelea kuweka amani Comoro na wanafanya kazi nzuri. Inapokuja kulipa mafao, Askari Polisi analipwa posho ya shilingi 150,000 wakati Mwanajeshi analipwa shilingi 230,000. Angalia tofauti kubwa iliyokuwepo, kwa nini hili *gap* hatulipunguzi? *(Makofi)*

Wakati zinakuja kufanya kazi za kupigana na nyingine, wote wawili wanakwenda, Jeshi linakwenda na Polisi wanakwenda, lakini mnapowapa mishahara na marupurupu, wao mnawapunguzia; kwa nini?

Mheshimiwa Waziri, naomba suala hili ulifikirie ili utakapokuja hapa walau uwapandishie posho na wao wajihisi kidogo wana nguvu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la rushwa na kubambikiziwa kesi. Hili limeenea sana, hasa *Traffic* ambao njiani ukienda mara nyingi wanajaribu kuwalazimisha madereva kulipa fedha hata kama hawajafanya makosa.

Kwa hiyo, Kamanda, bahati nzuri *IGP* yuko hapa, hili suala tulishughulikie ili tuhakikishe mambo kama haya hayafanyiki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. MAGALE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOHN S. MAGALE:** Vipi tena?

**SPIKA**: Siyo yako hukukopeshwa, endelea tu. Naomba uanze.

**MHE. JOHN P. M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii na mimi niweze kuchangia ajenda iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inatambulisha dhana ya Utawala Bora na Uongozi Bora kwa maslahi ya Jamii. Naomba kushauri yafuatayo:-

Umri wa kustaafu kwa wale ambao wana taaluma ya uelevu maalumu mfano Makomandoo, ni vyema wangeongezewa muda wa kustaafu ili tuondokane na dhana ya hao vijana kuja kushawishika na kuajiriwa kuwa mamruki dhidi ya Raia wa Tanzania. Hivi sasa wapo wastaafu wengi ambao wana taaluma mbalimbali ambazo ni nyeti, lakini umri wao bado ungeweza kutumika kwa maslahi ya

kuongeza ujuzi na uzoefu kwa vijana chipukizi. Naomba suala hilo lipewe umakini na tafakari makini.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuhimiza ya kwamba, ili kupunguza msongamano katika Mahakama zetu na Magerezani, ni bora Jeshi la Polisi wakaajiri watu wenye elimu ya Ustawi wa Jamii waweze kushirikiana na Polisi katika kutatua uhalifu mwepesi unaotokea katika maeneo yetu, badala ya kila kosa linapelekwa Polisi na kutakiwa dhamana na kupelekwa Mahakamani. Mtu akikosa dhamana anapelekwa Magereza, nashauri suala hili lipewe mtazamo mpana.

Mheshimiwa Spika, Bunge ni rufaa ya maslahi ya jamii, kama siyo Kikao hiki kukaa na kutafakari kwamba tuongeze fedha kwa maji na tuongeze pahala ambapo pana upungufu, ninaamini maamuzi magumu kama hayo yalikuwa yanahitajika vilevile katika Wizara hii ili iweze kuongezewa na iweze kutekeleza. *(Makofi)*

Mfano, Wizara ya Sheria na Katiba, tumeongeza fedha za kutumia na kuongeza wafanisi wa kutatua kesi Mahakamani; je, Jeshi la Polisi litaongezwa kiasi gani ili liwe na uwiano wa kwenda na kasi ambayo iko sambamba na uwezeshwaji uliofanywa katika Mahakama? Naomba Serikali ituambie watakuwa na utaratibu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile pana Mradi wa Utambulisho; vitambulisho ni mbegu ambayo itazalisha makusanyo ya mapato makubwa sana. Je, Serikali ina kigugumizi gani? Je, kwa nini Kamati ya Ulinzi na Usalama isilete pendekezo hapa la kuhakikisha kasi ya mwenendo wa vitambulisho inakamilika haraka sana? Faida ya vitambulisho ni Serikali kujitegemea, itapata makusanyo mazuri na itaondokana na udhaifu wa kuwa tegemezi katika misaada kutoka nje. Naomba suala hili Wizara ya hii ije na kauli maalum ya kutuambia wanatatua vipi tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Zimamoto inalaumiwa kila siku ya kwamba, haina uwezo wa kufanikisha uokozi katika

nchi yetu. Nakubali kwamba, Bunge sisi ndiyo watu wa kubeba lawama badala ya Zimamoto kwa sababu hatuna maamuzi magumu katika vipaumbele vya kuona kwamba zimamoto wapewe fungu kiasi gani. *(Makofi)*

Watu ambao wanapata vifo kwa sababu ya ukosefu wa huduma, sisi Wabunge tukubali kulaumiwa na ninaiomba Wizara hii iwe kichocheo na Kamati ya Bunge ije na hoja maalum ya kusaidia zimamoto pamoja na kuimarisha huduma za Magereza ili Magereza iwe sasa ni chuo cha mafunzo madala ya kuwa pahala pa kuendelea na usugu watu wakitoka Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge kuvunja imani ya umma ni rahisi sana, lakini vilevile unapovunja imani kuirejesha ni vigumu. Wizara hii ndiyo hifadhi ya bima ya usalama wa raia na ndiyo mbegu ya usalama wa Taifa letu. Naomba kwanza, nimpongeze *RPC* wa Simiyu, kwa wajibu mzuri anaofanya. Kupitia juhudi anazofanya *RPC* wa Simiyu, naomba kutoa mwito kwa *IGP* pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mje Maswa tutafakari na tusemezane jinsi gani tunaweza tukajenga Makao Makuu ya Wilaya ya Maswa, pamoja na huduma nyingine za Polisi. Kufika kwenu mtakuwa ni chachu na mtaamsha ari ya jamii kwamba iko pamoja nanyi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, bila mazalia ya mbu hakuna maradhi ya malaria. Naomba kusema ya kwamba, panakuwa na vioja na vimbwanga mbalimbali vya kushutumiwa hususan Vyama vya Upinzani, hususan na Wabunge, hususan na Viongozi mbalimbali, lakini, asiyechokoza hakasiriki, kama hakuna jambo ambalo linazaa machukizo na kuzaliwa vimbwanga pasingekuwepo na vimbwanga.

Mheshimiwa Spika, nakuomba, pamoja na Waziri Mkuu, wakati umefika tutafakari tufanye tathmini, ni nini ni mazalia ya machukizo yanayozaa vimbwanga na vioja katika upande wa wahojaji wa Vyama vya Upinzani. *(Makofi)*

Naomba hilo lipewe umuhimu mkubwa sana kwa sababu tusipofanya hivyo, tutakuwa ni watu wa tabia ya kuviziana na kuzomeana na kulalamika, lakini wahenga husema anayechokonoa naye huchokoneka. Kwa hiyo, ndiyo maana mnakuta kuna vimbwanga. Ninashauri na ninahimiza Kamati ya Ulizi na Usalama ya Bunge, iandae ajenda ya kutafakari hatima za kisiasa katika nchi yetu, tutafakari na tushauriane, pana kasoro ambazo upande kuna mazuri ya CCM na kuna kasoro za CCM, kuna mazuri ya Serikali na kuna kasoro za Serikali, kuna mazuri ya Upinzani na kuna kasoro za Upinzani. Yote haya kama tumeyaona na halafu hatutafakari, hatuwezi kukaa kimya mpaka patokee majanga ndipo tunaanza, Viongozi wa Dini, Viongozi wa Madhehebu wakutane. Tuzime moto kabla ya cheche kuumbuka.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ikusanye na ihakikishe kwamba hayo yanatendeka haraka iwezekanavyo. Tutafakari na tusemezane, ni aibu mwenye mali anapoambiwa na mkaguzi wake kwamba kuna wizi unafanyika, kamkasirikia mkaguzi wake. Noamba Vyama vya Upinzani vipokelewe kama doria ya ukaguzi wa Utawala Bora na utekelezaji wa demokrasia na siasa bora. *(Makofi)*

Tukipokea hivyo, basi Chama cha Mapinduzi nawaasa ndugu zangu, mhakikishe mnaposikia machukizo, mnakutana mnatafakari mazalia ya machukizo haya na shutuma hizi ni nini, badala ya kukaa tunazomeana bila kumaliza mazalia ya matatizo. Ni aibu mwenye mali kumzomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Upinzani, kama havitoweza kupewa hadhi na kulelewa, tunaandaa kumbukumbu mbaya za kuzalisha mfumo wa Vyama Vingi na kasoro zake zitakuja kuzaa maovu, ambayo baadaye tujifunze kutoka nchi nyingine, malipizano, malipizano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pana shutuma za kusutwa kasi ya ufanisi wa Jeshi la Polisi, tutaweza kusuta na kutuhumu Jeshi

la Polisi kwa ufanisi wake; lakini tukumbushane kwamba, wakati wa kudai Uhuru wa Tanganyika, *TANU* ilizaliwa kwa sababu ya dhuluma zilizokuwa zinatendwa na Serikali ya Ukoloni, *ANC* dhuluma ya Makaburu, *FRELIMO, SWAPO, Cape Verde*, kote huko, Palestina ni kwa sababu ya mfumo wa uongozi ukiwa na dhuluma, palipo na dhuluma pana mitikisiko na matetemo ya kisiasa. *(Makofi)*

Nashauri tutafakari, tusiwe na tabia ya kutumia Jeshi la Polisi kufunika maovu na upungufu ambao ungeweza kutatuliwa kwa kazi ya kisiasa inayopaswa kutekelezwa na Chama cha Mapinduzi.

Kwanza kabisa, napongeza uzuri wa vyombo vyote vya dola na pia muelewe ya kwamba na ninyi mna kasoro ambazo zinasababisha. Ili kasi ya vyombo vya usalama iende vizuri zaidi katika upelelezi, uhusiano rafiki na Watanzania unahitajika kuimarishwa. Kwa hiyo, napenda kusema ya kwamba, Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa, zisiwe mazalia ya machukizo kwa wanasiasa kuhamasisha jamii kulichukia Jeshi la Polisi, tutakuwa na mdorororo wa upelelezi na udodosi wa Jeshi la Polisi.

Kwa hiyo, nashauri kwamba, Jeshi la Polisi watambue kwamba, Siasa ya Vyama Vingi ndiyo sehemu ya mapumlio ya dukuduku mbalimbali. Jeshi la Polisi likisemwa, wasifikirie wanasutwa bali wanapewa viarifu vya taarifa ya kasoro za kuweza kusahihishwa. *(Makofi)*

Jeshi la Polisi nanyi mna deni la kuimarisha *morale* ya Watanzania na kuamsha ari ya mahusiano; hivyo, nawashauri kwamba ulinzi na usalama wa Taifa letu uko juu pia ya uwezo wenu wa *morale* na hamasa mtakazotoa ndani ya jamii. Utawala Bora hamasisheni na kosoweni yale yanayotendeka kwa sababu asiyeziba ufa hujenga ukuta.

Nawaomba ndugu zangu wa CCM, mkubali upungufu unaotokea ukisemwa kutoka upande wa Upinzani, kwa sababu maabara ikisema Mfalme ana minyoo,

haimfedheheshi Mfalme bali inatambulisha udhaifu wa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lilindwe na Serikali dhidi ya kuzuka tuhuma za kuwa na tabia ya kifuniko. Upendeleo wa *DCs*, naomba ueleweke kwamba, ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shibuda, ahsante. *(Kicheko)*

Leo amesema kama mstaarabu mmoja, hata Kiswahili tumekisikia wote, maana siku nyingine wengine huwa hatuelewi Kiswahili.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunitambua. Yale yaliyotokea juzi Arusha na kuwasilishwa kwa Bajeti hii sambamba ni *coincidence* mbaya na hii inatufanya wengi tuzungumze. Tunasahau kwamba, Tanzania siyo kisiwa, matukio kama haya yamewahi kutokea nyuma, mwaka 1998, Ubalozi wa Marekani ulilipuliwa pale Dar es Salaam, Nairobi, halafu kama sehemu ya Dunia hatuwezi kusahau lile tukio kubwa la *11th, September*, *2001* kule Marekani.

Sasa naomba ndugu zangu, tunapozungumzia masuala haya, tujue kabisa kwamba, lolote linaweza kutokea. Toka wakati huo, Dunia haijakaa sawasawa, kwa hiyo, lolote linaweza likatokea, ni kujipanga tu; vinginevyo, kama alivyosema Mheshimiwa Salasini, mimi namuunga mkono katika eneo hilo la kwamba, tusimnyoshee mtu kidole. Nadhani ni kujipanga na *coincidence* hii. Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imesomwa jana na juzi tukio hilo lilitokea! Basi tuone kwamba, eneo hili na hasa Wizara hii inatengewa fedha za kutosha ili iweze kukabili matukio kama haya.

Vinginevyo, tutalaumiana wakati sisi ni sehemu ya Dunia, tumekaa tukizungumza kwa yale mazuri watu

wanaruka wanakwenda Ulaya, wanakwenda wapi, katika muda mfupi na kurudi. Wanasema sasa hivi Dunia imekuwa Kijiji kimoja, wanasahau pia na mabaya yanaweza kutokea katika kipindi kifupi tu, hili ni lazima tulione.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeliomba kwamba, eneo hili la Wizara hii, Askari wataalamu kabisa waweze kuajiriwa, wapate mafunzo ya kutosha. Yanapotokea matukio haya tusitegemee wenzetu wa nje ambao tunashirikiana nao katika maeneo haya, kiasi cha kwamba sisi tukaonekana hatuwezi kumudu mpaka tutegemee watu wa nje.

Sasa hii Bajeti ya bilioni 700, mimi nimeisoma nikaona haitoshi na hasa tunapokumbuka matukio kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashauri kwamba, Bajeti ijayo basi eneo hili lizingatiwe na hasa katika Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama ili waweze kutulinda, watu wetu watulie wafanye kazi zao bila kuhangaika.

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa na wenzangu**,** lakini nikirudi Jimboni kwangu mimi huwa nalalamika kwa sababu Jimbo langu ni kubwa na mara nyingi nimeikumbusha Serikali kwamba, ina kilomita za mraba 18,000 na sehemu kubwa ni mapori. Ni maeneo ambayo yana utajiri mkubwa na uporaji ni mkubwa na wizi wa mali ya umma katika maeneo mbalimbali na rasilimali zake. Sasa tuna vituo viwili tu, yaani Itigi pamoja na Mgandu; ni vidogo.

Mwaka jana niliomba gari la doria, kwa bahati nzuri Serikali ikanisikia wakaniletea gari pamoja na pikipiki katika kuimarisha; nashukuru kwa hilo. Kwa bahati mbaya, gari lililoletwa halikudumu limeharibika na linahitaji matengenezo makubwa, maana sisi wenye vituo vidogo kama hivi linapokuja gari hata kama litakuja jipya mkoani kwa kawaida yale mapya yanabakizwa kwa wakubwa halafu yaliyochakaa ndiyo yanasogezwa kule, hatukatai, kwa

sababu hilo pengine ni utaratibu. Tunachotaka ni gari linaloweza kufanya kazi.

Sasa naomba Wizara hii itoe ufumbuzi wa kudumu kwani huwezi kufanya doria kutoka Itigi ukaenda mpaka Igalula kama huna gari la uhakika. Huwezi kufanya doria kutoka Itigi kwenda mpaka Rungwa, kilomita karibu 200, mpakani mwa Chunya bila kuwa na gari la uhakika. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara hii ijaribu kutuangalia ili tuweze kuokoa mali za watu na tuweze kuokoa rasilimali ambazo kila siku kukicha watu wanajitwalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaomba Wizara ije na mkakati basi itusaidie, maana Mheshimiwa Waziri Mkuu alichangia kiasi cha fedha kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Polisi Itigi. Kwa bahati mbaya, Kituo kile bado hakijaanza. Ilikuwa mwaka 2010 na ninadhani kutokana na ufinyu hasa wa bajeti na hata Kamanda *IGP* Mwema alifika na akaona hali ya Kituo cha Itigi ilivyo. Sasa hatuwezi tukaachiwa Wanasiasa tu, inakuwa kazi ngumu kama hatuna bajeti ya kutosha. Kwa hiyo, ninaomba na ninaiomba tena, Wizara hii itusaidie itenge fedha za kutosha halafu sisi tutawashawishi Wananchi wachangie sehemu inayostahili kwa upande wao, lakini kutuachia tu sisi tuanze mwanzo mpaka mwisho, sidhani kama ni sahihi na hasa kwa Mwanasiasa unapopita unahimiza ujenzi wa Vituo vya Polisi, ufunguzi wa Magereza na kadhalika, wana mtazamo tofauti juu yako wewe, ni kweli kabisa!

Unapopita unahubiri hii habari badala ya kuhubiri habari ya zahanati, shule na mambo mengine, sasa wewe unahubiri zaidi kujenga Vituo vya Polisi, Magereza na kadhalika, kidogo huwa wanakuangalia kwa mtazamo tofauti ingawa ni sahihi kabisa kwamba vitu hivi viwepo kwa ajili ya kuimarisha Utawala Bora na usalama wao wenyewe. Sisi huwa inakuwa ngumu unapowaambia kwamba waanze chini kabisa kujenga vitu hivi wakati kuna mambo mengine watu wetu wana kero kama vile za maji, shule pamoja na zahanati. Kwa hiyo, ninaomba Wizara hii watuangalie kwenye eneo hilo ili waweze kusaidia.

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, wenzangu wamesema sana kuhusu masuala ya posho. Posho za Maaskari imekuwa ni kero, sasa hili linasababisha tatizo lingine la rushwa. Mimi naipongeza sana mikakati ya Wizara hii na hasa katika kuajiri, safari hii wameajiri vijana ambao wamesoma, wamepelekwa kwenye Kata na Kata zetu sasa hivi kila mahali unapokwenda huwezi kukosa Polisi. Katika utaratibu huu wa Polisi Jamii kuwashirikisha Wananchi, tunaona mambo yanakwenda vizuri, lakini tatizo linapokuja kwamba Askari sasa wanaanza kutegemea Wananchi wa eneo alipofika au sehemu ambayo wanaishughulikia; kuna watu wawili au watatu ndiyo wanamfadhili kuweza kuishi, vizuri hapo ndiyo panapokuwa tatizo, kwa sababu hapo pia upotoshaji wa haki unaweza ukaingia, kwa sababu mwenye nacho anaweza kumnunua Askari kirahisi.

Kwa hiyo, naomba eneo hili tuliangalie ili hizi posho watu walipwe kwa wakati, mishahara yao ni midogo lakini kama wanalipwa kwa wakati posho zao wanazostahili, hatuwezi kuwatumikisha hawa watu bure, ni hatari sana, ni sawa na bwana mwenye nyumba ambaye anaondoka asubuhi anamwacha mama anamwambia nikute chakula kipo tayari na hakuacha kitu chochote; sasa atapata wapi?

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana, hili eneo watu wengi tumelizungumza sana, la posho za Askari, kila kukicha na tunapokuja wanatutuma malimbikizo yao. Ninaomba eneo hili liangaliwe na litengewe fedha za kutosha ili tuondoe hii kero.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, napenda kusisitiza kwamba, eneo hili tunaloliwakilisha liangaliwe kwa mapana na marefu. Siyo eneo la kuchezewa na jambo hili mimi ninaamini kabisa Serikali bado haijalifanyia utafiti wa kutosha kujua rasilimali iliyopo pale, Kituo cha Itigi pamoja na Mgandu hakitoshi. Ninaomba waone uwezekano wa kuweka kituo kingine sehemu ya Kitaraka na kama si Kitaraka basi iwekwe Kaskazi mpakani mwa Chaya pamoja na mpakani mwa Wilaya ya Manyoni na Tabora.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CHIKU A. ABWAO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, siku zote nimekuwa nikisema kwamba, Jeshi la Polisi halina matatizo makubwa, matatizo makubwa yanatokana na Viongozi wetu wa Serikali kulitumia Jeshi letu vibaya.

Nimekuwa nikisema hivyo mara zote bila kutaja ni nani Kiongozi ambaye anatumia vibaya Jeshi la Polisi. Leo naona nimtaje kwa sababu hii hali ni ya hatari kwani Kiongozi ambaye anaamua kutumia Jeshi la Polisi kwa makusudi kuvuruga amani kwa Watanzania hafai.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), ndiye analeta shida. Toka mimi nimetangaza nia ya kugombea Jimbo la Ismani, Wananchi wa Ismani hawana amani wala raha kwani wanasingiziwa kesi kila leo ni kwenda Mahakani kuwatoa washitakiwa wa Ismani. Kisa, kwa sababu Chiku Abwao ametangaza nia ya kugombea. Nikienda Ismani anazuia mikutano yangu yote kwa milango ya nyuma, vibali vinakuwa vya shida na tabu mtindo mmoja. Mheshimiwa Lukuvi, Mbunge wa Jimbo la Ismani, anatumia Jeshi la Polisi vibaya. Polisi wamekuwa wakilaumiwa katika nchi hii kwa sababu ya Viongozi kama hawa, Kiongozi ambaye ndiyo nafurahi anakuja namwona na mimi nilipenda awepo hapa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa huyu amekuwa akiwasumbua watu wa Ismani. Wananchi wamekuwa hawana amani, wanasingiziwa kesi na kibaya zaidi anasema kwamba, baadaye wanamwambia lakini wewe unawababambikiza kesi watu wa Ismani kwa sababu ya Chiku Abwao, akija kufanya mikutano Chiku Abwao kitu gani ana uzoefu tu wa kufungua baa! Nashukuru sana Mheshimiwa Lukuvi amekubali kutoa angalau wasifu wangu kidogo, lakini anasahau wasifu wangu mkubwa zaidi ambao

unamsumbua, amesahau angesema kwamba, Chiku Abwao pamoja na uzoefu wa kufungua baa na kunikaribisha nikafungue baa Ismani na Mungu akinijaalia nitafungua, lakini vilevile nina uzoefu wa kumshinda katika chaguzi mbalimbali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa huyu nilimshinda mwaka 1995 baada ya kumaliza biashara yake ya kununua Jimbo la Ismani alileta nguvu zote Jimbo la Iringa Mjini. Nilipambana mwanamke na Mheshimiwa Mfaramagoha Kibasa, akawa Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini. Nina uzoefu kwani nimeshinda tena mara ya pili. Mwaka 2010 baada ya biashara zake za Jimbo tena kufanikiwa alihamishia nguvu zake zote Jimbo la Iringa Mjini, nilipambana mtoto wa kike mpaka Mheshimiwa Msigwa akawa Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini. Uzoefu huu mbona hausemi? Mbona ni uzoefu wa sifa sana na uzoefu mkubwa na uzoefu huu hata Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani anaujua. Kata ya Lizaboni nilipelekwa Kiongozi wa Kitaifa peke yangu, nilipambana Lizaboni mpaka Kata ya Lizaboni tukaichukua, Mheshimiwa Nchimbi alikuja naye alifanya kampeni, nilimshinda na nina uzoefu wa kushinda; kwa nini haya hayasemi?

Wananchi wa Ismani leo wanabambikiziwa kesi hawana amani, Mheshimiwa anashindwa kushughulikia mambo ya msingi ya Jimbo la Ismani, Jimbo la Ismani limempata Mbunge akiwa Waziri toka mwaka 1995 lakini kaangalie hali ya umaskini na shida zilizopo Ismani. Lami yenyewe inayopita sasa Ismani ni ile niliyoanza kuipigania mimi mwaka 1995 ndiyo inapita kutoka Dodoma – Mtera – Iringa. Ismani hawana lami, Kiongozi ni Waziri miaka zaidi ya 20. Umeme unatoka Mtera jirani ya Jimbo la Ismani ambapo sasa umeme ungezagaa Ismani nzima, lakini ameshindwa kuwapigania watu wa Ismani wapate umeme, anapambana na Chiku Abwao, ananitukana mimi kwenye redio eti nina uzoefu wa kufungua baa, nina uzoefu wa kisiasa.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Siyo taarifa, sitaki taarifa nataka kutoa hoja...

**SPIKA:** Mimi ndiyo Mwenyekiti, naona hii taarifa ni ya kampeni sasa ndiyo maana tunasema, maana si kuchangia hicho. Naomba uchangie hoja iliyopo na siyo ya Lukuvi.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, hii hoja ndiyo yenyewe kabisa, nachangia Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Mambo ya Ndani ni pamoja na Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi ndiyo analolitumia Mheshimiwa huyu kuwakamata hawa watu na kuwaweka ndani na kuwasingizia kesi.

Najenga hoja kutia msisitizo kwamba, Wananchi wa Ismani wajue kwamba, nina uwezo wa kumshinda huyu Bwana na nitamshinda kwa rehema za Mwenyezi Mungu. *(Kicheko*)

Afanye mambo ya msingi kama Waziri wa Nchi hii, kuhakikisha nchi yetu inakwenda vizuri, kuna mambo makubwa mengi ya kufanyiwa kazi hapa. Wizara ya Mambo ya Ndani kuna mambo ya kufanyiwa kazi hapa. Wizara ya Mambo ya Ndani kuna mambo mengi yanafanyika na tunataka ashughulikie kama Waziri pia, asaidiane na Mawaziri wenzake ambao wanafanya kazi zao kwa misingi na taratibu zilizowekwa. Watanzania tumechoka kukaa tunaonewa na mimi nasema Wananchi wa Ismani msiwe na hofu kwani Kamanda nipo, nina uwezo wa kushinda na nitafanya kila niwezalo na sitachoka kuwatoa Mahakamani, sitachoka kuwatoa Polisi na nitakwenda kuwajengea ushujaa, nina uwezo wa kuwajengea watu ushujaa. Viongozi wote wa nchi hii wanajua Iringa Mjini wanakuja kwa tahadhali, nani analeta hali hiyo?

Sasa nahamia Ismani, napeleka majeshi yangu Ismani na nitafanya kazi Ismani tuone mwisho wake. Mimi sinunuliki, ulifanikiwa kununua mara mbili una uzoefu wa kununua, sinunuliki; hapatoshi!

Mheshimiwa Spika, sasa narudi kwenye Jeshi la Polisi; siku zote mimi sitaki kuwalaumu Jeshi la Polisi kwa sababu najua wanafanyishwa kazi kwa mashinikizo. Serikali badala ya kuwashinikiza Polisi kutunza uhalifu wao kwa kutumia Jeshi hilo, waliboreshe Jeshi la Polisi, wawajali wapate maisha mazuri, wapate maisha bora na wapate makazi bora. Hayo ndiyo mambo ya msingi. Unapokitumia sana kitu ukitengeneze ili ukitumie muda mrefu, lakini leo Askari wanatumika tu hovyohovyo hawapewi haki zao, wanateseka sana, mishahara yao midogo wala posho zao hazitoshi. Watumieni Jeshi la Polisi pia na kuwajali maisha yao, waweze kuwa Askari bora ambao wanafanya kazi kwa mapenzi makubwa bila kuwa na manung'uniko yaliyozidi.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nijue mpaka sasa Serikali imefikia wapi suala la uteswaji wa Ulimboka na suala la Kibanda; kuna hatua zipi zimechukuliwa mpaka sasa? Hatujaona kitu! Tunataka kujua hao watu ambao waliwatesa Ulimboka na Kibanda wamekamatwa; na kama hawajakamatwa siku zote hizi Jeshi la Polisi linafanya kazi gani?

Tunataka majibu yaliyo sahihi kabisa, waandishi wa habari pia hawana amani katika nchi hii, wananyanyasika wakisema habari njema kutokana na Upinzani wamekuwa wanaonekana kana kwamba na wao wako Upinzani! Mnaleta tabaka katika nchi yetu. Tunataka haki iwe sawa kwa vyama vyote vya siasa.

Mheshimiwa Spika, ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, tunashukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Ndassa.

Kwa sababu umeshamaliza kusema nadhani haitajibiwa; kwa nini ninyi mnaiingilia kazi yangu?

Mheshimiwa Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Nawapongeza wachangiaji waliosema vizuri humu Bungeni, lakini niruhusu nikuombe na kwa kuwa *IGP* yupo hapa, kufuatana na yale yaliyotokea Arusha, kwa sababu wendawazimu wapo wengi, usishangae kwa utaratibu huohuo mbovu wendawazimu haohao, *whether* kwa kutumwa au kwa matakwa yao wenyewe, Bunge lako Tukufu nalo likavamiwa. Hii ni kwa sababu, lipo kwenye *high way,* barabara zinapita huku na nyingine zinapita nyuma, nikuombe sana kwa kipindi ambacho bado tupo hapa, basi ulinzi uimarishwe sana. Kwa sababu hata Arusha, kama kusingekuwa na ulinzi wa kutosha, Polisi wasingekuwepo pale, hata wale waliohusika wasingekamatwa. Kwa kuwa Polisi walikuwepo na ndiyo maana walifanikiwa siku ya kwanza tu kuwakamata wale waliofanya maovu haya.

Mheshimiwa Spika, hata sisi kwenye maeneo yetu kuanzia sasa huku nyuma ambapo mtu anaweza akapita akarusha kitu kitafika humu ndani. Namna ya kuegesha magari nje nikuombe sana, usalama kwenye Bunge hili sasa uimarishwe, kwa sababu watu kule nje wanatuona tunavyozungumza, tunavyosigana humu ndani, kwa wendawazimu huohuo anaweza akasema hebu nenda kawakomeshe hawa waswahili huko ndani. Kwa hiyo, nakuomba sana ulinzi uimarishwe kwenye Jengo la Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze sana Makamanda wote nchi nzima na mikoa yote, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na niwaombe wenzangu hasa sisi Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na kazi inayofanywa na Makamanda wetu wa Polisi na wasaidizi wao huko chini, sioni sababu ya kukaa hapa na kuanza kuwabeza Makamanda hawa. *(Makofi)*

Tunazungumzia ulinzi na usalama, kazi hii inafanywa na Polisi lakini sisi Waheshimiwa Wabunge tunapokuja tunawabeza badala ya kuwatia moyo, hatuwatendei haki. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge kwamba, upo upungufu wa kawaida, lakini tunapowabeza Makamanda wetu hawa, hatuwatendei haki kwani wanafanya kazi ngumu na katika mazingira magumu.

Ukienda Jimboni kwangu, *ODC* mmoja kutoka kwenye Makao Makuu Ngudu kwenda Mwamashimba ni zaidi ya kilomita 120, gari bovu, matairi hakuna, mafuta hakuna, posho ndiyo hizo, sasa nitakuwa mtu wa ajabu leo nikisimama hapa na kumlaumu *OCD* wangu au kumlaumu *RPC* wangu. Naomba sana sisi Waheshimiwa Wabunge, tuisaidie Serikali ili kuwapa moyo hawa ndugu zetu wafanye kazi yao vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, Kitabu chako ni kizuri sana, nakujua huna maneno mengi, ni mtu wa vitendo, wewe pamoja na Jeshi la Polisi punguzeni maneno, vitendo viwe vingi zaidi, Jeshi huwa halina maneno na Polisi ndiyo Jeshi.

Sasa inawezekana na ninyi mtakuwa kama wanasiasa, ukiambiwa songa mbele, wewe songa mbele, hamna kugeuka nyuma. Sasa ndugu yetu Mkubwa wa Polisi, Bwana *IGP,* najua ni mtaalam na mzoefu mzuri sana, hebu tubadilike, tupunguze maneno twende kwenye vitendo zaidi. Ninyi mnafanya kazi kwa kanuni, taratibu na sheria, pale sheria inapokataza kwamba hili haliwezekani, basi lizuilike. Mmetufikisha hapa kwa sababu na ninyi kwa njia moja au nyingine mmekuwa kama wanasiasa. Yote haya yanayofanyika ni kwa sababu na ninyi mmekuwa kama wanasiasa. Kama wewe ni mwanasiasa sijui tufanyeje, lakini hebu tuache wanasiasa wafanye kazi yao ya siasa na ninyi mfanye kazi yenu. Mkifanya kazi yenu inavyotakiwa haya yanayotokea nafikiri hatuwezi kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe lingine kwa Mheshimiwa Waziri; hivi kuna tatizo gani mbona hawa vijana wetu polisi wanapokwenda likizo ambayo ni haki wanakopwa? Kwa nini

wanakopwa? Hata anapoambiwa nenda, akienda akirudi, anakaa mwaka wa kwanza, wa pili, wa tatu na nne bila kulipwa. Hivi unategemea nini kwa huyu Polisi mwenye mshahara wa shilingi 280,000 au 300,000? Hivi kuna tatizo gani katika kumpa stahili yake ya fedha ya likizo mpaka unamkopa, unamwambia nenda na anaporudi humlipi?

Sasa huko ndiyo kumesemwa kwamba wakati mwingine ni kutaka kusababisha waanze kuchukua rushwa. Uwezo upo kwa sababu unajua mwaka huu Koplo huyu, Konstebo au nani huyu anakwenda likizo, unamwandalia haki zake za likizo. Kwa nini mnamruhusu aende likizo halafu ajilipie? Naomba sana Mheshimiwa Waziri, najua ni mchapa kazi mzuri, nilishapeleka barua kwake nafikiri na *IGP* anayo nakala, Jengo la Makao Makuu ya Polisi Ngudu, alikwenda pale Waziri Mkuu kwa bashasha kubwa na ngoma, akafungua lile Jengo, lakini mpaka leo hakuna majibu. *OCD* analala *guest,* Jengo liko pale zuri tu na Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika akalisifia. Lile Jengo mpaka leo limeshindwa kukamilishwa, nimwulize Mheshimiwa Waziri tatizo ni nini? Naomba sana Jengo hili likamilishwe, samani ziwekwe ili Polisi wetu hawa wahamie kwenye Jengo lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo la gari. Napenda nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, Kwimba ni Wilaya kubwa kweli kweli, wengi mnaifahamu. Naomba kama inawezekana basi ipatiwe magari mawili, kama siyo magari basi hata pikipiki za kutosha. Nimesema kutoka Ngudu kwenda Mwamashimba, kutoka Ngudu kwenda Fukalu, kutoka Ngudu kwenda Nkalalu, Malya, Sumve, ni mbali kwelikweli. Ndiyo maana nasema Polisi wa kwangu, siyo wa kwangu kwa maana ya kwangu, wa kwenye eneo langu, ninawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tena tusiwabeze Polisi wetu, wanafanya kazi nzuri mno. Kwa mfano, pale Dar es Salaam wakisema tu leo trafiki wasiende barabarani, hakuna kitakachofanyika Dar es Salaam, kwa sababu magari yatashonana, hakuna gari litakalotembea. Badala ya kufika

hapa na kuwasifia angalau hata kidogo na wao wasikie, tunawabeza, hatuwatendei haki. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Kamanda wa Iringa, namwambia achape kazi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji, dakika tano tano.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu, kwanza, kwa kunijalia afya njema na nikawa miongoni mwa wachangiaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kama walivyofanya Viongozi wangu Wakuu, nami nilaani kwa nguvu zote juu ya matukio ya uvunjifu wa amani katika nchi yetu maana sisi katika *CUF* tunaamini kwamba, amani ya kweli ndiyo msingi madhubuti wa kufika kwenye maendeleo ya kweli katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la udini ambalo limekuwa likizungumzwa ndani ya Bunge letu. Jambo hili sisi katika *CUF* limetugharimu muda mwingi kuwaeleza Watanzania kwamba, sisi hatukuwa chama cha kidini. Nashukuru kwamba, jambo hili sasa linazungumzwa na Wabunge mbalimbali ndani ya Bunge hili, wakionesha kwamba, *CUF* haikuwa na siyo chama cha kidini, ila ilikuwa ikitumiwa kama *propaganda* ya kuua nguvu ya kisiasa ya Chama cha Wananchi *CUF*. Kwa sababu ya ukweli huo, naomba niwaombe Watanzania sasa tumuunge mkono Profesa Ibrahim Haruna Lipumba, Mchumi ambaye dunia inamfahamu, akishirikiana na Mwanasiasa Mkongwe, mwenye busara, Maalim Seif Sharrif Hamad, ili waiokoe Tanzania kwenye dimbwi hili la umaskini wa kutupwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la ajira katika Jeshi la Polisi. Juzi wakati tunazungumzia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tulizungumza hapa kwamba, ajira katika Jeshi na Taasisi zote za Kijeshi kigezo kiwe ni vijana waliopita katika Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Niseme kwamba, kwa kuwa Zanzibar kuna Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), ambalo shughuli zake zinafanana na JKT kwa huku Bara, naomba kwa vijana wa Zanzibar suala la ajira kigezo iwe ni kwa wale waliopita JKU. Naomba jambo hili kwa sababu Vijana wa Kizanzibari inawapa shida kubwa, inakuwa ni usumbufu mkubwa na inakuwa ni kadhia kwelikweli kupata nafasi ya kujiunga na JKT. Naomba sana kwa Zanzibar kigezo kiwe ni kwa wale waliopita JKU. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Ofisi za Kiwilaya za Polisi. Ni jambo linalosikitisha sana, kule Zanzibar Ofisi zetu za Kiwilaya za Kipolisi zimesahauliwa katika masuala ya vifaa vya kutendea kazi ndani ya ofisi. Jambo hili linapekelekea Viongozi wanaosimamia Ofisi zile kuhangaika wenyewe kutafuta vifaa kwa ajili ya matumizi ya ofisi. Jambo hili linasababisha ofisa anapopata uhamisho anaondoka na vifaa vyake akidai kwamba ni vifaa alivyovitafuta mwenyewe na huo ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Spika, suala la posho za askari zikiwemo za kujikimu na hata zile za upelelezi. Jambo hili tunavyofahamu ni kwamba, posho hizi zinatolewa kwa uwiano wa mishahara yenyewe. Katika kipindi cha mwaka 2012, Askari wamepata posho zile zile za zamani, hakukuwa na ongezeko lolote. Naomba niiulize Wizara; malimbikizo haya ya posho yatalipwa lini? Ikiwa hayatalipwa kupitia bajeti hii au hayatarejeshwa; je, mnawaambia nini Askari wetu hawa ambao fedha zao hazijalipwa?

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la magereza. Hapa Tanzania kwa huku Bara tuna Magereza 126. Uwezo wa Magereza haya kubeba wafungwa na mahabusu ni wastani wa watu 29,552, lakini hadi Aprili, 2013 Magereza yetu

yalikuwa yame-*float* kwa kuwa na watu 35,126, tofauti na kile kiwango cha kawaida ni 5,574.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika tano zimekwisha, ahsante.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Khatibu Said Haji, dakika tano.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia nami kuwa miongoni mwa waliopata bahati ya kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze na Askari wa Jeshi la Polisi wanaohusika na kikosi cha *anti-robbery*. Nia nzuri ya Serikali kupitia Jeshi la Polisi kuanzia Kikosi hiki ni kupambana na matukio mbalimbali ya ujambazi. Pamoja na madhumuni hayo, pia wanahusika na makosa kadhaa ambayo ni wajibu wao kuyafuatilia pale yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, leo nataka nizungumzie Askari hawa hasa katika Wilaya ya Tanga Mjini. Askari hawa wamepatiwa usafiri wa pikipiki kwa ajili ya kurahisisha utendaji wao. Cha kusikitisha ambacho nimeona nikiseme hapa kwa kuwasaidia vijana wetu, wana-*deal* zaidi na vijana wa bodaboda badala ya kushughulika na watu wanaojihusisha na makosa ya uhalifu wa ujangili.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea wakati mwingine askari hao hufukuza vijana wa bodaboda na kuwavunja na kuwaumiza. Nina ushahidi wa matukio yasiyopungua mawili pale Tanga Mjini, ambayo yamesababisha ulemavu wa kukatika miguu kwa vijana hawa kutokana na kufukuzwa na Askari hawa. Askari hawa walitakiwa watumie busara zaidi katika kuona kwamba, vijana hawa siyo majambazi bali

wamevunja Sheria za Trafiki. Wakati mwingine ni *helmet*, kosa la shilingi 30,000 linagharimu maisha ya kijana au kusababisha aishi katika hali ya ulemavu maisha yake yote, kwa kukosa kutumia busara. Namwomba Mheshimiwa Waziri, awaambie askari hawa kwamba, katika makosa kama haya, waangalie njia ipi ni sahihi ya kuyashughulikia ili waepushe madhara makubwa wanayopata vijana wetu kutokana na kufukuzana na askari hawa maarufu kwa jina la 'Tigo'. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie suala la pili la wahamiaji katika nchi yetu. Janga la wahamiaji haramu katika nchi yetu limekuwa kubwa na linazidi kila uchao. Hatua kadhaa ambazo zinaonekana kuchukuliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani kukabiliana na jambo hili zinaonekana kushindikana. Nataka niseme kuna taarifa ambazo Serikali inatakiwa izifuatilie. Kuna baadhi ya watendaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani, wamejiingiza katika biashara hii kwa ajili ya maslahi yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kumwomba Mheshimiwa Waziri ni kwamba, wakati mwingine kuna mambo yanayotokea na mnapewa ushahidi ili myafuatilie lakini hatua hazionekani kuchukuliwa. Mfano, katika Mkutano wa Kumi wa Bunge kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alielezea udhaifu wa Kamishna wa Uchumi na Fedha, Makao Makuu, Ndugu Victor Mgonja, anayejihusisha na suala la kutaka Warundi wapewe uraia wa nchi hii kwa njia za lazima. Ushahidi ukatolewa hapa na Mheshimiwa Mbunge, lakini nina imani mpaka leo bwana yule anaendelea na shughuli zake na hatukuambiwa kama taarifa zile zilizotolewa zilikuwa za uongo au ni hatua gani za uwajibishaji zimechukuliwa. Angeanza kuwajibishwa huyo mkubwa na wadogo wangeogopa, lakini mkubwa anapotoa amri kwa watu wa chini yake kwamba toeni uraia kwa Raia wa Burundi ambao hawana sifa na mfanyakazi wa chini anapokataa anapewa adhabu na hatua hazichukuliwi.

Mbunge anatoa ushahidi hapa Bungeni, Waziri anakabidhibiwa na hakuna hatua inayoonekana kuchukuliwa, kwa kweli hii inasikitisha sana. Sisi Viongozi tuanze

kuonesha mfano wa kuwajibika ili wale wa chini waweze kuiga. Naomba tupate jibu sasa ni hatua gani ambazo zilichukuliwa kwa Kamishna huyu Peter Mgonja, kwa kujihusisha na biashara hii haramu ya wahamiaji haramu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka nizungumzie suala ambalo linagusa vichwa vyetu. Nitoe pole sana, ni jambo ambalo kila Mtanzania linamsumbua kichwa juu ya kwa nini mambo haya yanatokea katika nchi yetu Tanzania yenye neema ya amani!

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, wakati mwingine Vyama vya Siasa, Viongozi, haya ni matokeo ya yale mnayoyasema bila kufikiria athari zake, ndiyo kwa sababu ananyanyuka mwanasiasa anakitaja chama fulani ni chama cha kidini. Leo nashukuru mapenzi ya dharura yaliyotokea hapa kwa Mheshimiwa Tundu Lissu kuisemea *CUF*. Haya mapenzi ya dharura sisi yametufurahisha. Leo anasema *CUF* kilisemwa ni Chama cha Kidini, lakini hata wao walipalilia hili kueneza *CUF* ionekane ni Chama cha Udini. Kuna mshairi mmoja Abdulaziz aliimba akisema, kilicho chema ni chema hakibadili tabia, ni bure mkakisema na mengi kukizulia. Mungu hukipa neema na amani kukitia. *CUF* itadumu na ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, zilikuwa dakika tano. Sasa namwita Mheshimiwa Aggrey Mwanri, atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Khalifan Barwany na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo atafuatia.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu wa mawazo hasa kuunga mkono hoja ambayo imeletwa hapa na Waziri wetu wa Mambo ya Ndani

ya Nchi, Dkt. Emmanuel Nchimbi. Kwa vile najua kwamba, ninaweza nikaingia spidi hapa, naomba nitamke waziwazi kwamba, namwunga mkono na ninaiunga mkono Hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, toka jana mpaka leo tunavyozungumza hapa, mambo mengi yamezungumzwa kuhusu Taifa letu. Kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya yangu ya Siha, napenda kutoa pole sana kwa Kanisa Katoliki pale Arusha, eneo la Olasiti ambapo mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya pale, na-*declare interest*. Nawapa pole sana kwa yale yote yaliyotokea pale.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamezungumza na sisi sote tukisikiliza mazungumzo yaliyosemwa hapa, tunaelewa kabisa kwamba, kuna hazina kubwa ambayo ikitumika vizuri inaweza ikalisaidia sana Taifa letu. Najua Dkt. Nchimbi pamoja na *IGP,* wanaweza wakajisikia vibaya, lakini Taifa kama Taifa, liwe ni Wamarekani, Waingereza, Wajerumani, Tanzania, South Africa, wana maadui. Mao alisema kwamba, adui ni mtu yeyote asiyekutakia mema, awe wa ndani, awe wa nje, awe baba yako, awe mama yako, madhali hakutakii mema, ni adui. *(Makofi)*

Kwa mambo haya ya ubeberu tunaweza tukaacha kuyasema hapa tukasema tutakwenda hivi tu, halafu tukafikishwa mahali pa ajabu sana. Mao anatuambia adui yako akikwambia hivyo unavyokwenda ni safi sana endelea hivyo hivyo, liache jambo hilo mara moja halifai. Ukimwona hivi, umeisha m-*characterize* umejua kwamba huyu ni adui yako, hakutakii mema, halafu anashangilia anapiga makofi anasema, Tanzania hivyo mnavyokwenda mnarumbana ni safi sana, endeleeni hivyo hivyo, jambo hilo halifai tuliache mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Mwalimu Nyerere aliposema nchi hii haina dini, watu hawakumuelewa. Leo baba yule amelala Butiama pale, tunamkumbuka na tunajua alikuwa na hoja gani na falsafa gani aliposema kwamba, Watanzania wana dini zao, lakini nchi kama nchi haina dini.

Watu tulimshangaa, leo tunamkumbuka sisi wote hapa. *(Makofi)*

Mwalimu akatuambia kabisa kwamba, Taifa likifika mahali ukaanza kuwa na watu wamefilisika, hawana cha kuwasaidia watu, watakimbilia hapa kwenye ukabila na dini watabana hapo. Akatuambia makabila tuyatumie kwa ajili ya matambiko, ndivyo alivyotuambia baba yule. Kabisa ndicho alichotuambia. Tunagawanyika gawanyika hivi, adui anatafuta kitu ambacho Lenin anakiita *the wicked linkage,* anapita hapo. Akishaona hivi kila mtu anazungumza, hatuwezi kuwa na heshima.

Rais wetu wa kwanza, Baba wa Taifa alituambia ni kweli tukiwa kitu kimoja, tukazungumza lugha moja, kauli moja, haitatuondolea umaskini, haitajenga uchumi, lakini itafanya kitu kimoja; hakuna mtu atakayetudharau na heshima yetu itakuwa ni heshima ya nchi hii na nchi yetu itasimama. Akituona hivi kila mmoja anasema jambo la kwake, kila mmoja anasimama anasema jambo la kwake, lakini huyu mnakaa kila mmoja anamlingishia mwenzake.

Mheshimiwa Spika, sauti yangu hii huwa naiombea msamaha, mimi sina ungomvi, jambo hili ninaliamini. Taifa hili likienda likateketea hivi, sisi tuliomo humu ndani hatutaacha kulaumiwa. Tutaambiwa waliokuwa Viongozi wa wakati ule na waliokuwa wawakilishi wa wakati ule ni hawa waliomo humu ndani, majina yataorodheshwa *and we shall have to stand up and be counted.*

Nataka niseme hapa imezungumzwa habari ya Dola, nikasema Dola, mimi nikashangaa hii Dola niliisoma wapi? Issa Shivji ametufundisha, Dani Wadada Nabudere ametufundisha, tumewasoma akina Lenin, katufundisha. Dola kila siku tuliambiwa hiki ni chombo cha kundi kinachoangalia tabaka, kama *proletariat*, wamekamata nchi hapo ni *dictatorship*.

**SPIKA:** *Microphone!*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nipo vizuri tu, sauti hii hata kama ungewekewa *microphone* si itasikika tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania sisi ni Wakulima na Wafanyakazi, kama Mheshimiwa Nchimbi anakuta vurugu imeingia mahali anakwenda vijijini kuna jambazi linasumbua pale kijijini, halafu unamwambia aende na fimbo tena hatujui maana ya Dola. Dola ni chombo cha mabavu, akienda pale hawezi kusema hivi, naomba tukae chini, naomba tuzungumze, sijui tuelewane na nini, aah, atabamiza kwanza, akimaliza kubamiza ndiyo tutakwenda kuelewana kule mbele na kiwango cha mabavu kitachotumika pale kinategemeana na uhusiano uliopo kati ya tabaka la Wafanyakazi na Wakulima na chombo chenyewe. Kiasi cha nguvu kitachokutumika pale kitategemeana na kiwango cha *resistance* kitachojitokeza pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukimwambia Mwenyekiti wa Kijiji pale au Mtendaji wa Kata unamwambia nenda kakamate pale, nguvu itakayotumika pale kwa sababu asipotumia nguvu atafika mahali pale panaweza kuingia mtafaruku watu wakafariki. Ukikutana na kundi linakwenda kwenye *armoury,* linataka kwenda kubeba silaha, utatumia nguvu kuzuia pale. Nami nataka nisimame hapo niseme Jeshi letu la Polisi linafanya nzuri tulitie moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pakitokea kitu kinaitwa *powerless* ukisema hapa hapatawaliki maana yake nini? Maana yake ni kwamba, unaweza kwenda kwenye shamba la mtu kuvuna mahindi ukaondoka, ndiyo maana ya kutotawalika. Maana yake unaweza kumkuta mtu anafanya biashara ya kuuza samaki amepata hela zake ukachukua samaki wale ukaenda bila kulipa. Maana yake ni kwamba, unaweza kwenda hotelini ukala chakula ukasema ninaondoka hakuna kulipwa, ndiyo maana ya kutotawalika. Ndiyo maana likitokea tatizo lolote lile pa kwanza tutakapo pakimbilia ni Polisi, Polisi itakwenda pale itafanya kazi. Polisi inachoangalia zaidi ni kupima uhusiano uliopo kati ya Wakulima na Wafanyakazi na chombo chenyewe. Kwa sababu hii Dola iliyopo hapa

na *Political Parties* zote kazi yake kubwa ni ku-*capture political power;* ndicho kinachotafutwa.

Mheshimiwa Spika, akishakamata madaraka yale, sasa pale ndipo anaweka chombo wanaviita vikorombwezo ndiyo inaitwa *super structure* inatengenezwa hapo juu, ni pamoja na mawazo na falsafa, ni pamoja na Dola yenyewe umeingiza humu inakaa pale inafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukija humu ndani watu wanasema hivi anachozungumza anazungumza siasa, *politics* ni *reflection* ya *economics na economics ni reflection ya politics.* Hii lazima tuizungumze vizuri, tuelewane humu ndani, akija mtu humu ndani anazungumza habari ya barabara, anazungumza habari ya zahanati, anajua anachofanya hapa. Watu wengine huyu anazungumzia siasa sana, kwani tumekuja hapa kuzungumzia nini, humu ndani tumekuja kuzungumza siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa tumekuja kuzungumza siasa. Kwa hiyo, mimi nataka niweke vizuri hapa kwamba, atakayekuja hapa na kama hapa unataka mtu akose barabara, akose umeme, akose maji, atapiga kelele ni siasa. Max alisema *"Always the economics guys determine the super structure"*. Mwisho wa kunukuu. Linalosemwa hapa juu kama halina msingi wa hapo chini ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tunafanya nini? Nataka tuliweke vizuri hapa, sisi tunashirikiana na Jeshi la Polisi, tunaye Mkuu wa Mkoa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, tunaye Mkuu wa Wilaya ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Katika *level* ya Kata, anayekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi wa Usalama ni Mtendaji wa Kata. Mwenyekiti wa Kijiji ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na Mwenyekiti wa Kitongoji ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaambia haiwezekani mwizi akaingia kwenye kijiji bila kuwashirikisha wanakijiji pale,

akafaulisha mpango ule. Tulichoambiwa hapa nini? Tumeambiwa kwamba, Serikali zetu za Vijiji zishirikiane na Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba, wote tunaondoka kwa pamoja pale. Moja, tumeambiwa kwamba, tuhakikishe tunatoa taarifa. Pili, tumeambiwa kwamba, tuhakikishe tunaanzisha doria. Jana Mheshimiwa Dkt. Chami alizungumza kitu kimoja kikubwa sana, hatukuwa na utaratibu wa kumpokea mtu kwenye kijiji au kwenye kitongoji bila kutoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Kijiji. Kwa nini tulikuwa tunafanya hivyo, tulikuwa tunafanya hivyo ili tuweze kupambanua kati ya mtu ambaye taarifa zimetolewa na ambaye hakutolewa taarifa. Kwa msingi huo, tukaambiwa aliyefanya uhalifu huu ni fulani fulani. Hili jambo tumeliacha hivi hivi *as a result* sasa tumefika mahali kila mtu anaweza kutoka nje kuingia kwenye kijiji.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie; mambo yaliyotokea katika maeneo mengine, yanayotokea Somalia, yaliyotokea Rwanda na Burundi, wala msije mkafikiri hayawezi kutokea hapa Tanzania, kama sisi tuna uhusiano mzuri, tuendelee kumwomba Mungu vizuri sana. Nataka niseme maneno yafuatayo...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** *Time* yako imeisha. Sasa nimwite Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, dakika tano.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, nianze kwa kutoa pole kwa Watanzania wote juu ya hali tete ambayo imejitokeza katika Taifa letu. Hofu imetanda, waumini msikitini, waumini kanisani wapo katika hofu kubwa juu ya usalama wa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, mara moja niliwahi kusema hapa kwamba, Taifa letu linaelekea kubaya. Ni vyema sasa tusiamini tu sisi tuliokuwa ndani ya Jumba hili tuna uwezo mkubwa kufikiri kuliko wale watu wa nje ambao wamechukua

dhamana ya kutuleta sisi hapa. Kuna watu wazuri kabisa, wana uwezo wa kufikiri, wana uwezo wa kupanga na pia wana uwezo wa kuelekeza. Ni vyema sasa tukaitisha Mjadala wa Kitaifa juu ya hatima ya Taifa letu. Hili ni muhimu kwa sasa Mwenyekiti wangu wa Taifa, Profesa Lipumba, tayari ni hoja ambayo anaizungumzia mara nyingi. Tusitazame ndani ya ukuta za Bunge letu, macho yetu yatoke nje ya jumba hili ili kuona hatima ya Taifa letu sasa ipo mahali pabaya.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia katika Kitabu cha Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani, ukurasa wa 24, nimeona juhudi ambazo zinafanywa na Serikali juu ya kudhibiti mauaji ya vikongwe na wazee. Mimi kwa Lugha yangu ya Kiswahili, wazee na vikongwe ni neno moja.

Mheshimiwa Spika, lakini kanzia kubwa katika Taifa letu sasa ni mauaji ya *albino.* Sidhani katika jumba hili kama kuna watu hawafahamu hilo na pia ninastaajabu kwa Waziri kutogusia hata kidogo juu ya athari ambayo ipo takriban zaidi ya miaka minane katika Taifa hili, juu ya mauaji ya *albino* katika nchi hii. Nimeangalia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho, sijaona mkakati wa Serikali kupitia Jeshi la Polisi kuna mkakati gani juu ya jambo hili!

Mheshimiwa Spika, nilipata simu nyingi jana na leo kutoka katika kona zote za Taifa letu, wakihoji kwa nini Wizara ya Mambo ya Ndani haijaeleza mkakati wake wa makusudi katika kudhibiti mauaji ya *albino*. Hamwoni, hamjui, hamtambui juu ya hili au *albino* siyo sehemu ya Taifa hili? Toka juzi mmeanza kuzungumzia mauaji ya Maaskofu hapa, mauaji ya Mapadri, mauaji ya Masheikh na watu katika maeneo ya dini, lakini mmekuwa vipofu na viziwi juu ya mauaji ya *albino* katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja zinajengwa hapa ninaunga mkono hoja, nashukuru, lakini bado hili halijazungumzwa. Tumezungumza sana kama Serikali imeshindwa sasa basi bora Vyombo vya Kimataifa vije viangalie hii hali. Tumeona mauaji ya Zanzibar na mengine, Vyombo vya Kimataifa vimekuja kufanya utafiti. Nani yupo nyuma ya mauaji haya katika Taifa

hili? Kunyamaza kwenu kimya ina maana kwamba, ninyi mpo nyuma ya mauaji haya.

Nashangaa akina mama zangu wapo ndani ya Bunge mnashindwa kuikemea Serikali, watoto wenu wanakufa kila siku katika Taifa letu, wamekaa katika matumbo yenu miezi tisa, mmejifungua kwa uchungu mkubwa, leo *albino* anakufa bado mnyamaza kimya hamuiambii Serikali ni namna gani iweze kuchukua hatua za makusudi juu ya mauaji hayo! Inatia uchungu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tunasema sasa tumewaambieni mara kadhaa mmeshindwa kulishughulikia suala hili, tutavuka mipaka ya nchi kwenda kuyaambia Mataifa huko. Maadam mmeshindwa ninyi tutatoka nje ya nchi kwenda kuiambia Dunia kwamba, Serikali ya Tanzania imeshindwa kudhibiti mauaji ya *albino*. Inasikitisha!

Mheshimiwa Spika, mmesahau juzi tulifanya maadhimisho pale Singida, nchi yote inazungumza juu ya *albino,* leo mnakuja na taarifa zetu hakuna kipengele hata kimoja kinachozungumzia mauaji ya *albino* katika Taifa hili; kuna nini hapa?

Mheshimiwa Spika, kuna nini hapa? Mnataka tuamini nini juu ya hili; nani yupo nyuma ya mauaji haya katika nchi hii? Tunaishi kwa hofu, hatuna amani katika nchi yetu; kwa nini?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake, nitashika shilingi ya mshahara wake kama hataelezea Serikali ina mkakati gani juu ya mauaji ya *albino.*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, dakika tano.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nianze kwa kusema kwamba na mimi nitoe pole kwa Watanzania wote kutokana na matukio yaliyojitokeza juzi Arusha.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, matukio yote haya ni matokeo ya matunda ya kauli zinazotolewa kutoka pande zote, iwe ni Chama Tawala au Vyama vya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba, tumefika mahali tumejisahau na tunatoa kauli ambazo haziashirii kulipeleka Taifa hili pahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile niseme kwamba, kuna vyombo ambavyo tumeviacha katika kutekeleza wajibu wake katika Jeshi la Polisi. Kuna chombo ambacho Mheshimiwa Mnyaa leo asubuhi kawahi kukiulizia, hiki ni chombo kinachoitwa *OMIS*, ambao ni Mradi uliopo katika Jeshi la Polisi, ni *Offender Management Information System*.

Mheshimiwa Spika, chombo hiki kina malengo makubwa ya kuweza kudhibiti uhalifu katika nchi, lakini hakijawezeshwa na hakijafanya kazi zake. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba, chombo hiki sasa kinawezeshwa na kinaweza kufanya kazi zake ili kudhibiti uhalifu unaoendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimesema kwamba, vijana ambao wameajiriwa mwaka 2010 Jeshi la Magereza, walimaliza masomo yao ya shahada na stashahada, lakini kiwango chao cha mshahara mpaka leo wanachopokea ni shilingi 219,000. Wanapokea kiwango hiki sawa sawa na mfanyakazi ambaye kamaliza Kidato cha Nne. Sasa nauliza mishahara stahili ya watu hawa watapewa lini?

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni wajibu wa Jeshi la Polisi kutoa vyeo kwa Askari wake kila mwaka. Inavyoonekana, Jeshi la Polisi au Serikali haitoi vyeo hivyo kwa wahusika. Sijui ni kwa sababu ya uwezo au vipi? Sasa kama hawawezeshwi kupewa vyeo, basi wapandishwe angalau madaraja ili

waweze kupandishiwa mishahara na wakati wa kustaafu kazi waweze kupata pensheni ambayo inaridhisha.

Mheshimiwa Spika, lingine, kuna Askari ambao wanastaafu kazi wanapewa stahili zao lakini baadaye wanapewa kazi kwa mikataba ya miaka miwili. Sasa ninachomwuliza Mheshimiwa Waziri; je, hawa Askari wanaostaafu kazi wakapewa stahili zao, wakapewa mkataba wa miaka miwili wa kufanya kazi mishahara yao inatoka katika fungu gani?

Mheshimiwa Spika, vilevile niulize kuna *RPCs* wangapi, *OCDs* wangapi, *RPSO* wangapi, *OSS* wangapi ambao wanatoka Zanzibar wafanyakazi katika Mikoa ya Tanzania Bara? Najua kwamba, kuna Makoplo wengi ambao wanatoka Zanzibar wanafanya kazi Tanzania Bara. Je, vyeo hivi nilivyovitaja wapo wangapi kutoka Zanzibar wanaofanya kazi Tanzania Bara?

Mheshimiwa Spika, kuna Wafanyakazi wa Jeshi la Polisi ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Muda umekwisha. Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, atafuata Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii niweze nami kuchangia kuhusu hoja iliyopo mbele yetu. Sitaki yale ambayo wenzangu wameshayazungumzia. Kwa kuanzia, nampongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, pamoja na timu yake, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kazi hiyo wanayoifanya vizuri, wanaifanya katika mazingira magumu sana na hatarishi.

Mheshimiwa Spika, nina salamu zangu kidogo kwa *IGP,* Mheshimiwa Said Mwema; Mheshimiwa Said Mwema

kabla hajawa *IGP*, Watanzania tulikuwa na shida kubwa sana, tulikuwa tunazongwa sana na majambazi. Majambazi yalifanya kazi, yaani kama vile yapo nyumbani kwao tu. Majambazi yalikuwa yanavamia mabenki muda wowote wanaotaka, iwe usiku iwe mchana. Walikuwa wanaingia Benki kama wanaingia nyumbani kwao wanapora wanatoka, wanaenda benki nyingine, ikawa ni hivyo. Majambazi pia yalikuwa yakiwasumbua sana abiria, walikuwa wanateka sana mabasi. Waliteka mabasi wakadhalilisha wasafiri kwa kuwavua nguo, kuwapora simu, fedha, *just at large* kama vile walikuwa wanafanya kazi nyumbani kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Said Mwema alipopata hii nafasi ya kuwa *IGP*, haikumchukua muda mrefu Watanzania tukawa tunalala usingizi mzuri sana. Kwa hilo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hili ambalo limetokea Arusha, siyo Arusha tu, kumekuwa na siri ya matukio haya, Katibu wa Mufti kumwagiwa tindikali, sijui Ruvuma walitaka kuchoma msikiti, lakini makanisa yanachomwa moto ovyo ovyo, Mapadri wanauawa na nini. Mheshimiwa *IGP*, nakuomba kwa mikakati ileile na kwa mbinu zilezile na ujuzi uleule ulioutumia ili ku-*arrest* ule mtandao wa majambazi, najua mna kazi ngumu na hamna vifaa, vitendea kazi ni vichache, lakini ndugu yangu nakuomba kwa mbinu zilezile uelekeze sasa nguvu zako kwa huu mtandao ambao unataka kutugombanisha Wakristo na Waislam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu haitapendeza watu waendelee kusikia kwamba, Padri kachinjwa, sijui kanisa limechomwa moto, sijui kumekuwa na utaratibu gani, halafu watu wakaanza kuguna. Mimi nakuomba uwe na moyo mkuu usichoke, lakini sisi Wananchi tusimwachie Mheshimiwa Said Mwema peke yake, tumsaidie pale tunapokuwa tumesikia fununu hawawezi wakaingia wahalifu nchini wakapenya mpaka vijijini watu tusijue lolote. Atakayesikia ajitahidi na yeye kutoa taarifa ili hawa watu waweze kushughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi japo bajeti yao ni ndogo, lakini wanafanya kazi ngumu sana. Wanajitahidi kufanya kazi kwa ufanisi, lakini katika mazingira hatarishi na katika mazingira magumu. Ili mtu awe Polisi, lazima awe na vitendea kazi na vitendea kazi tunaweza kusema Ofisi, wawe na magari, lakini wawe na silaha na wawe na *uniform.* Jeshi hili limekuwa likifanya kazi katika mazingira magumu sana. Ukiangalia ofisi walizonazo, wala siyo ofisi zinazoweza kufananishwa na ofisi za idara nyingine.

Mheshimiwa Spika, ukichukulia mfano Ofisi ya Polisi *(OCD)* Bagamoyo, naweza kusema Polisi Bagamoyo hawana ofisi, lile jengo wanalotumia ni nyumba ndogo iliyokuwa imejengwa akapewa Mkuu wa Wilaya fulani ambaye alipoingia akakataa akasema siwezi kuishi katika nyumba hii; ni finyu mno, *ventilation* yake ndogo sana, lakini ndiyo amepewa *OCD* anaitumia na wafanyakazi wake wote. Ukiangalia ile ofisi pamoja na hilo, katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2010/2011, walitengewa fedha ili waweze kujengewa ofisi mpya ambayo ina hadhi ya Wilaya. *Grader* lilikwenda pale likatengeneza, likafanya *leveling,* kuanzia hapo hakuna kitu ambacho kimeshawahi kufanyika na nyasi zimeshaota, bado watu wanahangaika kwenye kile kiofisi kidogo sana.

Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri na kwa sababu niliwahi kumweleza wakati fulani, anieleze atakapokuwa anahitimisha ni lini Polisi Bagamoyo watapewa au watajengewa Ofisi yenye hadhi ya Wilaya? Siyo ofisi tu, magari wanayo, hivi sasa wamepewa magari lakini ni mabovu matengenezo yake inabidi sasa *OCD* apite huku na kule kuomba mchango ili yaweze kutengenezwa. Ile siyo nzuri, inafanya doria isiwe rahisi, doria yake inakuwa ngumu, hawawezi kwenda masafa marefu, lakini magari pamoja na kwamba wanayo mafuta ndiyo kazi. Linaweza likatokea tukio mahali fulani Polisi wanaitwa mpaka wafike kwenye tukio inachukua dakika 45 au saa nzima. Matokeo yake ni lawama kwamba tunawaita hamwonekani, lakini kumbe ni katika kuhangaika kutafuta mafuta ya gari. Nilikuwa naomba basi

watakapokuwa wanatoa *allocation* wapewe fedha za kutosha kwa ajili ya kununua mafuta.

Mheshimiwa Spika, juzi nilipochangia katika Ofisi ya Waziri Mkuu, nilizungumzia kuhusu askari katika mipaka yetu kwamba, hawana silaha. Baadaye niliambiwa kwamba, hawapewi silaha kwa sababu hawana *strong rooms* za kuhifadhi zile silaha *(armoury)*. Mimi najiuliza hizo *strong rooms* zinachukua fedha kiasi gani ili kuzijenga ili silaha ziweze kupatikana zikatunzwa? Mimi nadhani *this time* katika bajeti hii wajitahidi kujenga hizo *strong rooms* ili wale askari waweze kupewa silaha wakae nazo kuliko kukaa wanalinda wakiwa wanatumia marungu tu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu Magereza na msongamano ulioko. Nilipokuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI, nilitembelea Magereza ya Keko, Segerea na Ukonga, nimekuta kuna msongamano mkubwa sana wa mahabusu na wafungwa. Tukichukulia vyumba hivi ni vile vilivyojengwa tangu enzi za mkoloni wakati idadi ya watu nchini ilikuwa ni ndogo sana. Sasa hivi idadi ya Watanzania imekua, tunafikia karibu milioni 45, lakini zile nyumba za kuhifadhia mahabusu bado ni zile zile. Ukikuta chumba ambacho kingechukua mahabusu 40 kinakuwa kimechukua mahabusu hata 100 au 120, mara tatu zaidi, kwa kweli hapo inakuwa siyo vizuri kiafya lakini hata haki za binadamu. Kwa hiyo, misongamano hiyo nadhani waangalie kesi zisikilizwe mapema ili watu wasiwe wanalundikana mahabusu kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Katiba na Sheria kama nilivyokwisha kuomba tena kwamba, Wananchi wafundishwe sheria, ukifanya hili utafungwa miaka kadhaa au utalipa faini au vyote viwili. Watu wakielimishwa elimu ya sheria mbalimbali, elimu ifike mpaka vijijini, wapo watu watakao-*respond* na wapo watakaokwepa hawatakwenda Magerezani. Kwa njia hiyo, hata misongamano itakuwa imepungua sana. Misongamano ikipungua tunaipunguzia hata Serikali mzigo wa kulisha na kununua madawa. Kwa

hiyo, ni vizuri Serikali ikaangalia sheria mbalimbali Wananchi waweze kufundishwa.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia habari za Zimamoto, tunaona Halmashauri nyingi hazina magari ya kuzima moto. Wapo Maaskari wa Zimamoto lakini vitendea kazi hawana. Sasa unajiuliza moto unapokuwa umetokea mahali inakuwaje?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAMIA HASSAN SULUHU – WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Niseme kwamba, toka jana nilikuwa nasikiliza kwa makini kabisa mjadala unaoendelea na kuna mambo nimekuwa nikiyasikia lakini pia nilikuwa nikijifunza. La kwanza, suala zima la ukosefu wa rasilimali fedha unaonyima uwezo kwa Vyombo vyetu vya Dola vinavyofanya uchunguzi wa matukio ya uhalifu, kufanya kazi hiyo kwa umakini na kwa ubora zaidi. Hali ambayo inakwaza kukamilishwa kwa uchunguzi dhidi ya watuhumiwa. Tumekuwa tukisikia Waheshimiwa Wabunge wakiuliza mara kadhaa wale waliohusika na kesi hii wako wapi mbona hatusikii kitu, lakini yote ni kutokana na kuchelewa kwa uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, la pili nililokuwa nikilisikia ni suala zima la rushwa iliyokithiri kwenye Jeshi la Polisi, Mahakama zetu na Idara mbalimbali za Serikali, pamoja na kuwepo kwa usiri uliojengeka katika jamii unaowaokoa wahalifu na kuwaadhibu Wananchi. Lingine ni ukosefu wa imani ya kumwabudu Mungu; hili nimelijaza mwenyewe. Kwa sababu vitabu vyote tunavyovijua; Injili, Taurat, Zaburi na Quran, vyote havina maamrisho ya kusema au kumwamrisha mwanadamu kufanya fujo dhidi ya mwenziwe au kufanya matukio ya uhalifu dhidi ya mwenziwe. Laiti ingekuwa hili tunalifanyia kazi, basi yanayotokea yasingekuwa yanatokea.

Lingine nililojifunza hapa ni kwamba, matokeo yote haya pamoja na hili la kutokumcha Mwenyezi Mungu, ndiyo

yanayoleta uvunjifu wa amani hapa nchini. Sasa kuna Mwanafalsafa alisema uvunjifu wa amani unakuja kwa binadamu kushindwa kufikiri. Mimi nataka niwaulize au tujiulize humu ndani na Watanzania kwa ujumla; je, kweli na mawazo yetu aliyotupa Mungu tumeshindwa kukaa na kufikiri na kulifanyia kazi suala la rushwa lisiwepo nchini?

Je, kweli tumeshindwa kutafuta rasilimali kuwapa Vyombo vya Dola kufanya kazi zetu kwa umakini mkubwa? Je, kweli pamoja na ibada zetu za kila siku za Jumapili na Jumamosi tumeshindwa kweli kumfuata Mungu katika maamrisho yake mpaka tunaifikisha nchi hapa ilipofikia? Kwa hiyo, ningependa Watanzania hebu tujiulizeni hayo na tuone tunafikia wapi.

Mheshimiwa Spika, jana pamoja na leo, kumesemwa maneno mazuri sana. Ndugu yangu, Mheshimiwa Zitto, jana amezungumza vizuri sana. Mheshimiwa Mbatia leo amezungumza vizuri sana, Mheshimiwa Selasini amezungumza vizuri sana, lakini unajiuliza tukisimama hapa tunazungumza vizuri lakini kinachotokea nje ni matendo ya nani; ni matendo yetu sisi Wanasiasa? Matendo ya Vyombo vya Dola? Matendo ya Jeshi? Ni ya nani? Kama tuna mawazo ya kuzungumza vizuri hivi kwa nini tunaifikisha nchi yetu hapa ilipofika? Ni nani akamatwe? Nani ashikwe na nani alaumiwe?

Mimi naomba tulibebe wote kwa pamoja na tujiulize ni kazi ya nani. Kuna suala zima la haki na wajibu, tumekuwa tukidai haki zetu hapa za kulindwa, haki za usalama nchini na haki za aina hiyo kutoka kwa Jeshi la Polisi, kutoka kwa Serikali na kutoka kwa Vyombo vya Dola. Je, tumejiuliza sisi kama Wabunge, kama Watanzania, wajibu wetu ni nini katika kuleta amani ya nchi?

Hatujajiuliza na pengine ni sisi ambao tunakwenda kuchochea na kuleta mfarakano ndani ya nchi. Wajibu wetu ni nini? Haki tunaidai sawa kwa Serikali na Waziri atasimama atujibu, lakini sisi wajibu wetu ni nini? Hakuna mtu ambaye amesema tuna wajibu gani.

Nadhani na sisi tutimize wajibu wetu. Tunapozungumza wajibu, leo asubuhi nilikuwa naangalia magazeti nikaona kwamba, wale raia wa jana ambao tulidai tuambiwe ni akina nani? Magazeti yanasema ni Raia wa Saudi Arabia. Sasa kama ni kweli waliingiaje? Walifikaje? Wanakaa kwa nani? Kama ni hoteli ya akina nani? Ni sisi Watanzania ambao tumewapokea, ambao tumeficha yametokea haya. Je, wajibu wetu Watanzania ni nini kuficha hawa watu walete maovu au ni nini?

Aliyerusha bomu ni mtoto wetu, ni ndugu yetu, ni nani yetu? Hakuna aliyesikia kuna huo mpango? Tumesema nini? Tunataka Jeshi la Polisi wa-*perform miracle* itatoka wapi, hawana *camera in mind* kwamba wanajua hili litatokea kwa hiyo tujipange hivi; ni sisi wa kuwasaidia, lakini hatuwasaidii.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema; "Nguvu za dhana huvunjwa na yakini na yakini haipatikani mpaka kuwe kuna uchunguzi au utafiti ulio imara na ulio makini". Lazima kuwe na utafiti mzuri ili kuipata yakini. Toka jana hapa tumekuwa tukishutumiana, kuna *triangle;* CCM wamesababisha haya, CHADEMA wamesababisha haya, *CUF,* Chama cha Kiislam. Tumekuwa tukishutumiana kwa mambo ambayo hayana uhakika. Mimi naomba tuache Vyombo vya Dola vifanye kazi, Polisi na Idara zao wafanye kazi, Idara ya Usalama wa Taifa wafanye kazi, *Intelligentsia* ya Jeshi wafanye kazi, ili kwa pamoja wajue matatizo yanayotokea nchini yanasababishwa na nini na yataondokaje; watachukua hatua gani.

Polisi wakifanya kazi tunarudi hapa kuja kuwalaumu hawakuwajibika! Sasa hatujui tunafanya kitu gani? Mimi naomba tuwaachie Vyombo vya Dola vifanye kazi tupate yakini na inapopatikana yakini ukweli utajulikana na tukishajua ukweli hizi shutuma tunazoshutumiana zitakuwa hazipo na badala yake wote sasa tutakaa pamoja tuseme tunafanya nini kuondosha matatizo haya ndani ya nchi yetu. Ndiyo mwanadamu anavyokwenda, ndiyo maendeleo yanavyokuja. Kuna hatari ya kufikiri baada ya kutenda jambo. Sisi hapa tunafanya mambo nje halafu tunakuja

kufikiri humu ndani, huu siyo mtindo mzuri na hautatupeleka pazuri ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Kafulila, alisema hapa jana, tusiachie wahuni wachache kuharibu nchi yetu na hili ni jukumu letu sote, Polisi na kila Mtanzania kama tunawajua hao wahuni basi tuwa-*expose* akina nani, wanaharibuje na tuwafanyie kazi kwa pamoja waondoke. Kuna kipindi nilikuwa nasoma Gazeti la China, nikaona kikatuni kimesimama sijui mkubwa wa nini anakataza rushwa, lakini mkono wake uko nyuma una kapu limejaa mapesa anatiliwa huko. Sasa na sisi tusifanye hayo, hapa tunazungumza vizuri tukirudi kwenye viriri vyetu tukaenda tukazungumza vibaya. Jamani amani ni kitu kikubwa.

Amani ni kama uzi wa hariri, wasiojua hariri ni *silk*. Uzi wa hariri ni mwembamba sana, lakini madhubuti na unapoukata kuuunga ni kazi. Hariri haiungwi na ukiiunga hata kitambaa chake utakiona kina *low quality,* hakina ile *quality* ya hariri yenyewe, inakuwa ina mafundo mafundo, kuna mtu ananisaidia. Kwa hiyo, jamani amani ni uzi wa Hariri tusiukate, tukiukata kuuunga ni kazi kwelikweli. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mkuchika, atafuatiwa na Mheshimiwa Lukuvi.

**MHE. GEORGE H. MKUCHIKA – WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Kabla sijaendelea, niseme kwamba, naunga mkono hoja hii. Pili, napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole waumini waliovamiwa wakiwa katika ibada Arusha juzi. Natoa wito kwa Watanzania wenzangu kwamba, yaliyotokea Arusha yanaweza kutokea mahali popote, tuungane wote kukataa majanga kama haya. Watanzania tukumbuke alivyotuasa Baba wa Taifa kwamba, katika vita ya dini hakuna mshindi. Yatatokea matatizo wataumia watu, wale walioumia wataingia mitini watakwenda kujiandaa watakwenda kulipiza na tena na tena, nchi yetu itatufikisha mahali haitatawalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kutofautiana sana na wenzangu wengi waliolaani Jeshi la Polisi kwamba, halifanyi kazi na wengine walifika hatua hata ya kusema ifike muda tulivunje. Jamani, ndugu zanguni, naomba nikuulizeni hebu tungefanya majaribio muda wa saa 24 tukae bila Jeshi. Mwingine amesema hapa Dar es Salaam wale Askari wa Trafiki mvua iwe inanyesha halafu Polisi wasiwepo, kila kitu kitasimama Dar es Salaam. Wote tunakumbuka hapa Serikali ya Awamu ya Nne wakati inaingia madarakani, wizi ulishamiri wa mchana, watu walikuwa wanabomoa Mabenki mchana mpaka wanauliza hivi kama hela yetu Benki haina usalama wapi kuna usalama! Sasa naomba kauli zetu tunazozisema hizi, sema mnasikika sawa, lakini hao wanaokusikieni inawezekana wana akili sana, siyo inawezekana, wana akili sana, wanajua kwamba huyu anachekesha, wanajua kwamba huyu anasema kweli. Mimi nilikuwa nataka kusema hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema nawapongeza Jeshi la Polisi, wanafanya kazi katika mazingira magumu, vitendea kazi walivyonavyo havitoshi kwa sababu ya uchumi wetu, hatufanyi makusudi, lakini nataka niwaambie Kimataifa, Polisi mmoja anapaswa kuhudumia watu kati ya 450 mpaka 600. Polisi wa Tanzania mmoja anahudumia watu 1,100, hawatoshi. Pamoja na matatizo haya, wanafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, mtu mwingine alisema hapa tuvunje Polisi, Jeshi waendeshe kila kitu. Mimi hapa ni *Qualified Army Officer* tena *tested,* ambaye nimepigana vita na kushinda. Kazi ya Jeshi, *TPDF* ni tofauti na Polisi. *TPDF* tunafundishwa kupambana na adui porini, *you completely annihilate the enemy*, kazi ni kummaliza adui. Polisi kazi yake ni kumwita na kupeleleza kesi. Mimi hapa *retired respected army captain,* lakini sina utaalamu wa kupeleleza kesi. Leo mnasema mvunje Polisi, kila kitu afanye *TPDF;* mnajua haya mambo au mnasema tu? *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasema nataka niwapongeze sana Polisi, wanafanya kazi nzuri. Shakespear aliandika hiyo. Namnukuu Shakespear alisema: *"The evil that men do lives after them, good is oft interred with their bones".* Tafsiri yake kwamba,

matendo maovu binadamu anayoyatenda, yanadumu muda mrefu sana, lakini yale mazuri hayadumu. Ndiyo maana ninyi Polisi sijui imekuwa kitu gani basi hayo yanadumu muda mrefu, lakini kwamba walikomesha ujangili, waliwasaidia kukamata majambazi, wamefanya nini, wamakamata madawa ya kulevya Uwanja wa Ndege, yote yale hamuyaoni! Hatushangai Shakespear aliandika "*The evil that men do lives after them, good is oft interred with their bones".*

Mheshimiwa Spika, Polisi, mimi ni mtu mzima, ni mzee wa miaka 65, nakupeni pole kwa haya mliyoyasikia, msikate tamaa chapeni kazi. Afrika inaheshimu Jeshi la Polisi la Tanzania, wanakuja kusoma hapa. *IGP* huyu tumemtoa *Interpol* alikuwa anafanya kazi Shirika la Kimataifa la *Interpol,* tukamwambia sasa wewe uwe hapa uwe *Inspector General*. Sisi tuna watu wanatosha ndiyo maana nchi hii inakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, kuwaomba tu Wanasiasa wenzangu, tusiifanye kazi ya Polisi kuwa ngumu. Baadhi ya Wanasiasa tunafanya kazi ya Polisi kuwa ngumu. Wewe unahutubia mkutano wa hadhara, mnasema mkitoka hapa sisi wote tuondoke tukavamie Kituo cha Polisi tukawatoe watu wetu waliomo mle ndani. Katika mazingira kama hayo, Polisi anasema ndugu tafadhali, ndugu ndugu huku Jeshi la watu elfu moja au mbili wanakwenda kuvamia Jeshi la Polisi wawatazame tu. Naomba kauli zetu Wanasiasa, tuchunge maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, lingine, nataka kulisema, ndugu yangu Mheshimiwa Lissu hapa jana alisema nayo yamo katika kitabu. Anasema: "Yaliyotokea juzi Arusha ni kwa sababu Serikali imenyamazia matukio haya. Jamani hivi kweli Serikali nchi hii inanyamazia matukio haya? Polisi wameshughulika, Rais wa Nchi ameongea na Watanzania katika hotuba ya kila mwezi akakemea, jana Makamu wa Rais akakemea na leo tumeambiwa Rais wa Nchi alikuwa nje amekatisha ziara kurudi kuja kushughulikia mambo ya Arusha. Naomba tuwe wakweli. Leo wewe mtu unasimama hapa unawaambia Watanzania Serikali hii haijali; *are we serious?*

Mheshimiwa Spika, sasa nasema Mheshimiwa Rais pamoja na kuongea hilo anaendelea kukutana na viongozi wa dini mbalimbali, baadaye atakutana na viongozi wa dini zote, leo hapa Mkoa wa Dar es Salaam wanafanya mkutano wa madhehebu yote ya dini kuhakikisha kwamba, Dar es Salaam kunakuwa shwari. Hivi haya yote tunayoyafanya ndani ya Serikali bado tunaambiwa hapa kwenye *loud speaker* na watu wanasikia kwamba, Serikali inanyamaza? Hao Watanzania mnaowaambia wanajua nani anasema kweli na nani anaongopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine tunaambiwa hatuwatangazi waliokamatwa, hatujui mwisho wapi. Nchi hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria, taratibu na kanuni. Hii ni nchi inayoheshimu *rule of law*. Anayesema kwamba huyu ni mhalifu na inamtia hatiani, kazi hiyo ni ya Mahakama. Kwa nini mnataka tutoe matangazo ya matokeo ya kesi kabla haijamalizika Mahakamani? Tena wengine wanaosema hivyo ni Wanasheria waliobobea na wamezoea kujiita *Learned Brother* hao wanaotaka tutangaze kabla ya wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Kambi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Lukuvi halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Wassira lakini simwoni. Mheshimiwa Lukuvi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Nchimbi kijana mwenye uwezo kabisa na amedhihirisha kwamba ana uwezo wa kuongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pole kwa yale yote yaliyotokea Arusha. Wapenda amani wote wa Tanzania na wapenda amani wote wa dunia, wanalaani kitendo hiki na

nampa pole sana Baba Askofu wa Arusha na waumini wa Arusha. Nampa pole vile vile Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwa haya yaliyotokea na kama wanasikiliza Bunge hii wanajua na Waheshimiwa Wabunge wako pamoja nao. Nafikiri kwa umoja wetu tunapaswa kuendelea kuyalaani na kukemea matendo haya hasa kama hili la Arusha ambalo limetokea kwa namna ya pekee.

Mheshimiwa Spika, tulizoea kuliona bomu lililolipua Ubalozi wa Marekani lakini angalau lile tulijua lina *roots* za moja kwa moja kutoka nje, lakini hili bado hatujajua kama lina *roots*. Kwa hiyo, kama wanaoshikwashikwa na kutajwa ni baadhi ya Watanzania *then*, kama walivyosema wenzangu jambo hili ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika na kama alivyosema Mheshimiwa Rais na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwenye kauli yake kwa hatua ya awali tunawapongeza sana Jeshi la Polisi na wananchi ambao wameshirikiana nao angalau kufikia hapo walipofikia.

Mheshimiwa Spika, nina imani na Watanzania wengi wana imani na Jeshi la Polisi kwamba litatimiza wajibu wake na haya mambo yatafika mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kulipa pongezi Jeshi la Polisi, lakini kulitia moyo Jeshi la Polisi. Kwa sababu katika hotuba nyingi hapa na maneno mengi kana kwamba, Jeshi la Polisi pamoja na udhaifu wa kutokuwa na vitendea kazi na pesa nyingi, ni kana kwamba wamekuwa *so condemned*, hawafanyi kazi, hawatekelezi wajibu wao na wengine kama alivyosema Mheshimiwa Mkuchika walikuwa wanatakiwa wafutwe moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia Jeshi la Polisi, kama tungekuwa tunapiga kura hapa asilimia 90 wanawaunga mkono sana. Hayo maneno machache mliyoyasikia, pengine ni asilimia kumi au tano. Lakini kwa sababu humu ndani tuna malengo mengi, tunasema ili tusikike au wengine tunasema kwa dhati. Kuna watu

wanaosema ili wasikike, waonekane na wengine wanaosema kwa dhati. Lakini wale wanaosema kwa dhati wanawaunga mkono.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanawaunga mkono kwa sababu hakuna tukio la kheri ambalo Polisi hahusiki. Kwenye sherehe zetu, kwenye mikutano yetu tunawatumia Polisi na ukiona mtu hapendi sana Polisi lazima ujiulize kuna nini? Ukiona mtu anaichukia sana Polisi lazima ujiulize maswali. Kwa nini unalalamika Polisi inakushughulikia wewe peke yako tu kila siku?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kuwapongeza sana Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri mnayofanya mwendelee kufanya. Najua wengi wanazungumzia habari ya fedha kwamba fedha hazitoshi. Utendaji wa Polisi hautegemei fedha tu, nawapongeza Polisi kwa utashi. Polisi halitekelezi majukumu yake kwa pesa peke yake. Polisi ya Tanzania inatekeleza kwa utashi, kazi inafanya kwa mapenzi na utashi. Kwa hiyo, utashi huu ndiyo unawezesha Jeshi la Polisi kufanya kazi vizuri ndani ya nchi hii, sio fedha peke yake.

Mheshimiwa Spika, fedha sehemu zote na kwenye idara zote kila mahali hazitoshi. Tangu tumeanza kwenye bajeti ya Waziri Mkuu mpaka leo kila Wizara fedha hazitoshi. Lakini kilichojidhihirisha ndani ya Polisi pamoja na kwamba fedha hazitoshi, lakini utashi unatosha. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa utashi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Kiongozi wa Jeshi la Polisi *IGP* Mwema ambaye amefanya *reform* kubwa sana ndani ya Jeshi, Jeshi limekuwa la kiungwana. Jeshi linafanya kazi nzuri sana, tumeshuhudia sasa ukaribu kati ya wananchi na Jeshi lao. Nampongeza sana, lakini nampongeza zaidi Kamanda wangu Kamuhanda, Kamanda wa Mkoa wa Iringa. Ukiona hotuba nzima ya wanaume imekutaja humu kurasa nyingi Kamuhanda, Kamuhanda huko Iringa lazima ujisifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani wamekutaja sana, hawawezi kukupongeza. Huko Iringa Kamuhanda anafanya kazi kubwa na nataka unisikie huko, usitetereke na Makamanda wako wa Iringa. Endelea kufanya kazi nzuri. Haya maneno ya Mheshimiwa Chiku ya kuganga njaa humu ndani usiyasikilize. Siasa za kuganga njaa humu ndani na kusingizia Lukuvi anawatumeni kazi, Lukuvi hawezi kuwatuma kazi. *(Makofi)*

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Lukuvi ni Mbunge wa Jimbo la Ismani, hawezi kumtuma Kamanda wa Polisi eti ambambikie mtu kesi. Hivi haya maneno yanaingia akilini?

**WABUNGE FULANI:** Hayaingii.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Leo tunazungumzia hoja kubwa ya Arusha. Mbunge aliyechaguliwa na amekaa miaka kumi, anakuja hapa kuzungumza mambo ya Ismani na mambo ya Iringa, inakuja akilini katika hotuba kama hii? *(Makofi)*

Sasa naomba watu wa Iringa mumsamehe Mheshimiwa Chiku Abwao na bila shaka mnajua Wabunge wa Iringa tuko wengi, kila mtu na uwezo wake na nataka tu kumwambia Mheshimiwa Chiku Abwao, kizuri chajiuza kibaya chajitembeza. *(Kicheko)*

Usione vya elea, Ismani umeikuta na utaiacha, tupo wenyewe tutaendelea kuwanayo na tutaendelea kuitunza Ismani, usiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkuchika amesema kidogo, wanasiasa wa pande zote tuliunge mkono wa Jeshi la Polisi. Tuache kulitumia chambo. Maana hata samaki ukimtumia chambo unataka anase. Lakini Jeshi hili la Polisi tumejitahidi sana kulitilia chambo halinasi, tunachukia. Tusilichokoze Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi njiti zake zimejaa, tusilichokoze. Wakati fulani nimeona baadhi ya viongozi hata wa Upinzani wanatumia busara wanazungumza na viongozi wakuu, wanaepusha shari. Tuendeleze utaratibu huo wa kuepusha shari kwa mazungumzo badala ya kuonesha ubabe, mimi nani. Ukishasema mimi nani na yeye ana moto binadamu ni binadamu tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimesimama kuunga mkono hoja, lakini kuwapa moyo vijana wa Jeshi la Polisi na Makamanda wao, endelezeni. Haya mafanikio machache tuliyonayo bila ninyi yasingekuwepo, endelezeni. Msikatishwe tamaa na ajenda za watu wachache...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge sasa hivi nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Pereira Silima atatumia dakika kumi za kuchangia, lakini atakopwa dakika zingine na Mheshimiwa Waziri naye atakuwa na dakika 45 na huyu atakuwa na dakika 25. Naibu Waziri Mheshimiwa Pereira Silima!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niungane na Wabunge waliotangulia kuchangia kwenye hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Naanza kwa kuiunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nafikiri ningelisema, ni kutoa tena pole kwa watu wa Arusha na Watanzania wote kwa tukio ambalo limetokea kule Arusha. Nilikuwa Arusha, nilishafanya kazi hii, lakini kule hawakuwepo Watanzania wote. Kupitia Bunge hili naomba niwape pole Watanzania wote na niwaambie kwamba, sisi ambao

mmetupa dhamana ya kuilinda hii nchi, tutachukua hatua kuhakikisha kwamba, wahalifu si tu tunawapata, lakini tunachukua hatua za kisheria zinazopaswa.

Mheshimiwa Spika, fursa hii pia naomba nichangie kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge hasa kwenye Fungu 29 - Magereza, Fungu 14 - Zimamoto na kuzungumzia Fungu 51 lenye mambo ya wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Wabunge wote waliochangia na nianze kuwaambia kwamba, michango yao tunaithamini na tumeipokea. Wale ambao wametoa ushauri, ushauri tutaufanyia kazi na kwa vyovyote hata tukijibu leo hapa, lengo halikuwa leo tuwe tumechukua hatua. Lakini tutaufanyia kazi na katika muda wa kuanzia leo mpaka bajeti ijayo au muda mwingine ambao tutapata kuzungumza, mtatufanyia tathimini ya kile tulichokitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ambazo nyingi ni za ushauri. Kama nilivyosema tutazichukulia hatua. Kulikuwa na hoja kwamba, wafungwa katika bajeti ambayo tunaipitisha wanatakiwa wale sh. 577/= kwa kila mmoja kwa siku, badala ya sh. 3,155/=. Hili ni tatizo la msingi ambalo linasababishwa na ufinyu wa bajeti na kabla hatujafanya mambo ambayo ni kinyume na haki za binadamu Serikali inalichukulia hatua na kuhakikisha kwamba hali hii inaboreka na wafungwa wanapata chakula wanachostahili kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine au ushauri kwamba, wigo wa *Parole* upanuliwe. Naomba nitoe taarifa kwamba, marekebisho ya Sheria ya *Parole* yako njiani na wigo wake utabadilika katika maeneo tofauti hasa katika maeneo ya vifungo na masharti mengine ya *Parole*.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kuhusu posho ya chakula cha askari wakiwa Magereza na Polisi. Wengi walikuwa wanafikiri 5,000/= haitoshi na tufanye 7500/=. Ushauri huu ni mzuri na utazingatiwa na Serikali na ushauri huu umeshafika kwenye Kamati ya Bajeti ya Bunge letu

Tukufu. Kwa hiyo, kama haikuwezekana leo kuna siku tutafanya *review* pengine itawezekana.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa utaratibu wa askari kujiendeleza ambayo imetoka kwenye Kambi ya Upinzani. Wanasema utaratibu wa miaka sita unawafanya wadumae na wasiweze kujiendeleza. Naomba kwanza niikatae kauli ya kusema kwamba, utaratibu ule umechakachuliwa. Utaratibu katika nchi zinazoendelea na katika fikra za kawaida huwa unarekebishwa. Kwa hiyo, katika kuendeleza usimamizi wa Askari katika Jeshi la Magereza utaratibu huu wa masomo umerekebishwa na haukuchakachuliwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu kwenye chombo chochote ni lazima uzingatie mahitaji ya wataalam, ngazi na wapi nani kaenda, nani kabaki. *Succession plans* na mambo mengine. Kwa hiyo, utaratibu huu haukuchakachuliwa, isipokuwa umefanywa uendane na mahitaji ya wataalam na askari. Hivi sasa kuna zaidi askari 500 wa Jeshi la Magereza pamoja na Maafisa ambao wako masomoni kwa utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imechangiwa na Wabunge wengi sana kuanzia kwenye Kamati ya Ulinzi na Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Kibona, Mheshimiwa Filikunjombe, Mheshimiwa Shekifu, Mheshimiwa Kilufi, Mheshimiwa Chiligati, Mheshimiwa Arfi na wengine kwamba ni vyema tuboreshe makazi ya Askari wa Magereza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hili tunalifahamu na jitihada zinakwenda taratibu, lakini zimeanza. Jeshi la Magereza linaandaa mpango wa maboresho ya Jeshi lenyewe na *services* zake na hili jambo liko ndani ya mpango huo. Pamoja na hilo, Jeshi lenyewe lina mpango wanaita mpango wa ubunifu wa kuhakikisha kwamba Magereza katika maeneo tofauti wanajenga nyumba kwa kujisaidia wenyewe kwa kutumia rasilimali za asili zilizopo kwenye eneo husika. Zaidi ya nyumba 90 zimejengwa na nyingine zimekamilika na nyingine zimo katika hatua za kuzikamilisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo tunao utaratibu na mazungumzo yameanza ya kuhakikisha kwamba, sasa kupitia bajeti, imedhihirika kwamba si rahisi kukamisha ujenzi na kuweka Askari wetu katika nyumba zinazofaa. Kwa sasa tunaangalia uwezekano wa kutumia *PPP* na hata mikopo kwa dhamana ya Serikali. Hili kwa muda mfupi unaokuja tutalitolea taarifa namna gani tunataka kuendeleza kazi hii.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na Waheshimiwa Wabunge wengi waliozungumzia suala la kuwa na Magereza ya Wilaya. Kuna baadhi ya Wilaya 45 zikiwemo mpya na za zamani ambazo hazina Magereza ya Wilaya. Hili tunalifahamu na kupitia baadhi ya *measures* hizo nilizozisema, tutahakikisha kwamba sehemu zote za nchi hii kuanzia Wilaya na hata maeneo chini ya hapo, yatapata Magereza yanayostahiki ili wale ambao jamii inahitaji kuwaficha, watafichwa na watafichika.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni msongamano mkubwa kwenye magereza yetu. Jambo la msongamano ni jambo mtambuka na limeendelea kutukabili kutokana na ongezeko kwanza la uhalifu, lakini pia muundo wetu wa Sheria. Kuna baadhi ya kesi zinaweza zikawa ndogo, lakini zikakosa dhamana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mahabusu wengi wanarundikana, uchache na uchakavu wa magereza kama nilivyosema hapo mwanzo. Lakini pia kuna baadhi ya kesi tunachelewa kumaliza upelelezi wa mashauri wenyewe kutokana na *complications* zilizopo. Lakini naomba niwahakikishie kwamba, Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, tunajitahidi kuhakikisha kwamba vikwazo vilivyopo na vinavyosababisha msongamano vinatatuliwa kupitia utoaji wa elimu lakini na kusukuma ushauri, lakini hata kujenga magereza zaidi kwa ajili ya kuhifadhi wafungwa na wahalifu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba kwa nini wafungwa walale saa kumi na sio saa mbili au zaidi ya hapo. Sheria ya Magereza yenyewe ya mwaka 1968 na Kanuni zake

namba 234, zinaelekeza kwamba, wafungwa wasilale zaidi ya saa kumi na moja na nusu. Hili ni kwa sababu ya shughuli ambazo zinatakiwa zifanywe ili kukamilisha hali ya usalama kwenye magereza yetu.

Mheshimia Spika, kwanza, kabla wafungwa kutakiwa waingie wakalale, wanatakiwa waangaliwe kwamba hawana vitu ambavyo haviruhusiwi magerezani au kwenye mabweni yao, wengine wanakuwa wamekwenda Mahakamani, wengine wamekwenda mashambani, wanaweza kurudi na vitu vya hatari kwenye magereza, kwa hiyo, wanalazimika kupekuliwa. Magereza ambayo yanawafungwa na mahabusu wengi kazi hii ni lazima ianze mapema na imalizike mapema.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi ni lazima hili lifanyike mpaka hapo tutakapokuwa na magereza ya watu saba au wanane tu au tutakapobadilisha Sheria na tutakapopata taratibu nyingine za kufaa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo wanafunzi ambao wako masomoni au wafungwa waliochelewa kwenye kazi au wapishi na wale ambao wanahitaji mazoezi maalum ya viungo, wale tunawaacha mpaka hapo kadhia hizo zinakapofika wakati wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kwamba, upekuzi unadhalilisha utu wa watu ambao wako magerezani. Naomba nitoe taarifa kuwa lengo hasa la upekuzi ni usalama na hili ni kwa usalama wa gereza lenyewe, lakini pia kwa usalama wa askari pamoja na wafungwa na mahabusu na upekuzi hufanywa kwa Sheria na taratibu na Kanuni ambazo ziko pale.

Mheshimiwa Spika, chini ya Sheria hizi na Kanuni hizi utu, haki za binadamu na staha unazingatiwa. Mtu ambaye anatakiwa apekuliwe kitu cha kwanza anaambiwa atoe vitu vyote ambavyo anahisi vinahatarisha na haviruhusiwi gerezani. Utu wa mtu hapo ndiyo upimwe, siyo pale ambapo amelazimishwa kupekuliwa na akakutwa na kitu ambacho

hakiruhusiwi, kama unataka utu uhifadhiwe mwanzo, basi tumia fursa hii ya kuhakikisha kuwa unasema mimi nina hiki na hiki na unavitoa. Ukiondoka hapo kinachofuata kama unashukiwa ni lazima upekuliwe inavyowezekana ili mradi usalama wa Gereza ulindwe.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hivyo, siyo kwamba wanapekuliwa mbele za watu kama inavyoelezwa au mbele za watu hadharani wanasema, wanapekuliwa kwenye maeneo maalum na *gender issues* zinazingatiwa. Kwa hiyo, kwa sasa ili tuondokane na hili tunafikiria kwa sababu hata wale ambao wanapekuwa nao ni wanadamu na hawapendi kuona ambavyo havitakiwi vionekane. Tunafikiria kuwa uchumi ukiimarika tupate *detectors* badala ya kumshika, kumgusa na kumuacha akae vipi, tutatumia *detectors* lakini hili litategemea hali ya uchumi unavyoimarika na fedha za kununulia zinapopatikana.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, Serikali itumie magereza kutengeneza samani zinazohitajika Serikalini. Hili naomba nikupongeze kwa uamuzi wako na kuwa mfano kwa hili na zipo Taasisi ambazo nazo zinatakiwa zifuate njia ambazo umeanza kuonesha. Jeshi la Magereza lina uwezo na liko tayari kutengeneza samani za Serikali kwa faida ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kuwa watoto wasichanganywe na wahalifu wakubwa; kwanza Sheria ambazo zipo za Kimataifa na Kitaifa zinasema kuwa watoto ambao wana mgogoro na Sheria wasiwekwe magerezani. Pia katika kulifanya hili, basi ni lazima kuzingatia aina ya makosa ambayo mtoto anayo, umri pamoja na urefu wa kifungo chake au kama ni kwanza amekuja, basi ni kuangalia kadhia ambayo inamhusu.

Mheshimiwa Spika, hili tunalifanyia kazi kwa kushirikina na *UNICEF* na jitihada hasa ni kutaka kuwa na mfumo pekee wa watoto kuanzia mahabusu, kituo cha polisi mpaka tufike kwenye kifungo hata Mahakama tunatakiwa tuwe nazo za watoto ili tuweze kuwalinda watoto kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mlo wa wafungwa; kuna hoja kwamba, kwa nini wasile saa mbili usiku kama tunavyokula *dinner* wengine. Kwanza suala la milo mingapi wanakula, magerezani siyo muhimu kuhesabu milo, lakini kipimo maalum ambacho kinatolewa ni kuhakikisha kuwa mahitaji ya mwili wa binadamu wa kawaida yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa wanakunywa uji asubuhi *grams* 450 na mchana wanakula *grams* 500 ikijumuisha, kwa maana ya chakula cha jioni na mchana. Kufikiria wazo la kuwalisha wafungwa baada ya saa moja jioni, ni tatizo kwa kuwa menejimenti ya wafungwa kama nilivyosema mwanzo uanze saa moja halafu ufanye taratibu ili wakafungiwe siyo rahisi lakini pia uwalishe mchana, usafishe, upike, uoshe, uwalishe tena vitendea kazi hivyo kwa sasa hatuna.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili tutaendelea kuliangalia na kulirekebisha kama vile ambavyo uwezo na haja itakavyotokea kulikuwa na wazi kuwa wajawazito wapatiwe vifungo vya nje, hili lilikuwa la Mheshimiwa Pudenciana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, Wajawazito wanatakiwa kupata huduma tofauti, lakini kwa mujibu wa Sheria za Uendeshaji wa Magereza kuna sifa zinazoainisha nani afungwe nje, urefu wa vifungo, labda na makosa aliyofanya na kadhalika. Kwa hiyo, la kwanza ni hilo, halafu la pili linakuja je, ana hali gani yule muhusika. Kwa hiyo, kwa Sheria na Kanuni za sasa, sifa hizo zikitimia mtu huyo atafungwa kifungo cha nje ana mimba au lah!

Mheshimiwa Spika, lakini mara nyingi kwa sababu ya ubinadamu, watu wenye mimba huwa wanapatiwa misamaha ya Rais katika maadhimisho tofauti na hata wakiwa magerezani *status* zao zinakuwa zinatazamwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Mkumbo alisema kuhusu vitendo vibaya na viovu Magerezeni. Jitihada

kubwa sana inafanywa ya taratibu na miundombinu kuhakikisha kuwa jambo hili halifanyiki na linapofanyika watu watakuwa wamedhamiria na inawezekana wakawa ni wachawi katika kulifanya. Kitu ambacho kinasaidia hatua mbalimbali zinazochukuliwa ni pamoja na watu wa dini ambao wanakaribishwa Magerezani kutoa neno la roho, kuwa hiki kitendo kibaya kiacheni, msifanye na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia *infrastructure* ambazo zipo kwa maana ya ujenzi zinaweka maeneo ambayo kulifanya labda uwe umekusudia, ulifanye hadharani, lakini kama unataka uficho, siyo rahisi kuupata katika ujenzi wa vyoo, katika ujenzi wa madirisha na ukaaji wa askari.

Mheshimiwa Spika, halafu kulikuwa na lingine kuhusu Jeshi la Magereza lijitegemee katika chakula, Jeshi la Magereza limeweka mpango maalum wa kuhakikisha kuwa linakwenda huko na limetenga Magereza Teule hasa kwenye Kongano la *SAGCOT* maeneo ya Morogoro na Iringa katika kuhakikisha kuwa chakula kinazalishwa na uzalishaji unaendelea.

Mheshimiwa Spika, pia kuna maeneo yametengwa na mwelekezi ameshalipwa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa miundombinu ya umwagiliaji inatayarishwa kuhakikisha kuwa umwagiliaji utatumika katika kuzalisha chakula kwa ajili ya magereza na pengine ziada. Pia suala la ubia linafikiriwa kuhakikisha kuwa, uwezo wa magereza unapanuka baada ya kupata rasilimali za kitaalam au fedha kutoka sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, upande wa Zimamoto, kulikuwa na wazo au ushauri kuwa, waachiwe wabakishe mapato ambayo wanakusanya. Hili tunaliunga mkono na Serikali imelisikia na najua ni sikivu.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na wazo la kuwa, Jeshi la Zimamoto halina vifaa na utalaam, katika kulifanya hili bakizo liwe kubwa, nafikiri hii itaweza kufanyika. Kwa hiyo, Jeshi la Zimamoto ni kweli linafanya kazi katika mazingira magumu, lakini Serikali itajitahidi kadri bajeti itakavyoruhusu

kuhakikisha kuwa, wanapata magari na vitendea kazi vingine ili ifanye kazi za kunusuru maisha na mali za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kulizungumziwa kuhusu tozo la Zimamoto ambalo wala hawatoi vifaa. Naomba niseme kuwa, hili ni kwa mujibu wa Sheria na ada hizi zinaendelea, ni kwa ajili ya ukaguzi wa kitaalam na tunaendelea kutoa elimu ili siyo Wabunge tu waliulizie, bali hata raia waelewe kwa nini wanalipa hizo pesa.

Mheshimiwa Spika, kuna mkakati gani wa kuliimarisha Jeshi la Zimamoto? Jeshi la Zimamoto limeanza kuwa ni *command* moja na ni Jeshi kamili kwa kuunganisha vikosi ambavyo vilikuwa TAMISEMI na vingine vya Viwanja vya Ndege. Pia Serikali imeruhusu *retention* kujaribu kuongeza uwezo wa fedha ili tuweze kufanya kazi nzuri kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuwa, katika muundo huu, Makamanda wa Mikoa wamepata mafunzo na wamepelekwa Mikoani, tunategemea kuwa watasaidia kwa karibu katika matukio kuliko wakiwepo Dar es Salaam au miji mikubwa pekee.

Mheshimiwa Spika, zaidi katika kuimarisha uwezo wa Jeshi la Zimamoto la Uokoaji ni kwamba, tunaweka vipaumbele katika masuala ya kujenga uwezo wa uokoaji, lakini haina maana kuwa masuala ya kuzimamoto wenyewe tunayapuuza.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na hoja kuwa, Jeshi la Zimamoto limepewa 40% tu ya pesa ambazo zilitengwa mwaka uliopita, ukweli ni kuwa kulikuwa na wafanyakazi wa Zimamoto ambao bado walikuwa wanalipwa katika Halmashauri na maeneo mengine ambayo walikuwa huko mwanzo, lakini ukipiga hesabu zote, mpaka mwezi Februari, Zimamoto ilishapewa 90% ya makisio ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba, mapato ya Fungu la Wizara kutofikia lengo. Kwa kweli idadi

au asilimia 76ambayo ilioneshwa kwenye kitabu cha Waziri ni mpaka mwezi wa Februari, lakini kutoka Februari mpaka hivi sasa, napenda niwahakikishie kuwa lengo limeshafikia asilimia mia moja, sasa tunatafuta nyongeza ili tuoneshe ni wakali kiasi gani katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu kutoa uraia kwa wakimbizi na hofu ni kwamba, wakimbizi ambao tunawapa uraia wanaweza kuwa ni *time bomb*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba tena niunge mkono hoja na nashukuru kwa kunipa muda huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunamwona Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni ambaye alikwenda Arusha kutuwakilisha katika matatizo yaliyotokea. Sasa, naomba utoe salamu za huko. Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi kwa dakika chache zilizobaki, nina hakika zitatosha kwa ajili ya kutoa taarifa fupi kuhusu safari ya Arusha.

Mheshimiwa Spika, nimepata nafasi ya kwenda kutembelea sehemu ambako kulitokea ile ajali ya bomu, ambalo lilikuwa ni bomu la kutupa kwa mkono pale Olasiti, lakini pia nimepata nafasi vile vile ya kwenda kumtembelea Baba Askofu Lebulu na nimepata nafasi ya kwenda kutembelea Hospitali ya *Mount* Meru kwa ajili ya kuona wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla nimewashukuru sana wananchi wa Arusha na hasa Olasiti kwa namna walivyopokea tukio hili. Tumekuta wameshatulia kiasi cha kutosha, hata pale Olasiti penyewe hali ni tulivu. Kwa kweli

watu wamehamaki hakuna shaka juu ya hilo, lakini wamefarijika sana na hatua za Serikali za kuanza kufanya uchunguzi mara moja.

Mheshimiwa Spika, pia wameshukuru sana kwa safari aliyoifanya Makamu wa Rais mara tu baada ya kusikia jambo hili, ambapo siku ile ile akapata nafasi ya kwenda pale. Kwa hiyo, upande wa Kanisani, upande wa Baba Askofu na bahati nzuri tumemkuta Balozi wa Papa bado yupo Arusha, kwa kweli wote wamefarijika na wanatoa shukrani nyingi sana kwa Serikali na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchunguzi bado unaendelea, wamekamatwa watu wanane na kama tulivyoeleza hapo awali wanne ni watu wenye asili ya kutoka Uarabuni, watatu ni Watanzania ambao ndiyo hasa tulianza nao katika vuguvugu hili. Kama tulivyosema mmoja ni huyo ambaye anaitwa Victor Ambros, mwenzake ni Joseph na yuko mtu mwingine wa tatu. Kwa hiyo, uchunguzi kwa makundi haya yote bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini labda niseme tu kuwa, hawa raia wanne ambao walikamatwa, walikamatwa hasa kwa sababu ya kutaka kujiridhisha kwa sababu imetokea kuwa wako Arusha siku moja kabla na siku ya tukio ndipo walipoanza safari ya kwenda Nairobi. Sasa kwa sababu barabara zile zilikuwa zimeshafungwa, isingewezekana wao kupita kirahisi bila kuhojiwa, kwa maana ya kujiridhisha. Kwa hiyo, matumaini yetu ni kwamba, pengine taarifa itatoka mapema leo au kesho kwa sababu wameanza toka jana kuona kama wanahusika kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hawa wengine bado uchunguzi na mahojiano yanaendelea. Tumeomba wana Arusha pale, yeyote mwenye kujua taarifa zozote zile ambazo zinaweza kutusaidia, kuweza kubaini kwa uhakika juu ya nani kafanya jambo hili na kwa nini, basi aweze kujitokeza na kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pale hospitalini katika majeruhi 66, majeruhi 24 wamekwisharuhusiwa, wametoka, watatu wamepoteza maisha, waliobaki tunaendelea kuwauguza katika hospitali mbalimbali mmoja Muhimbili, wengine wako Seriani pale, lakini wengi wako *Mount* Meru.

Mheshimiwa Spika, pale Mount Meru *Hospital,* sehemu kubwa ya wale ambao waliathirika wameshafanyiwa upasuaji kwa ajili ya kutoa vipande vya vyuma vilivyokuwa vimewaathiri na wengi tumekuta wako katika hali nzuri na wanaendelea vizuri, wengine leo watapelekwa katika chumba cha upasuaji na wengine inawezekana kesho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichowaomba Madaktari pale, ni kuwa, vile vipande vya vyuma ambavyo vimepatikana, wasivitupe wakabidhi vyombo vya dola ili tuweze kubaini kama bomu hili la mkono limetengenezwa kienyeji au ni bomu lililotengenezwa kiwandani na kwa hiyo ni mabomu yanayotokana na majeshi. Kwa hiyo, hii itatusaidia sana kuweza kubaini kwa uhakika chimbuko la bomu hilo ni nini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo niseme tu kwa ufupi, ni kwamba, tumepata nafasi ya kuzungumza na vyombo vya habari, kwa kweli tunawashukuru sana kwa sababu toka tukio lilipotokea wamejitahidi sana kueleza jambo hili kwa namna ambayo imewasaidia Watanzania kujua ni nini kimetokea.

Mheshimiwa Spika, vile vile leo tumesikia Makamu wa Pili wa Rais kutoka Zanzibar naye ameamua kwenda kuwapa pole viongozi na wananchi. Pia wakati naondoka, nimearifiwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Zanzibar naye anatarajia kwenda kuwapa pole. Kwa hiyo, nawashukuru sana viongozi hawa wote kwa namna ambavyo wamejipanga kwa ajili ya kwenda kuwapa pole.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka niseme, tukio lile ni tukio kubwa, ni kitendo kibaya na nimewaomba sana Watanzania, mambo makubwa kama haya siyo ya

kushabikia kisiasa, tusiingize ushabiki wa namna yoyote jambo kubwa la namna linapotokea, kikubwa kwanza, nii kuhuzunika na wale ambao wamepatwa na hili janga, kuwapa moyo na kwa pamoja kushirikiana, tuweze kuona ni namna gani tuweze kupata ufumbuzi wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya wako baadhi ya Viongozi wachache wamepitapita kule, badala ya kutumia hali hiyo kwa ajili ya kusikitika na wananchi, wameingiza visiasa kidogo ambavyo kusema ukweli havikuwa na tija sana. Naomba sana hili lisiwe jambo ambalo tunalitumia kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, narejea kuwashukuru sana wana Arusha na Viongozi wa Arusha, nalishukuru sana Jeshi la Polisi, wamefanya kazi nzuri mpaka sasa. Nilikuwa nausikiliza mjadala jana na leo kwa kiasi fulani, naona lawama nyingi hivi, lakini jamani chombo hiki kinajitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama tutafika mahali na kujaribu kukionesha kana kwamba hakitusaidii, kesho na kesho kutwa tutawavunja moyo sana hata pale ambapo watakuwa wana nia nzuri ya kutusaidia. Tuwatie moyo, tuwape nguvu zaidi na Serikali tutaendelea kuwaimarisha kadri bajeti itakavyokuwa inaturuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha.

Mheshimiwa Tundu Lissu Mwongozo utanipa baadaye, uzuri ni kuwa, Mwongozo huwa hauozi, maana ni jambo lililotokea zamani, unataka ufafanuzi, tukifika tu uwahi uombe Mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba saa kumi na moja muwahi kwa sababu leo hakuna wachangiaji wengine, isipokuwa mtoa hoja. Kwa hiyo, kama mlikuwa na maswali yenu, mkiwahi itakuwa vizuri kwa sababu mtamsikiliza, kuliko amalize kujibu halafu mnaingia. Naomba muwahi saa kumi na moja.

Kwa hiyo, tukiwahi Mheshimiwa Tundu Lissu utaomba huo Mwongozo wako. Sasa nasitisha shughuliza Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, kuhusu Mwongozo.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) juu ya jambo ambalo limetokea leo asubuhi.

**SPIKA:** Kanuni 68?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Kanuni ya 68(8) ya Kanuni za Kudumu

**SPIKA:** Hebu isome hiyo tafadhali.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ni Kanuni ya 68(7).

**SPIKA:** *Okay*.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala wa leo asubuhi, tulisambaziwa orodha ya Wabunge walioomba kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na orodha ya wote waliokuwa wameomba kuchangia katika orodha hiyo.

Kwenye orodha ya wachangiaji wa leo ukiacha mtoa hoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Pereira Silima, kuna Mawaziri wengine watano ambao waliomba kuchangia, hawakuchangia wote lakini wanne wamechangia.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia utaratibu wa kuchangia wa majadiliano yanayohusu utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 99, kujadili utekelezaji wa bajeti ya Wizara na sehemu zingine za Kanuni zetu za kudumu sijaona kama Mawaziri wanaruhusiwa kuchangia mjadala wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, vile vile, nimeangalia kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 63, 3(2) na 3 (3).

Ibara ya 63(2) inazungumzia mamlaka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali, lakini Ibara ya 63(3)(b) inalipa Bunge lako Tukufu uwezo wa kujadili utekezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, watu wanaotakiwa kuchangia humu ndani utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya kila mwaka, ni Wabunge siyo Serikali, kwa sababu katika Katiba yetu Bunge liko katika sura ya Tatu ya Katiba na linahusu Wabunge na Serikali iko Sura ya Pili na inazungumzia Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, watu wanaotakiwa kuchangia juu ya utekelezaji wa bajeti ya kila Wizara kwa kila mwaka wa Bajeti ni Wabunge. Leo Mawaziri hao wanachangia utekelezaji wa bajeti ya Waziri mwenzao.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kama hii inaruhusiwa kwa mujibu wa Kanuni zetu zinazoongoza mjadala wa Bunge pamoja na Katiba ambayo nimeisema. Kwa vile naona kama inanyakua fursa ya Wabunge wasiokuwa Mawaziri kujadili, sisemi kwamba hizi nafasi zingepelekwa Chama kingine, lakini Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ambao siyo Mawaziri walitakiwa wachukue hizi nafasi ambazo zimechukuliwa na Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako juu ya suala hili kama linaruhusiwa kwa mujibu wa Kanuni zetu. Ni hayo tu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Bahati mbaya ninyi mnaoelezwa hamkuwepo kwenye kikao ambacho haya yalikubalika. Sasa hivi tunafanya mjadala kwa kufuatana na *ratio* ya Wabunge waliomo kwa Vyama. *ratio* ya CCM, kwa mfano, siku ya leo, ni tarehe Saba, siku ya pili, kwa saa zangu toka tunapoanza asubuhi mpaka jioni ni Wabunge kumi na nane tu wanaopaswa kuzungumza, ni wachangiaji 18. Kwa *ratio* ya Vyama unachukua ile 18 asilimia 73 ni Wabunge wa CCM, kwa hiyo, nafasi za CCM zipo, nafasi za CHADEMA zipo, nafasi za *CUF* zipo, nafasi za Vyama vingine ni *insignificant*.

Kwa hiyo, kwa utaratibu tuliokubaliana nao ninazo dakika ambazo nikikuta Mbunge wa Vyama hivi vya *NCCR* Mageuzi, *TLP* na *UDP* kama aliomba katika Wizara ile, lakini kwa sababu ya *ratio* hii hayumo, ndiyo natoa nafasi kwa muda wangu ule nina 20 *minutes*.

Kwa hiyo, katika makubaliano hayo ilikuwa, iwapo kutatokea mtu wa *front bench,* maana yake Waziri ambaye ni Mbunge mpaka tutakapobadilisha Katiba, makubaliano kwenye Kamati ya Kanuni wasichukue muda mwingine zaidi ya ule ambao ni *allocated* kwa Chama cha Mapinduzi.

Kwa hiyo leo ukiona wale waliojadili walitakiwa wa Chama cha Mapinduzi kuwa 13 *in fact* walichangia 12 tu. Kwa hiyo, hiki kitu kipo *in order* kwa sababu ndivyo tulivyokubaliana. Sasa tutakapobadilisha Katiba wasipokuwa Wabunge tutawaingizaje humu ndani? Hakuna namna, kwa hiyo mpaka hapo tupo sahihi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tuendelee, Mheshimiwa mtoa hoja!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Jumla ya

Wachangiaji walikuwa 122, kati yao wachangiaji 91 walichangia kwa maandishi na wachangiaji 31 walichangia kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru Wabunge wote wa CCM na wa Vyama vya Upinzani kwa kuchangia kwa kuonesha nia ya kuona vyombo vyetu vinawezeshwa zaidi. Lakini pia niwashukuru kipekee Mawaziri waliopata muda wa kuchangia, wamekoleza utamu wa bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nianze moja kwa moja kujielekeza kwenye hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge. Nianze na hoja au ushauri uliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama ilitaka kwanza, Wizara yangu iwezeshwe na hasa Jeshi la Polisi, jumla ya shilingi bilioni mia moja na moja ili iweze kukamilisha majukumu yake. Naomba kulitaarifu Bunge lako kwamba, katika mazungumzo kati ya Wizara yangu na Kamati tulikubaliana kwamba maombi haya ni ya msingi na yatawezesha sana utekelezaji wa ufanisi wa majukumu ya Jeshi la Polisi na kwa sababu hiyo tulikubaliana kwamba Kamati italibeba katika Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Mhehsimiwa Spika, taarifa nilizonazo ni kwamba, Kamati ya Bunge ya Bajeti imeshaanza na naambiwa kwamba dalili ni nzuri. Kwa hiyo, wale Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, tunawasihi wawe wamesikiliza kilio kikubwa cha Wabunge ambacho kiliweka msisitizo kwenye ombi hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo liliainishwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama, ni suala la kuongeza posho ya Askari kutoka sh. 5,000/= mpaka sh. 7,500/= kwa siku. Hili ni moja pia miongoni mwa mambo yaliyoainishwa katika maombi mapya ambayo yamepelekwa na Kamati mbele ya Kamati ya Bajeti. Nia yetu kama Wizara tunaomba Kamati

ya Bajeti ilisukume kama ilivyodhamiria tufanikiwe, kwa sababu ni kweli kwamba ufanisi wa Askari wetu utafanikiwa sana kama fedha hizi zitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni ya kutaka uwekwe utaratibu wa kuwekwa siku, saa muda na eneo la kuweza kufanya maandamano. Nataka nitumie nafasi hii kukubaliana na Kamati kwamba, jambo lolote lisilo na utaratibu ni fujo. Kila kitu kinakwenda kwa utaratibu na ndiyo maana watu wana kanuni zao, ukitaka kupika unapika jikoni, ukitaka kuoga ni bafuni, ukitaka kupata upepo ni *beach,* ni utaratibu wa maisha unajiwekea. Kila kitu kina utaratibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili la maandamano, nchi zote ambazo zimeendelea duniani hawakurupuki tu kila mahali, wameweka utaratibu. Marekani wana utaratibu, Uingereza ina utaratibu, zote zimeweka utaratibu. Huwezi ukatoka na ukasema leo tumedhamiria kwenda kufanya maandamano na atakayetupokea atatupokea kwenye kiti cha Spika, mtakamatwa tu. Spika ndiyo amekaa hapo leo, hakuna atakayekuja kukaa kwenye kiti cha Spika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili ni jema na ni kwa maslahi ya nchi. Mtu anaweza asilione jema kama hana nia njema na Taifa, lakini pia itafanya utaratibu uwe wazi zaidi, hofu ziondoke, watu wasiwe na mashaka.

Mheshimiwa Spika, muda ukifika wa kutolea maoni jambo hili Wizara yangu itatoa ushirikiano wa kutosha, lakini maeneo ambayo Wizara yangu inapaswa kushiriki, haitasita kushiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine uliotolewa na Kamati ni kuhusu uwezekano wa Vyombo vya Serikali kuwa na matumizi ya pamoja ya rasilimali. Mtu ambaye hafikiri sawasawa ndiye anaweza kukataa ushauri huu, kwa sababu rasilimali zote za umma; boti, magari na kadhalika, zinatokana na fedha za walipa kodi. Kwa hiyo kwa kadri utakapoweza

kupunguza matumizi kwenye eneo moja, utaweza kufanikisha majukumu kwenye maeneo mengine. Kwa hiyo, ushauri huu wa Kamati tumeuchukua na vyombo vyetu vitahakikisha vinaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile zimetolewa pongezi maalum kutoka kwa Kamati kwa jinsi ambavyo Jeshi la Polisi linajitahidi. Kwa kweli nitumie nafasi hii kusajili katika Bunge lako kwamba, kwa kweli Mkuu wa Jeshi la Polisi, *IGP* Said Mwema toka ameteuliwa mpaka sasa amefanya kazi ya kupigiwa mfano. Amefanya mabadiliko makubwa katika Jeshi la Polisi, Jeshi tulilonalo leo ni tofauti sana na Jeshi tulilokuwa nalo miaka kumi iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tukisema Polisi haina mabadiliko yoyote, hatutendi haki, ni dhambi, hatulitendei haki Taifa letu. Kwa hiyo, nasema Bunge lako na Taifa lijue kwamba, katika miaka ambayo *IGP* Said Mwema amekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, amefanya kazi ya pekee, kubwa na nzuri kupita maelezo yanayoweza kuelezwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, niende sasa katika hoja za Upinzani. Hoja ya kwanza ilihusu upelelezi kuchelewa na yakatajwa maeneo ambayo Upelelezi umechelewa. Nitatoa taarifa ya maeneo hayo:-

La kwanza, suala la Katibu wa BAKWATA, Mkoa wa Arusha kurushiwa bomu. Upelelezi wa Jeshi la Polisi katika eneo hili ulishakamilika na faili lilipelekwa kwa Wakili wa Serikali kwa ajili ya maelekezo, ndiyo utaratibu wa sasa ulivyo.

Mheshimiwa Spika, suala la Katibu wa Mufti kumwagiwa tindikali, upelelezi umekamilika na jalada limepelekwa kwa *DPP*. Suala la shambulio la Padri Ambros, upelelezi umekamilika na jalada limepelekwa kwa *DPP*. Matukio ya uchomaji wa Makanisa, kesi ziko Mahakamani na watu wanaendelea kujitetea Mahakamani kwa jambo lile la kuchoma Makanisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie tu Msemaji wa Upinzani Bungeni kuhusu Wizara yangu kwamba, akiwa anazihitaji takwimu hizi wakati mwingine siyo lazima sana aziombee Bungeni, naweza nikampa tu hata nje ya ukumbi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo niende kwenye suala ambalo Waswahili wanasema, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Katika hotuba ya Upinzani wameeleza jinsi ambavyo katika Vyama vya Siasa, sina hakika, lakini wamesema katika Vyama vya Siasa wao ndio wamefanya mikutano mingi zaidi kuliko Chama kingine chochote cha Siasa. Kwa hiyo, nawapongeza sana CHADEMA kwa kazi hiyo kubwa mliyofanya ya kuimarisha chama chenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na pongezi hizo vile vile wametoa malalamiko makubwa kuhusu kuzuiliwa kufanya mikutano. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kusema pongezi zangu za ninyi kuweza kufanya mikutano hiyo zinaambatana na Polisi waliolinda hiyo mikutano mingi mliyojisifia kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Polisi isifuate maagizo ya wanasiasa, nakubaliana na ninyi kwamba, Polisi kwa kweli haipaswi kufuata maagizo ya wanasiasa, inatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia Katiba, sheria na taratibu za nchi. Ni kosa kubwa sana kuliendesha Jeshi la Polisi kwa maelekezo ya wanasiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mpaka leo *RPC* wa Iringa anaendelea kuwa katika nafasi yake, kwa sababu wanasiasa ndiyo walikuwa wanataka atoke. Kwa hiyo, nikuhakikishieni kwamba, maelekezo haya ya Bunge ya sisi kutofuata maelekezo ya wanasiasa katika kuliendesha Jeshi la Polisi, tunayatekeleza kwa nguvu sana na tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo liliibuliwa na Kambi ya Upinzani ni suala la Koplo Meshack wa Arusha,

ambaye walisema alisingiziwa kuwa ni kichaa na bosi wake na baadaye ikabainika kuwa siyo kichaa. Jambo hili tutalifanyia kazi ili tujue ukweli wake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwaase Askari kwamba zile taratibu za malalamiko wasiache kuzifuata. Kila ngazi ikikupuuza nenda ngazi inayofuata. Hata sasa tuna malalamiko ambayo tunayashughulikia ya Askari ambao ngazi zao hazikuwasaidia na sisi ngazi yetu tunayashughulikia. Lakini wakiwa wanapeleka tu malalamiko kila mahali na yenyewe ina matatizo yake kujua nafasi yako kama askari unaielewa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ilijengwa hoja kwamba, Mheshimiwa Aden Rage alitoa silaha hadharani kule Igunga na hajachukuliwa hatua zozote. Suala la Mheshimiwa Rage kutoa silaha hadharani lilikuwa katika eneo la uchaguzi na hatua zilichukuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa Sheria ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, suala la kwamba kuna Waziri na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma wanajaribu kuzuia jambo lake lisishughulikiwe, ilikuwa riwaya tu ya kufurahisha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo liliibuliwa na Upinzani ni kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo. Nakubaliana na Msemaji wa Upinzani kwamba, kwa kweli tunalo tatizo, kwa sababu hatuwezi kusema hatuna tatizo la kuzagaa kwa silaha wakati majambazi wanashambulia kwa kutumia silaha. Kwa hiyo, niseme tutachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, tulianza mapema mwishoni mwa mwaka jana, tulitangaza watu wasalimishe silaha zao, karibu silaha mia mbili zilipatikana. Misako inaendelea kila siku lakini nataka niseme bado tunatakiwa kulisimamia kwa uzito zaidi. Kwa hiyo, nikuhakikishie Msemaji wa Upinzani kwamba hili tutalisimamia zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la kuongezeka kwa watu wanaokamatwa na madawa ya kulevya, sitaki kusema kwamba, imesababishwa sana na madawa kuwa mengi zaidi, lakini nataka kusema kwamba, ni maoni ya Wizara kwamba, kukamatwa kwa wingi kwa madawa ya kulevya ni matokeo ya kazi kubwa inayofanywa na kikosi kazi maalum kilichoundwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kikosi Kazi hiki kinahusisha majeshi yetu, Jeshi la Polisi, Usalama wa Taifa maana kuna wengine hawajui hata shughuli ambazo Usalama wa Taifa wanafanya. Kwa hiyo, Jeshi la Polisi, Usalama wa Taifa, pamoja na Jeshi la Wananchi wote wanashirikiana katika kikosi kazi hiki kutafuta madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, nilitaarifu Bunge kwamba, mwezi mmoja uliopita Askari wa kikosi kazi kile tumewapandisha vyeo kutokana na kazi kubwa ambayo wameifanya siku za karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile katika eneo la Uhamiaji, Kamati ya Ulinzi na Usalama, ilipendekeza kwamba, kiwango cha *retention* kwa Uhamiaji, kibaki 61%.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara, katika mazungumzo yetu na Kamati, tulikubaliana kwamba, ni kweli, kwamba, ukishusha kiwango chao, utendaji wao wa kazi utapungua. Lakini vile vile dhamira yetu ya kuwaondoa wahamiaji haramu itaathirika sana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa vile vile na hoja ambayo iliibuliwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama, kuhusu haja ya matumizi ya *sticker* za kwenye *Visa.*

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba, ni kweli, tunazo baadhi ya nchi hazijaanza kutumia *sticker* katika *Visa*. Hii inaruhusu mianya ya wizi, inaruhusu mianya ya kupotea mapato ya Serikali. Maana ukiwa na mtu kazi yake anagonga mhuri halafu *Visa* inatoka, ngumu sana kwenda kuhesabu ile

mihuri aligonga mingapi au wino uliendа kiasi gani, kwa hiyo, kwa kweli, huu ni mwanya mkubwa. Nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba, tatizo hili kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje pamoja na Hazina tutalimaliza, ili tukakapokuja kwenye bajeti ijayo, isiwe tena hoja ya kuizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *NIDA,* Kamati ya Ulinzi na Usalama, ilitaka fedha za *NIDA* ziongezwe zaidi. Nataka kwanza nishukuru sana msukumo wa Bunge pamoja na Kamati, ambao kutokana na changamoto nyingi, mwaka jana mtakumbuka bajeti ya *NIDA* tulipewa bilioni 10 katika mahitaji yaliyokuwa zaidi ya bilioni 150. Mwaka huu bajeti inaonesha kwamba, tumetengewa bilioni 151.2. Naomba kulishawishi Bunge lako kwamba, kwa kuanzia tunaweza kufanya kazi kubwa na fedha hizi. Kwa hiyo, tupewe tu muda wa kufanya kazi na tutaonesha matokeo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilitaka kujua kwamba, *NIDA* mpaka sasa imeshapata fedha kiasi gani katika kipindi chote ambacho kimepita? Katika kipindi chote ambacho kimepita, *NIDA* imepata jumla ya shilingi bilioni 46.3 ambapo fedha hizi zimetumika kumlipa Mkandarasi kujenga Kituo cha Uwekaji Kumbukumbu, kuweka vitendea kazi, uratibu wa zoezi la awali pamoja na mishahara ya wafanyakazi wa *NIDA.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye wale ambao walichangia kwa mdomo au ngoja nimalizie kwanza hii ya Upinzani. Walisema taarifa zinazokaa kwenye kadi ya *ID* ya Tanzania ni chache mno.

Mheshimiwa Spika, nataka tu kulitaarifu Bunge lako kwamba, katika utaratibu wa *Biometric,* ambao unatumika na Kitambulisho chetu cha Taifa, kumbukumbu unazojaza kwenye fomu; Wabunge wote mlipata bahati ya kujaza fomu kwa ajili ya kupata kitambulisho, kila ulichoandika kwenye fomu kipo katika kadi yako. Sasa taarifa zako haziwi kwa ajili ya kila mtu, ndio maana anasoma ambaye anatakiwa

asome. Mpaka sasa pamoja na kujaza taarifa zote ulizoweka kwenye kadi kuwemo kwenye kadi ile, bado haijatumia hata robo ya uwezo wake wa kutunza taarifa.

Mheshimiwa Spika, madhumuni yake ni kwamba, mwishoni inaunganishwa na mitandao mingine. Kwa hiyo, kila mtandao utatumia mahitaji yake, kama ni Benki itatumia inayotaka, kama ni Posta watatumia wanayoyataka, kama ni Hospitali watatumia wanayoyataka. Ndio maana kuna mchango wa maana tu kwamba, ilitakiwa hata *group* la damu liandikwe kwenye kadi hiyo sawasawa, lakini kwa matumizi ya nani?

Mheshimiwa Spika, ukijisajili na Hospitali, kwenye mtandao ule ambao unahusika na Hospitali, litawekwa *group* lako la damu. Kwa sababu, utakwenda kutibiwa kule, umeishiwa damu, wataangalia, huyu ni *group O.* Lakini sasa kwa matumizi ya Kibenki damu wanafanyia nini? Kwa hiyo, kila mtu anatumia matumizi yanayomhusu yeye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Josephat Kandege, aliomba kujenga nguvu zaidi katika Vituo Vya Utambuzi; tunakubaliana na hoja yake, ili tusije tukawapa vitambulisho watu wa ajabu ajabu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, aliomba wahamiaji haramu wasipate vitambulisho; tunakubaliana na yeye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, alitaka uangalifu katika suala hili, tunakubaliana na yeye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zambi, alitaka kazi ya vitambulisho iimarike, tunakubaliana na yeye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Beatrice Shelukindo na yeye alitaka umakini, tunakubaliana na yeye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo na yeye alitaka wahamiaji haramu waondolewe, tunakubaliana na yeye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, alitaka kasi ya kutoa *Passport* kwa watu wenye sifa iimarishwe, tunakubaliana na yeye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abuu Jumaa, alitaka Maafisa Uhamiaji wanaokosa uaminifu wachukuliwe hatua, nakubaliana na yeye. Kwa vyovyote vile katika Wizara nzima, sio Uhamiaji tu, suala la kukosa uaminifu katika kuhudumia wananchi na kuhudumia umma halikubaliki. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile niwahakikishieni tu kwamba, vyombo vyetu tunavyoviongoza vinajua kwamba, jambo hili hatulikubali, lakini tutaendelea kuhakikisha wanajua kwa vitendo kwa kuwaondoa wale ambao wanaharibu uaminifu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Janet Mbene na yeye aliongelea suala la Maafisa wetu kutumia rushwa na lenyewe tunakubaliana kwamba, hili si jambo la sawasawa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ntukamazina, aliongelea hongo kwa Maafisa Uhamiaji wa mipakani ambao wakati mwingine wanaruhusu wahamiaji haramu wenye mifugo kuingia kwa wingi katika maeneo ya mipakani. Nasema ni kweli, ni kero kubwa na tumeanza kuchukua hatua za kuikomesha kero hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Akunaay, aliongelea hoja ya kuchapa *Passport* Mikoani badala ya Dar-es-Salaam ili kupunguza uchelewaji wa *Passport* hizo.

Mheshimiwa Spika, nimwambie hoja yake ni nzuri, ila tu katika uchanga wetu wa sasa, udhibiti unaweza ukatupa tabu. Kwa hiyo, hoja ni nzuri, lakini nadhani jambo kubwa ni kufanya watu wa Mikoani wapate huduma bila gharama

kubwa zaidi na bila kucheleweshwa. Kwa hiyo, tutaboresha zaidi, ili kufanya hii isiwe kero ya *Passport* kuwa Dar-es-Salaam na Zanzibar peke yake ndiko zinakochapishwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohammed Missanga na Mheshimiwa Christowaja Mtinda, wote waliongelea suala la wahamiaji haramu, ambao maelezo ni kama yale niliyoyatoa awali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, aliomba Zanzibar ipewe nafasi ya kuajiri Maafisa Uhamiaji. Nataka niseme tu, katika utaratibu wa uhamiaji, wamekubaliana nafasi za kupewa upande wa Zanzibar na nafasi za kupata upande wa Bara. Kwa hiyo, ikitokea dharura sana ndio maombi yanatumwa sehemu moja, lakini hayaathiri mgawo waliokubaliana. Kwa sababu, jambo kubwa ni hili kwamba, mgawo huu usipotee, ndio jambo kubwa kwetu sisi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Clara Mwatuka, aliongelea wahamiaji wanaovuka Mto Ruvuma na wanaruhusiwa kukaa kwa sababu wana kadi ya *CCM; duuh*, hii kali kuliko zote.

Mheshimiwa Spika, suala la mtu kukaa nchini, linatawaliwa na Sheria. Ikiwa kuna sehemu wanasema eti ukiwa na kadi ya chama fulani unaruhusiwa kuwa mhamiaji, kadi ya chama sio kitambulisho cha uraia wala kadi ya chama sio kibali cha kuishi kwenye nchi fulani. Kwa hiyo, huo sio utaratibu na hatuna malalamiko rasmi ya jambo hili tulichunguze, lakini si utaratibu. Hayajawahi kutoka maelekezo ya mdomo wala ya maandishi, ambayo kadi ya CCM inakuwa Hati ya Kusafiria na ukiona mtu analiamini jambo hili, ujue na yeye ana tatizo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Khatib Said Haji, aliongelea habari ya Kamishna Mgonja kuchukuliwa hatua. Hili niliweke vizuri, katika Bunge lililopita kulikuwa kuna malalamiko hapa kwamba, Kamishna Mgonja, alilazimisha

watu wawili au watatu, wapewe uraia ambao ni watu wa Burundi na aliyetoa malalamiko anasema aliagizwa hivi, alipokataa kutekeleza, akahamishiwa Manyara.

Mheshimiwa Spika, sasa ilikuwa bahati mbaya tu kwamba, mtu mwenyewe aliyetoa malalamiko, aliomba kuniona miezi miwili nyuma yake, akiniomba nimsaidie abakizwe Dar-es-Salaam na akaelezea wazazi wake walivyo wagonjwa; baba yake mgonjwa sana, mama yake mgonjwa sana na alieleza kwa uchungu kuhusu wazazi wake wanavyoumwa, mpaka akalia Ofisini.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana mtu akilia, napata matatizo kidogo. Kwa hiyo, nikamwahidi kwamba, sasa hivi kwa kuwa umeshahamishwa nenda kwanza, baada ya miezi sita hivi nitakutengenezea utaratibu wa kukusaidia ili uweze kurudishwa Dar-es-Salaam, uangalie wazazi wako.

Mheshimiwa Spika, sasa bahati mbaya hakuwa mvumilivu. Katoka hapo, kaenda tena kwa watu wawili, watatu na wao akawapa habari hiyo hiyo, mwisho akagundua hapa namna pekee ya kuhama ni kukimbilia Upinzani nikaseme hii habari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli, ilipokuja tena Bungeni miezi mitatu baadaye kama hoja kwamba, amehamishwa kwa sababu hii, badala ya kuja kwamba, anaomba kurudi Dar-es-Salaam kwa kweli wala sikuijibu na ilikuwa inamsaidia yeye kule aliko ajue kwa sababu, Uhamiaji waliomba kuwa Askari na ukiwa Askari namna nyingine ya Waziri wako kukukumbusha yeye ni Waziri, ukipitisha hoja kupitia upande ambao sio, Waziri anaacha tu kujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sijafuatilia, lakini, bado taarifa yangu ninayoizingatia ni ile kwamba, wazazi wake wagonjwa sana. Kwa hiyo, nitafuatilia afya ya wazazi wake, kwa hiyo, kama kuna mazingira ya kusaidia afya yao iimarike, tutamsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu lingine ni hoja ya Mheshimiwa Zambi, kwamba, Uhamiaji wachape kazi kwa juhudi, tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Kibona, kwamba, Kituo cha Uhamiaji kijengwe kule Isongele; tumeshapata kiwanja, kwa hiyo, tunahangaika na hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo lilichangiwa ni *issue* ya ndugu zetu *Albino.* Mheshimiwa Barwany, alisema amefadhaishwa sana kukuta kwamba, katika Hotuba ya Waziri, haijaongelea kabisa habari ya *Albino.*

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri katika Bunge lako kwamba, kwa kweli, habari ya *Albino* na habari ya Wazee; maana yeye anasema Wazee tumewaongelea sana, lakini *Albino,* hatukuongelea. Habari ya *Albino* na Wazee, haikuwepo kwenye Hotuba yangu, hii ya wazee niliongeza wiki moja hivi iliyopita, ndio niliiongeza kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, nilitembelewa hapa na Wawakilishi wa Wazee kutoka nchi nzima, walikuwa karibu 20 na wakaniuliza umesikia kwenye Redio Tamko letu? Nikawaambia sijasikia; wakasema Tamko letu limesema hivi, yalipoanza mauaji ya *Albino,* Jeshi la Polisi na nguvu zote za Serikali, mmeelekeza mpaka mmeyakomesha, lakini mauaji ya Wazee miaka nenda, miaka rudi mnashindwa kuyakomesha. Kwa hiyo, kwa kweli, Serikali, mnapendelea *Albino,* mnatuchukia sisi Wazee.

Mheshimiwa Spika, sasa ikanisumbua, nikasema hawa wazee nawapozaje? Ndio nikazungumza nao, nikawaambia Wazee, basi nitaweka kwenye Hotuba yangu; ndio msingi wa kuiweka pale.

Mheshimiwa Spika, sasa kumbe hapa leo Mheshimiwa Barwany na yeye kachachamaa. Basi, pale wakati Mheshimiwa Barwany anaongea, mimi mwenzenu jasho

limenitoka, nikasema sasa haya mambo ya kufurahisha watu, nijaze kwenye Hotuba, sasa inafumuka ya ambaye yuko ndani ya Ukumbi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Barwany, nikuhakikishie tu kwamba, hatujapuuza suala la matatizo ya *Albino;* katika kipindi kilichopita tumepeleka zaidi ya kesi 11 Mahakamani na watu 13 wamehukumiwa kunyongwa kwa kuwaua *Albino* na tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabati na Mheshimiwa Kilufi, waliongelea habari ya Wanasiasa kuhamasisha raia kuvunja Sheria. Nitumie nafasi hii kuwaomba tu Wanasiasa na hasa Waheshimiwa Wabunge, kwa kigezo chochote ambacho mtu atataka kuweka, nchi inaongozwa na vyombo vitatu; Bunge, Mahakama na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hakuna namna ambavyo chombo kimoja sio kiongozi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, wote ni viongozi. Waheshimiwa Wabunge, wote ni viongozi wa nchi yetu, tuna dhamana ya kusimamia utawala wa Sheria katika nchi yetu. Kosa kubwa kuliko yote tunaloweza kufanya, ni kupuuza Utawala wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Wabunge, tutimize wajibu wetu huo kwa moyo wa upendo, kwa kutambua kwamba, tunalitumia Taifa letu. Nchi yetu si kwa matumizi yetu peke yetu, maana kuna Mheshimiwa Mbunge alisema, naomba mambo haya ya vurugu yatokee wakati nimekufa. Tafadhali! Tuna watoto na wajukuu, tunataka na wao waikute nchi yetu imetulia, tuwarithishe nchi ya amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sabreena Sungura, aliongelea habari ya ubambikizaji wa kesi. Ni kweli, ziko tuhuma mbili, tatu za ubambikizaji wa kesi na zingine tumekuwa tukichukua hatua. Siku za karibuni tumechukulia hatua Askari na Maafisa kadhaa kutokana na tuhuma hizo. Yako wanayoyafanya kwa makusudi kwa nia ya kupata

rushwa, lakini yako mengine wanayofanya kwa kutotafsiri Sheria sawasawa. Kwa hiyo, ni suala tu la kuchambua lipi limefanyika kwa misingi ipi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wako wale ambao ukienda Magerezani, muda wote atakwambia amebambikiwa kesi. Nilikwenda Gereza la Bukoba Mjini, nikawauliza wafungwa pale, waliobambikiwa kesi, walioonewa ambao kesi si zao wainue mikono, wakainua wote, wote wamesingiziwa. Nikampa nafasi mmoja atueleze ilikuwaje akasingiziwa.

Mheshimiwa Spika, alipoinuka akaeleza kwa uchungu sana, akataja majina ya Askari waliomsingizia, lakini mwisho akajisahau akasema Mheshimiwa Waziri, hawa jamaa Polisi wanavyotufuatafuata sisi siku zote tunaua, wao tunawakimbia hatuwaui, tutaanza kuwaua na wao. Tukasema ooh, sasa amekataa nini anakubali nini?

Mheshimiwa Spika, baadaye nikaambiwa kumbe ni katika majambazi sugu, yaani wakisikia ametoka nje ya Gereza, mji mzima wa Bukoba unachanganyikiwa kwamba, sasa sijui nini kitaendelea hapa. Kwa hiyo, ni mambo ya kupima tu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vita kawawa, aliongelea habari ya kutumia *Triangle* badala ya miti na majani barabarani; tunakubaliana na yeye kwamba hilo ni sawasawa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tundu Lissu, yeye aliongelea ukimya wa Serikali, kuhusu suala la udini na mimi niseme tu kama ambavyo watu wengi ambao wameongea wamesema kama Viongozi wa nchi, kwamba, sio muda wa kutuhumiana kwamba, nani amekuwa kimya, nani hajawa kimya.

Mheshimiwa Spika, ukiomba kura kupitia Makanisani, ukiomba kura kupitia Mapadri, Maaskofu na Wachungaji, watu wakisema wewe ni mdini hutakiwi kulalamika,

unatakiwa kuacha. Ukiomba kura kupitia Misikitini, ukitumia Masheikh, Maimamu na wengine, watu wakisema wewe ni mdini, hutakiwi kulalamika, unatakiwa kuacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliotwambia kwamba, nchi yetu haina dini, tusichaguane kwa misingi ya dini, hawakuwa wajinga. Werevu wetu ndio unaotufikisha hapa leo. Tunafikiri tukishamaliza kutumia Kanisa kuingia Ikulu, baada ya hapo tutatawala salama na watu watasahau kwamba, tulitumia dini au tukishamaliza kutumia Msikiti watu watasahau baada ya uchaguzi, haiwi hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa tutafanya tu hapa, ndoa za dharura nyingi kweli hapa. Kwamba, jamani, wenzetu hawa waliwahi kusingiziwa; ukishasema hivyo, moyoni mwako sema niliwahi kutumia Msikiti kuomba kura? Niliwahi kutumia Kanisa kuomba kura? Nilitimiza wajibu wangu kwa Taifa langu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukijiuliza hivyo, dhamira yako itakwambia hukutimiza wajibu wako na ukifika hapo, jirekebishe bila kuona aibu, kujirekebisha ni uungwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Tundu Lissu, alitaka baadhi ya watu waone uwezekano wa kujiuzulu. Niseme tu kwamba, wanachohangaika watu siku zote kwenda kuomba kura huko barabarani, wanaomba kura kwa wananchi ni kutafuta mamlaka ya kufukuza na kuajiri. Wengine pia wanaanzisha Ofisi zao wawe na mamlaka ya kufukuza na kuajiri. Mtu atanishangaa sana akiona naenda kule CHADEMA, halafu nasema huyu Katibu Mkuu hafai, toa; umemuweka wewe?

Mheshimiwa Spika, moja ya mbinu rahisi sana za kujua Nchimbi kachanganyikiwa, nitakapokwenda CHADEMA kuwaambia fukuzeni Katibu Mkuu wenu. Watajua Nchimbi, hapa ana matatizo makubwa. Kama una hamu ya kufukuza Mawaziri, gombea Urais. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh na Mheshimiwa Ritta Kabati, waliomba bajeti ya Wizara ya Polisi iongezwe, tunakubaliana nao kwa kweli, tunahitaji sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sara Msafiri, yeye aliomba leseni za madereva ziweze kuweka rekodi ya makosa wanayoyafanya barabarani. Leseni zetu zinaweza kuweka rekodi, hizi tulizonazo sasa, lakini mitambo ya kusoma bado haijaweza kutosheleza kila mahali na kuukamilisha huo mfumo, ushauri mzuri, tunaufanyia kazi ili uweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Idd Azzan, aliongelea kudhibiti madereva walevi na ni kweli, hoja ipo kwamba, mtu unakutwa umelewa, unatozwa faini, halafu unaendelea na safari. Kwa kweli ni muhimu mtu akikutwa amelewa, aachwe kwanza pombe itoke kwa hiyo, nasema hili jambo ni nyeti, tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa David Kafulila aliongelea habari ya mageti matano kule njia ya Uvinza. Niseme ni jambo linalozungumzika, tutaangalia mazingira yake ya kiusalama na nini halafu tulione likoje.

Mheshimiwa Spika, halafu Mheshimiwa Kafulila, Mheshimiwa Lembeli na Mheshimiwa Clara waliongelea habari ya kuwepo kwa rushwa katika *traffic,* nakubaliana nao tunalo tatizo la rushwa katika *traffic,* linaudhi na linakera. Nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunajipanga kuchukua hatua, ngumu sana kulimaliza moja kwa moja, lakini tunataka tufike mahali kila anayechukua rushwa ajue kwamba, akikutwa hataweza kusawazisha uharibifu utakaopatikana kwa jambo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mustapha Akunaay alitaka askari wasilewe kazini, tunakubaliana naye, ndiyo utaratibu *actually,* ndivyo ambavyo askari anapaswa ajiheshimu. Lakini vilevile alitaka vijana wanaojihusisha na ulinzi wa Polisi jamii, wanaofanya kazi ya kudhalilisha jeshi letu wachukuliwe hatua na wadhibitiwe, nalo nakubaliana naye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aliko Kibona alitaka tathmini ya Polisi jamii ifanyike ili tujue kama kweli inatusaidia mpaka sasa. Ni kweli, yapo maoni kwamba, kuna watu wanadhani Jeshi la Polisi limekuwa dhaifu sana kutokana na mabadiliko haya, wamekuwa wapole mno, lakini mambo haya ni ya kisayansi lazima uyafanyie utafiti.

Mheshimiwa Spika, tumepata msaada kutoka *COSTECH* wa zaidi ya milioni 300 kwa ajili ya kufanya tathmini ya maboresho ya Jeshi la Polisi ambayo Polisi jamii ni kipengele tu cha maboresho hayo. Kwa hiyo tathmini hiyo itatusaidia kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, halafu Mheshimiwa David Silinde alilaumu sana na akataka Polisi ivunjwe au iwe kitengo cha JWTZ. Hili limesemewe semewe na mimi nitasema tu kidogo kama ambavyo wengine wamejaribu kulisemea. Polisi wanafanya kazi nzuri sana, yako makosa ya askari wachache ambayo hayasababishi tulivunje Jeshi la Polisi na wala haisababishi Jeshi la Polisi liwe halina maana, wako askari wachache tuseme tu tutaendelea kushughulika na hawa askari wachache.

Mheshimiwa Spika, askari hawa wamefundishwa namna ya kukaa na raia, wamefundishwa namna ya kudhibiti vurugu, kudhibiti wezi, kudhibiti nini. Jeshi la wananchi hawafundishwi kuvunja mguu, wanafundishwa kupambana na adui wa nje ya nchi. Mazoezi yao ya shabaha wanafanya mazoezi ya kulenga kichwa, hawafanyi mazoezi ya kulenga mguu.

Mheshimiwa Spika, Polisi wanafanya mazoezi ya kulenga mguu, Jeshi la wananchi wanafanya mazoezi ya kulenga vichwa. Sasa ni vizuri kulijua jambo hili kwamba, hawa kazi yao ni kulinda mipaka yetu na kupambana na adui wa nje. Nchi za jirani zinatuheshimu zinajua jamaa kozi waliyopewa ya kulenga vichwa wanaijua. Sasa hatutaki mazoezi haya wafanyie kwa Watanzania, tusijipeleke huko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Iddi Azzan alisema upo utoaji mbaya wa silaha kiasi kwamba, kuna watu wakiwa tu na fedha kidogo laki saba na kadhalika wanapata silaha ndani ya siku mbili na tatu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Azzan kuwa, pamoja na kusema yeye mwenyewe pia aliwahi kuniambia nje ya ukumbi wa Bunge, tumelichukua jambo hili kwa uzito kamili, tutalichunguza na inapobidi tutachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub alisema kwamba, kuna baadhi ya Polisi hawajapata mishahara kwa zaidi ya miezi miwili. Jambo hili la kutopata mishahara sijapata malalamiko rasmi, lakini niseme tu kwamba, askari wote wa Jeshi la Polisi na majeshi ambayo yako chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ambao hawajapata mishahara yao kwa maelezo yoyote yale, watoe taarifa kwa Wakuu wao wa Polisi wa Wilaya katika siku saba.

Mheshimiwa Spika, katika siku saba zinazofuata Wakuu wa Polisi au wa majeshi ya Wizara yangu iliyoko kwenye Wilaya hiyo watoe taarifa kwa Wakuu wao wa Mikoa na katika siku saba Wakuu wa Mikoa watoe taarifa Makao Makuu ili tatizo hili tulimalize mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwahakikishieni, katika jeshi hapo nimemaliza, majeshi yameshasikia huko, watatekeleza hilo na tunataka tatizo hili tusiendelee nalo kwa sababu kwa kweli siyo jambo jema, hatuwezi kumfanyisha kazi mtu bila kumlipa, si sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu kulikuwa na suala la askari wenye shahada kuchelewa kupandishwa vyeo, hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Pindi Chana na askari wanawake kupata fursa za masomo. Kumekuwepo na malalamiko ya askari wenye shahada ya kwanza na ya pili kutopata nafasi ya kupanda vyeo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kwanza, ni nia yangu kuona kwamba, askari wenye shahada ya kwanza na shahada ya uzamili wanatumika vizuri katika Jeshi la Polisi.

Kwa hiyo, nilikwishaliagiza Jeshi la Polisi kuanza mchakato wa kuwapandisha vyeo askari wenye shahada na mchakato huo umeanza.

Mheshimiwa Spika, malalamiko mliyoyasikia karibuni ni matokeo ya kundi kubwa kupata, kwa hiyo mkirudi kwa wapiga kura wenu wale askari wakiwatembelea, waambieni awamu ya pili ni nyie, wajue tu kwamba ni awamu, lakini maagizo kwa maaskari wenye shahada ya kwanza na uzamili wapande vyeo nimeshaagiza na Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza wameshaanza kutekeleza. Kwa hiyo utekelezaji ndiyo uliozaa malalamiko hayo. Kwa hiyo, muwahakikishie kwamba, tunajua jambo hili.

Mheshimiwa Spika, halafu Mheshimiwa Sabreena Sungura aliongelea habari ya Ofisi za CCM ambazo ziko sehemu nyingi nchini ziwe Vituo vya Polisi. Nilikuwa na rafiki yangu mmoja alikuwa anasema, yeye akienda hotelini hawezi kutoka bila kuondoka na taulo, bila kuondoka na kikombe, yaani mradi chochote, ikiwa mazingira hayaruhusu hata kijiko tu, sasa ile ni hamu ya kuchukua mali ambazo siyo zako ambayo ikikolea sana unaanza kuwaza Ofisi za wenzako za CCM na nini. Kwa hiyo, ni hamu tu inakuwa imekolea sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala la magari mabovu kusindikiza Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, tumechukua hatua, kwanza, tumepeleka milioni 30 kwa ajili ya kurekebisha, lakini tutachukua hatua zaidi ili vyombo wanavyotumia vifanane na hadhi yao.

Mheshimiwa Spika, halafu Mheshimiwa Titus Kamani aliongelea habari ya Kata ya Itilima kutokuwa na gari, Itilima wana gari pengine lina matatizo tu, lakini Busega ndiyo hawana gari tutazungumza naye tuone tunafanya nini.

Mheshimiwa Spika, halafu Mheshimiwa Lolesia Bukwimba aliongelea habari ya vitendea kazi kwenye Jimbo

lak,e tutaifanyia kazi. Mheshimiwa Mfutakamba aliongelea habari ya kujenga vituo vya Polisi kwenye Jimbo lake na yenyewe tutaifanyia kazi hali ikiruhusu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gerson Lwenge aliongelea habari ya Ofisi na nyumba ya *RPC* kule Mkoa mpya wa Njombe, tumesikia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema aliongelea habari ya kujengwa Kituo cha Polisi cha Marangu, Polisi wameshachangia milioni 30, lakini tutazungumza naye tuone nini tunaweza tukasaidiana zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Cyril Chami aliongelea habari ya Kituo cha Polisi cha Wakaoni ambacho mkataba wao ni milioni 329, Jeshi la Polisi kupitia *IGP* wameshachangia milioni 77, Kamati ya Kijiji imeshalipa milioni 122, utaratibu ni kwamba, Kamati ya Kijiji itamalizia fedha iliyobaki lakini tutaendelea kulizungumza tuone tunavyosaidiana.

Mheshimiwa Spika, suala la upungufu wa *radio call* kule Zanzibar ,tumepeleka *radio Call* 10 siku za karibuni ili kupunguza tatizo la mawasiliano na kituo cha Bumbwini kimeshapelekewa fedha za ukarabati. Tutaendelea kuboresha kadiri hali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Akunaay amezungumzia suala la gari katika Kituo cha Haidom, halijawahi kutolewa gari kwa kituo hicho, kwa hiyo tutazungumza naye ili atuelimishe zaidi habari hiyo ilikuwa lini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la rufaa ya Mheshimiwa Mnyika kwa Waziri tunaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mariam Kasembe aliongelea kuhusu taarifa za mapema za uhalifu kama *message* na nini. Niseme tu, ni kweli kwamba, tuna matatizo

ya matumizi ya simu za mkononi, wengine wanazitumia kwa kutukana wenzao, kutisha wenzao, yaani hazitumiki vile ambavyo inapaswa kutumika.

Mheshimiwa Spika, tumelizungumza na hata katika mitandao yetu, ingieni kwenye mitandao yetu ya kijamii ukute vijana wa Kitanzania wanavyosukumiana matusi humo. Huwezi kuamini wanatoka kwenye nchi inayoitwa imestaarabika. Haya ni mambo ambayo tunayazungumza kwa sababu ni kansa katika Taifa. Ni jambo ambalo inatakiwa kama Serikali tuchukue hatua ya namna gani tunamalizana nalo. Tumeanza kulifanyia kazi ili tuondokane na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Maryam Msabaha aliongelea suala la Wakenya kujaa katika hoteli za Kitalii za Zanzibar. Taarifa tulizonazo Wakenya walioko kwenye Hoteli za Zanzibar za kitalii ni 129. Kati yao nane ndiyo waliondolewa nchini kwa kukosa vibali halali, lakini ndiyo mambo ya ushindani, maana Wakenya Dubai wako 70,000, wanafanya kazi hii na nje ya nchi yao kwa ujumla wao wako milioni moja na laki nane.

Mheshimiwa Spika, ukipita kwenye *website* ya Ubalozi wao utakuta wanavyohamasishana namna ya kurudisha fedha nyumbani kufanya kazi za kujenga nchi yao na utaratibu wamewekeana wa kurudisha fedha.

Mheshimiwa Spika, nadhani na sisi kwetu ni changamoto maana ama sivyo tutakuwa tunalia tu, jamani wako saba, wako nane, wamekuja tena, wengine wameongezeka wawili, halafu matokeo yake hatuwezi kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono, hatua inayofuata, Katibu!

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 14 – Jeshi la Zima Moto na Uokoaji

Kif. 3001 – *Fire and Rescue Services*… … sh. 9,882,951,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 – *Fire and Rescue Services Training Institute*… … … … … sh. 2,272,044,000/=

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ni *subvote* 3002, kifungu cha 220800, *Training-Domestic*. Fedha zinazoombwa hapa za shilingi milioni 747 ningetaka kujua kama *training* hii inafanyika kuhusu uwezo wa kuwawezesha wataalam wa zimamoto kukabiliana na matatizo ya moto hasa kwenye maghorofa marefu ya zaidi ya ghorofa 30 na kuendelea. Naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni hela ambazo zimepangwa kwa mafunzo ya kuongeza uwezo wa Jeshi la Zimamoto katika nyanja nyingi ambazo tunazi-*cover* ikiwemo hii ambayo amesema Mheshimiwa Mbunge.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3003 – *Fire Safety*… … … … … … … sh. 509,480,000/=

**MHE: LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu cha 3003, *Fire Safety,* kasma 220300, *Fuel, Oils and Lubricants* kinaombewa milioni 16 kinyume na

mwaka jana. Nahoji watawezaje kumudu kwa chini ya nusu ya kiwango ambacho walitumia kwenye bajeti ya mwaka jana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala haya ya manunuzi tumeonelea *bought purchases* zifanywe *Headquarters,* kwa hiyo kwenye hizi tumepunguza ziko kwenye *administration.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3004 – *Operations*… … … … … … ... sh. 191,200,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3005 – *Dar es Salaam Regional Office*… … … … … … … … sh. 389,279,000/=

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hii *subvote* 3005, kifungu 220300, *Fuel, Oil and Lubricant,* naona mwaka jana ilikuwa milioni 47, lakini mwaka huu milioni 25, kwa nini ipungue namna hii wakati shughuli za *fire* kila siku wanalalamika kwamba, kuna matatizo ya kufika, inakuwaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yangu yanafanana na kile kifungu kilichopita.

**MWENYEKITI:** Kwamba wananunuliwa *centrally.*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** *Yes.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3006 – *Arusha Regional Office*… … … sh. 314,714,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3007 – *Dodoma Regional Office*… … sh. 286,072,000/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 3007, kasma 230400, *Routine Maintenance and Repair of Vehicles and Transportation Equipment,* sasa hivi inaombewa milioni 60 mwaka jana iliombewa milioni 13. Napenda maelezo kwa nini sasa hivi imeongezeka karibu mara nne.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwamba, vifaa ambavyo vinafanyiwa *maintenance* vimechakaa zaidi kuliko mwaka jana, lakini lingine ni kwamba, tunajaribu kupanua *outreach* ili tuifikie Tanzania kwa kiasi kikubwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3008 – *Mwanza Regional Office*… … sh. 352,532,000/=

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu kidogo 410600, Kuna shilingi 2000 imewekwa kwenye kifungu hiki na hii 2000 imeweka kwenye *almost* Mikoa yote katika vifungu vyote, naomba kujua ni ya nini isipokuwa tu Mkoa wa Ilala ndiyo imewekea shilingi milioni 9 Mikoa mingine yote shilingi 2000, naomba tujue ni za nini hizo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 2000 ni *token.*

**MWENYEKITI:** Zamani ilikuwa 100 sasa wameongeza.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3009 – *Mbeya Regional Office*... ... ... sh. 309,816,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3010 – *Kinondoni Regional Office*... ... sh. 323,774,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3011 – *Mara Regional Office*... ... ... sh. 239,316,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola, ndiyo Mkoa wa Mara huo.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo Mkoa wa Mara hapo, nilikuwa naona kuna shilingi 2000 tu kwenye kile kifungu cha 410600, elfu 2000?

**MWENYEKITI:** Swali lingine ni kwamba, kwa nini umeweka shilingi 2000/= kila mahali? Wanasema ni ile *token*. Zamani walikuwa wanaweka shilingi 100/=, sasa wanaweka shilingi 2000/=, maana yake hakina fedha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3012 – *Kigoma Regional Office* ... ... ... sh. 226,442,000/=

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nipo kwenye kifungu kidogo cha 220400, *Medical Supplies and Services,* naona hapa mwaka jana ilitengwa shilingi 6,000,000/= lakini mwaka huu ni sifuri. Nataka ufafanuzi kwamba, watu hawa hawatapata huduma hiyo kwa mwaka huu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yaliyobakia hasa ambayo yanahusu *procurement* yanafanywa *Headquarters*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3013 – *Pwani Regional Office* … … ... ..sh. 276,140, 000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3014 – *Manyara Regional Office* … … sh. 226,458, 000/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 3016, kasma 220800 *Training Domestic,* nataka kujua...

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, kifungu gani katika *subvote* ipi? Tuko *sub vote 3015*.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hiyo hiyo.

**MWENYEKITI:** Samahani, ni *subvote 3014.*

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Nataka kujua *Training Domestic*, ambayo kasma yake 220800, imetengewa shilingi 2,000,000/=, lakini mwaka jana waliweza kufanya kazi na sh. 1,000,000/=, nataka kujua ni kwa nini safari hii hawawezi kufanya kazi na sh. 1,000,000/=?

**MWENYEKITI:** Umeharakisha kazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3015 - *Geita Regional Office* … … … ...sh. 184,846,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa jibu swali la Mheshimiwa Leticia Nyerere. Mheshimiwa Leticia uliza tena swali.

**WABUNGE FULANI:** Ameshauliza.

**MWENYEKITI:** Hapana yeye alikuwa ameuliza kabla, sasa ndiyo unapaswa kuuliza.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 3016, *Training Domestic* ilikuwa imepangiwa sh. 2,000,000/=, lakini mwaka wa fedha uliopita ilikuwa imepangiwa *eleven million*.

**MWENYEKITI:** *Subvote* 3015, hiyo ya kwako siyo yenyewe.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3016 – *Temeke Regional Office* ... ... ... sh. 356,464,000/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 3016, kasma 220800, *Training Domestic,* ilikuwa imepangiwa sh. 2,000,000/=, lakini mwaka wa fedha uliopita ilikuwa imepangiwa milioni 11.2. Naomba *explanation* hii shilingi milioni mbili inafanya aina gani ya *training* ambayo mwaka jana ilifanyika kwa shilingi milioni 11.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa kwa ajili ya mafunzo tumezitenga kwenye Chuo cha Mafunzo ya Zimamoto na hizi ni kwa ajili ya mambo madogo madogo, zitatosha na zitabaki.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3017 – Singida *Regional Office* ... ... ... sh. 222,110,000/=
Kif.3018 – Tabora *Regional Office* ... ... ... sh. 287, 694,000/=
Kif.3019 – Iringa *Regional Office* ... ... ... ...sh. 257, 370,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3020 – Rukwa *Regional Office* … … … sh. 222, 794,000/=

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimechanganyikiwa kidogo katika Mkoa wa Rukwa hapa. Kasma 220300, *Fuel*, *Oil*, *Lubricants*, shilingi milioni 38 na Rukwa hawana hata gari, tuna *land rover* tu.

**MWENYEKITI:** Hebu, taratibu, tafadhali, hatujakusikia, hebu anza upya. (*Kicheko*)

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Halafu Mikoa yote kuna magari na wametengewa hivyo hivyo, lakini huku hatuna hata magari, tuna *land rover* tu!

**MWENYEKITI:** Aah! Hatuendi hivyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3021 – Ruvuma *Regional Office* … … …sh. 232, 690,000/=
Kif. 3022 – Kagera *Regional Office* … … … sh. 252,996,000/=
Kif. 3023 - Mtwara *Regional Office* … … … sh. 240,180,000/=
Kif. 3024 - Lindi *Regional Office* … … … … sh. 228,874,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3025 – Njombe *Regional Office* … … … sh. 213,610,000/=

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimamia kwenye *subvote* 3025, lakini nikianzia na kifungu hiki cha 220100 na hii inajitokeza mpaka vinavyoendelea chini. Je, ni kwa nini, huu ni Mkoa mpya, lakini mwaka jana huu Mkoa pamoja na mikoa mingine mipya walipangiwa fedha, fedha hizi zilikwenda wapi na hii Mikoa imeanza mwaka huu?

**MWENYEKITI:** Aisee! Umenionea Mkoa wangu ndiyo unataka kuuliza, walikuwepo na walifanya kazi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani majibu, lakini umemwelewa swali lake?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa za Serikali zikibaki huwa zinarudishwa Hazina.

**MWENYEKITI:** Hazikubaki hii Mikoa ilianza kabla ya hapo, eeh! Ilianza kabla ya hapo wakawa na shughuli za kufanya.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Nimekumbuka! Pesa ambazo zilikuwa zimetengwa mwaka jana zilikuwa zinatoka Makao Makuu na kulikuwa hakuna *subvote* hizi.

**MWENYEKITI:** Hazina mnaweza kutwambia nini? Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Lukuvi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU(SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Mikoa hii imeanza na nakumbuka hata fedha zao tuliomba na hizi fedha ni kidogo kweli, lakini sehemu kubwa ya watumishi katika Idara mbalimbali zilikuwa hazijakwenda. Hata hivyo, hizi fedha zilikwenda na zimetumika katika maandalizi na mwaka huu tumeimarisha ikama yetu katika hii mikoa mipya na ndiyo maana sasa tumeomba fedha nyingi zaidi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Amechagua Njombe ili sijui nisemeje? Haya!

Kif. 3026 – *Shinyanga Regional Office* … … sh. 291,994,000/=
Kif. 3027 – *Ilala Regional Office* … … … … sh. 359, 386,000/=
Kif. 3028 – *Kilimanjaro Regional Office* … … sh. 291,784,000/=
Kif. 3029 – *Morogoro Regional Office* … … sh. 279,430,000/=

Kif. 3030 – *Katavi Regional Office* ... ... ... sh. 220,158,000/=
Kif. 3031 - *Tanga Regional Office* ... ... ... sh. 275,398,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3032 – *Simiyu Regional Office* ... ... ... sh. 204.788,000/=

**MHE. SUZAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama nimemwelewa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, wakati akizungumzia Mkoa wa Njombe alisema kwamba, fedha zile zilitumika kwa ajili ya maandalizi. Naomba pia kupata maelezo, ni kwa nini sasa basi, Mkoa huu wa Simiyu pia haukutengewa fedha mwaka jana. *(Makofi)*

**NAIBU AZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kulitokea makosa ya kiutendaji na hivyo hawakutengewa. Hata hivyo, pesa zao mwaka huu zipo na zinapelekwa Simiyu kama kawaida.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 28 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kif.1002 - *Finance and Accounting* ... ... sh. 1,812,184,100/=

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa, umesimama. Hapa siyo mshahara wa Waziri hapa ni Jeshi la Polisi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001- *Police Main Force* ... ... ... ... sh. 132,845,725,100/=

**MHE. JAMES MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kifungu 2001, kasma ya 220800, *training domestic,*

mwaka juzi ilikuwa milioni 83, mwaka jana shilingi milioni 126, mwaka huu ni shilingi bilioni sita, kutoka shilingi bilioni 126 mpaka bilioni sita. Nataka nipate ufafanuzi, je, hii *operation* kali kiasi hicho ni ya namna gani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Wabunge wameonesha katika michango yao, *operation* za Jeshi la Polisi zimezidi kupata changamoto mpya hivyo kuhitaji fedha zaidi.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye kasma 221100, *Travel Out of Country*, mwaka jana kulikuwa na shilingi milioni 394, lakini mwaka huu imepangwa shilingi milioni 628. Naona fedha hizi ni nyingi sana, hebu nipate maelezo kwa nini zikawa nyingi sana sasa hivi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatekeleza maelekezo ya Wabunge ili askari wetu wajifunze zaidi mbinu za kisasa ambazo hatuwezi kuzipata ndani ya nchi peke yake, ndiyo maana fedha zimeongezeka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Police Marine*… … … … … ...sh. 1,878,176,000/=
Kif. 2003 - *Railway Police Division*… … … ..sh. 869,289,000/=
Kif. 2004 - *Police Signals Branch*… … … sh. 3,207,549,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2005 - *Police Zanzibar*… … … … … sh. 6,731,036,300/=

**MHE. KIDAWA H. SALEHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 2005, *Police* Zanzibar, kifungu 229900, *Other Operating Expenses* ni vitu gani vinavyojumuisha kifungu hiki,

kwa sababu kwenye bajeti yake ya mwaka jana ilikuwa shilingi milioni 62, mwaka huu ni shilingi milioni 18.6, shilingi milioni 43.4 *less*. Kwa hiyo, labda tuelezwe hiki kinakusanya vitu gani na kwa nini iwe imeshuka hivi. Ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, kifungu hiki kimepungua katika maeneo yote ili kuongeza eneo la *operation* ambalo limeonekana kuwa na changamoto zaidi katika Jeshi la Polisi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2006- *Police Air wing*… … … … … …sh. 2,146,844,000/=
Kif. 2007 -*Tazara Police*… … … … … ... sh. 1,038,287,000/=
Kif. 2008 -*Field Force Unit* … … … … … sh. 7,889,343,200/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2009 - *Traffic Police*… … … … … … sh. 2,166,215,000/=

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niko kwenye kifungu kidogo 410400, *Traffic Police* sasa hivi naona kama wanatumia kamera ambazo zimepitwa na wakati na wanahitaji *equipments* ambazo zinakwenda na wakati. Kwa mfano, *Traffic Police* wakimkamata mtu anayeendesha kwa *speed...*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Owenya uliza swali lako, maelezo yote hayo yanatoka wapi mbona hapo kuna sifuri tu.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kwa nini hawajatenga fedha kwenye kitengo hiki wakati wanahitaji vifaa zaidi kama *Camera* za kisasa.

**MWENYEKITI**: Sawasawa. Mheshimiwa Waziri maelezo!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha, Jeshi la Polisi halikupanga kununua vitu hivi vinavyoitwa *specialized equipments,* ndiyo maana eneo hilo halikutengewa fedha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2010 -*Police Airport*… … … … … … sh. 1,122,602,000/=
Kif. 2011- *Police Dog and Horses*… … … sh. 1,025,068,000/=
Kif. 2012 - *DSM Special Zone*… … … … …sh. 6,917,910,000/=
Kif. 2013 - *Police Ilala*… … … … … … … sh. 5,934,621,000/=
Kif. 2014 - *Police Kinondoni*… … … … … sh. 5,832,054,000/=
Kif. 2015-*Police Temeke*… … … … … … sh. 3,266,176,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2016 - *Police Arusha*… … … … … … sh. 6,685,536,500/=

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma 230900, *Routine Maintenance and Repair of Naval Operations including Sea* iliyotengewa shilingi milioni 20...

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza uko wapi?

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 102, kasma 230900, imeandikwa *Routine Maintenance and Repair of Naval Operations including Sea*. Nataka kufahamishwa kwani sikujua kama Mkoa wa Arusha unapakana na Bahari, hizi *Naval Operations* ambazo mwaka juzi hazikuwa na hela, mwaka jana hazikuwa na hela, ila mwaka huu zimetengewa shilingi milioni 20, maelezo yake nini, kuna bahari ipi Arusha?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, Mheshimiwa Waziri majibu!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, atakapokuwa Waziri Mheshimiwa Tundu Lissu atajua hili ni jina tu la *code*.

**MWENYEKITI**: Eeeh! Rudia tena hatujasikia vizuri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Hakusikia.

**MWENYEKITI:** Hatukusikia!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, jina la kifungu ndiyo linaitwa hivyo, kila mahali kipo na mwaka uliopita fedha hizi zililipwa kupitia fungu la *Main Force*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2017 - *Police Iringa*… … … … … … sh. 3,501,999,100/=

**MWENYEKITI:** Si mnaona hata Iringa hiyo *Naval* ipo, sijui ndiyo nini.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2018-*Police Kilimanjaro……………….Tshs.* 6,177,401,600/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2019-*Police Kigoma………………….Tshs.* 4,987,511,100/=

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nauliza kasma 210300, naona pale posho zimepungua. Mwaka 201 ilikuwa Shilingi milioni 96, mwaka huu ni Shilingi milioni 45, na jinsi ninavyofahamu Kigoma kuna Askari walihamishwa Kibondo mwaka 2011 wakapelekwa Kigoma, hawajalipwa fedha; wengine wamehamishwa, wameletwa Kasulu, wamehamishwa zaidi ya Askari 25 na wanadai muda mrefu. Sasa mmepunguza hizi fedha. Kwa nini mmepunguza wakati kuna madeni makubwa sana ya Askari waliohamishwa Kigoma? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimepungua kutokana na kuanzishwa Mikoa mipya. Kwa hiyo, fedha imepunguzwa karibu kila kifungu cha aina hii ili Mikoa mipya iweze kuhudumiwa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza kwenye ile *item* namba 411000 - *Rehabilitation and other civil works.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafahamika wazi kwamba Askari wetu wanakabiliwa na tatizo la makazi…
fedha ambazo zimetengwa Shilingi milioni 12 ambazo ni kidogo, hivi kweli zitaweza kukidhi mahitaji ya ukarabati pamoja na ujenzi kwa sababu Askari hawana nyumba kabisa ikiwemo katika eneo langu la Kasulu?

**MWENYEKITI:** Safi. Mheshimiwa Waziri naomba ujibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimekuwa ndogo sana kutokana na ufinyu wa Bajeti.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kasma 220300. Ukiangalia pale unaona kwamba ile *Fuel, Oils, Lubricants* imekuwa ikishuka kutoka mwaka uliopita kuja mwaka huu. Lakini Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa Mikoa michache kabisa ambayo ni maalum kabisa katika *operation* ambazo zinahitaji mafuta kwa sababu ni Mkoa ambao una mpaka mrefu kuliko eneo lolote lile katika Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu ni kwamba mpaka sasa kuna wavuvi wa dagaa wanachangishwa mafuta kwa ajili ya Polisi wafanye *operation* maeneo ya Ukanda wa Ziwa. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, ni kwa nini Mkoa wa Kigoma katika eneo hili haupewi umaalum hasa ukizingatia kwamba Mkoa wa Dar es Salaam peke yake unagharimu takribani *one billion Shillings,* Kigoma Shilingi milioni 260; kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni kwa nini Kigoma haipewi umaalum katika mazingira kama hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Aseme ni kwa nini fedha zimepungua ukilinganisha na mwaka 2012? Ndilo swali lenyewe.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimepungua kutokana na mahitaji ya Mikoa mipya.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2020 - *Police Kagera…………………..Tshs.* 5,649,203,800/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba ufafanuzi kutoka kwa Mawaziri, kifungu 210300 - *Personnel Allowances,* ukiangalia *across* Mikoa yote ya Kipolisi, ina *allowance* ya kufanana ya Shilingi milioni 45 wakati tunajua kwamba Mikoa hii inatofautiana kiukubwa na Wafanyakazi pia wanatofautiana. Nilikuwa naomba maelezo kwa vifungu vyote, ni kwa nini *allowance* hii inalingana kwa *across* Mikoa yote?

**MWENYEKITI**: Hapa tukianzia mfano wa Kagera.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo utaona fungu hili ni *Personnel Allowances (Non-Discretionary),* yaani haibanwi kisheria, ndiyo maana inafanana kote. Ni wajibu wa Makamanda kule kutumia busara zao kuona mambo yanakwenda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan Kiwanga nilikuona.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo *sub vote* 2020, kifungu kidogo cha 22100 - *Office and General Supplies and Services*. Sasa ukiangalia hiki kifungu karibu Mikoa yote inafanana, Sh. 46,440,000/=yaani kama wame-*copy* na ku-*paste*. Inakuwaje wakati Mikoa inatofautiana? Nataka majibu yenye uhakika.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Majeshi yetu yana ikama ambayo ina vikosi na *platoon* na nini. Sasa ukitaka yote kuweka hapa, ikama za vikosi mbalimbali na kujua mgao ukoje itakuwa taabu kidogo. Niseme tu, fedha zilizowekwa zimezingatia mazingira ya maeneo yanayohusika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2021 - *Police Lindi* …………………… *Tshs.* 3,800,479,600/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2022 - *Police Mwanza*…………………*Tshs.* 4,497,260,200/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje halafu Mheshimiwa Leticia.

**MHE. EZEKIA D. WENJE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye kasma ya 220300 - *Fuel, Oils, Lubricants.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mwanza una Wilaya saba. Ukichukua fedha iliyowekwa hapa Shilingi milioni 343, ukigawa kwa kila Wilaya, kila Wilaya itapata Shilingi kama milioni 40 na kitu. Sasa swali langu ni kwamba, kama kweli tuko *serious* ili Polisi wapate mafuta ya kufanya kazi, kila Wilaya kwa Mkoa wa Mwanza jinsi ulivyo mkubwa kwa jiografia, tukipelekea kila Wilaya Shilingi milioni 40 na kitu, haitoshi. Naomba nipate ufafanuzi kutoka kwa Waziri, kwa nini hii fedha isiongezwe ili angalau ikidhi mahitaji ya kila Wilaya katika Mkoa wa Mwanza?

**MWENYEKITI**: Kanuni inakataza kuongeza. Kwa hiyo, sema hii fedha kweli itatosha? Kuongeza haiwezekani, ni maelezo tu sasa. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, fedha haiwezi kutosha, lakini katika maombi ya Kamati, kwenye Kamati ya Bajeti na hili pia limeongelewa.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 2022, kasma ya 220100 - *Office and General Supplies and Services*, iko Shilingi milioni 46. Sasa swali langu, ningependa kujua kiwango hiki kimejumuisha Vituo vya Polisi cha Hungumalwa na cha Ngudu, kwa sababu hawana vitendea kazi, *especially computer* hawana?

**MWENYEKITI:** Sijui, haya Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, hii inahusu Mkoa wa Mwanza. Kwa hiyo, watajipanga wenyewe kutegemea mahitaji yao.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2023 - *Police Mara*……………………..*Tshs*. 4,796,900,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko na baadaye Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye *sub vote* 2023, *Police Mara, item* 220700 - *Rental Expenses* ambazo wametenga Shilingi milioni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye randama inaonyesha kwamba hizi ni kwa ajili ya mikutano na vikao. Lakini kama tunavyojua, vituo vingi vya Polisi tunapangisha kwa watu binafsi; lakini ningetaka kujua ni wapi sasa fedha za pango kwa ajili ya vituo hivi vya Polisi ambavyo ni vya kupangisha zimekuwa *allocated*.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri umemwelewa hapo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kulipia mapango zimewekwa katika kasma ya Utawala.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *sub vote*, 2023, kifungu kidogo 220300 kinachohusiana na mafuta, oili pamoja na vilainishi, kuna Sh. 299,700,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka ufafanuzi, nimepiga hesabu hapa kwa Wilaya nne zilizoko chini ya Mkoa wa Mara pamoja na Makao Makuu ya Mkoa, nimepata kwa siku watakuwa na Sh. 150,000/= tu. Sasa Sh. 150,000/= kwa siku ukijumuisha mafuta, oili na vilainishi, nilikuwa naomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri kwa shughuli zilizoko Mkoa wa Mara: Je, hizi kweli Sh. 150,000/= zitatosha kufanya kazi gani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida tu ya maswali mengine yanayofanana na hili, ni kwamba mahitaji ya Polisi kwa gari ni lita 15 kwa siku. Kwa Bajeti tuliyopata ni lita nne kwa siku. Kwa hiyo, jitihada yetu ni kupata hizo nyingine, kwenye Kamati ya Bajeti pia limepelekwa hilo.

**MWENYEKITI**: Haya, Kamati ya Bajeti inabidi ijazwe humu humu ndani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2024 - *Police Tarime – Rorya…………Tshs*. 2,708,836,900/=

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo kwenye kifungu 2024 - *Police Tarime – Rorya.* Katika kifungu hiki, hawajatengewa…

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Nakijata; ni kifungu 221400 ambacho ni cha *Hospitality Supplies and Services.* Kwa Kanda hii ya *Police Tarime - Rorya* hatujatengewa, sijui ni kwa nini. Wenyewe hawahitaji hicho kifungu?

**MWENYEKITI:** Naomba ukitaje hicho kifungu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *item* 221400 kwa Tarime - Rorya hakuna, lakini wengine wote wametengewa. Ni kwa nini Tarime hawajakuwa *allocated* na kifungu hicho cha *Hospitality Supplies and Services?*

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, tunakitafuta hatujakiona.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani kwenye fungu hili hakipo. Sasa nauliza ni kwa nini hakijatengewa kwa Tarime - Rorya wakati kwingine kote wametengewa?

**MWENYEKITI:** *Item* yenyewe haipo?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** *Item* hiyo haipo, lakini kwa wengine wote ipo. Kwa nini Tarime -Rorya hakuna? Ndiyo swali langu.

**MWENYEKITI:** Sasa kama haipo, sijui.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutachukua hatua za kiutawala kuona kwamba wanapata fedha za shughuli hiyo.

**MWENYEKITI**: Naomba utueleze vizuri, hata *sub item* yenyewe haipo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema ni kwamba, kifungu hiki kweli hakipo na kwa umuhimu aliouelezea Mheshimwa Mbunge, daima katika kuendesha Serikali kuna utaratibu wa *reallocation* ya kuona namna ya kutatua maeneo ambayo yamerukwa kwa ajali. Kwa hiyo, jambo hili ni muhimu litafanyiwa kazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2025 - *Police Mbeya........................Tshs.* 6,081,237,600/=
Kif. 2026 - *Police Mtwara......................Tshs.* 4,429,075,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2027 - *Police Morogoro...................Tshs.* 7,184,180,400/=

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma ndogo 220300 - *Fuel, Oils* and *Lubricants.* Naona kwamba mwaka 2012 walitengewa Shilingi milioni 353, lakini mwaka huu ni Shilingi milioni 349. Yaani ndogo zaidi. Nauliza: Je, Mkoa wa Morogoro mmepunguza Wilaya au/ yaani mmepeleka kwenye Mkoa mwingine; kwa nini hali imekuwa hivi, wakati kila siku wanachangishana mafuta mfukoni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, maelezo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti hii ndogo iliyoko hapa ni kutokana na kupelekwa kwenye Mikoa mipya.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2028 - *Police Manyara*.....................*Tshs.* 4,376,272,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2029 - *Police Singida*.......................*Tshs.* 4,429,713,000/=

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nipo katika kifungu kidogo 220300 - *Fuel, Oils, Lubricants.* Mwaka 2012 ilikuwa ni Sh. 329,550,000/=, mwaka huu zimepungua mpaka Sh. 297,600,000/= kama pungufu ya Shilingi milioni 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua ni sababu zipi zimepelekea fedha hizi za mafuta na vilainishi kupungua, ukizingatia Mkoa wa Singida ni mkubwa na una maeneo yamesambaa sana. Nilitaka kujua ni sababu zipi zimepelekea kupungua huko.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwenye vile vifungu vingine, punguzo hilo ni kutokana na kupelekwa kwenye Bajeti ya Mikoa mipya.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 330400 - *Routine Maintenance and Repair of Vehicles and Transportation Equipment,* ambayo mwaka 2011 ilikuwa na Shilingi milioni 12, mwaka 2012 ilikuwa sifuri na mwaka huu ni sifuri; nataka kujua Mkoa wa Singida hauna magari yanayohitaji *repair* ya Polisi au hauna magari kabisa au nini? Kwa nini hiki kifungu ambacho kinahusu matengenezo ya magari ya Polisi kimewekewa Shilingi sifuri kwa Mkoa wa Singida kwa miaka hii miwili ambayo imepita?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki hakijawekewa fedha kutokana na mahitaji ambayo yanaasisiwa na Mikoa yenyewe kuhitaji matengenezo makubwa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu hicho hicho alichouliza Mheshimiwa Tundu Lissu, lakini bahati mbaya mwenzangu *data* hana. Mkoa huu una magari manne yako juu ya mawe, sasa nashangaa hapa haijatengwa hata senti tano. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2030 - *Police Pwani……….................…..Tshs.* 5,408,213,200/=

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 2030, kasma ya 220300, inayohusu petroli, mafuta na vilainishi, mwaka 2012 fungu hili lilitengewa Sh. 331,700,000/= mwaka huu zimepungua na kutengewa Sh. 297,600,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufahamu, kutokana na ukubwa wa Mkoa, maeneo mengine huwezi kufika mpaka upande maboti, ambayo yanachukua zaidi ya lita 200 na kitu, kigezo kipi kimetumika ili kupunguza kasma hiyo wakati tulikuwa tunahitaji tupate zaidi ili kuonyesha ufanisi wa kazi wa Askari wetu wanaotulinda.

**MWENYEKITI:** Hehehee! Mimi jibu nalijua. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu yangu yasikukere. Jibu ni hilohilo kwamba tumehamishia fedha kwenye Mikoa mipya.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Sasa msiulize swali linalofanana, eeh! Haya, tuendelee.

Kif. 2031 - *Police Ruvuma………………….Tshs.* 3,992,353,700/=

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, *sub vote* 2031 kasma 221000 - *Travel in Country*. Naomba kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa nini kasma hii imepungua kwa zaidi ya Shilingi milioni 26 ilhali Mkoa huu ni mkubwa sana. Mkoa huu umeongezeka Wilaya moja ya Nyasa, na Mkoa huu una wahalifu wengi ambao wanavuka nje ya mpaka kupitia Ziwa Nyasa, na vilevile kupitia Mto Ruvuma kwenda Msumbiji. Tulitegemea kwamba kasma hii ingeongezeka fedha kuliko kupungua. Naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hasa ukizingatia kwamba Mkoa huu yeye anaufahamu zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma ni moja ya maeneo ambayo shughuli za kiooperesheni zinatakiwa kuimarika zaidi. Kwa hiyo, fedha zimehamia kwenye uimarishaji wa shughuli za operesheni pamoja na Mikoa mipya.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

kif. 2032 - *Police Rukwa*……………………Tshs. 2,791,004,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mipata!

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kuhoji kifungu kidogo cha 220300 kimetengewa pesa chache, karibu nusu zimepunguzwa na huku Mkoa huu umeongezewa Wilaya, Wilaya ya Matai imekuwa mpya, lakini pesa zimekuwa chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukanda mkubwa sana wa mwambao tunapakana na *DRC* ambayo hali ya usalama ni tete sana. Nataka kujua kwa nini pesa zinapungua badala ya kuongezeka?

**MWENYEKITI:** Mambo ya *fuel, oils and lubricants.* Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa fedha hizi pia kumetokana na kuanzishwa kwa Mikoa mipya ambayo nayo inahitaji mambo mbalimbali.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima)*

Kif. 2033 - *Police Shinyanga*.................. Tshs. 3,686,906,800/=

**MWENYEKITI:** Aaah! Jamani imeshagonga. Kwani wewe Shinyanga tena Mheshimiwa Mkosamali?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza tu kwa sababu majibu ni yaleyale, lakini nataka kujua kifungu hiki cha *oil, fuel and lubricants* fedha zinapungua kila mahali lakini pia kuna fedha ambazo ni za ku-*travel in the country*. Sasa wakati wa ku-*travel* watu wananunua mafuta pia. Sasa tofauti ni nini na kwa nini walianzisha Mikoa mipya bila kuwa na bajeti ya hiyo Mikoa? Kwa nini wanataka kupunguza fedha kwenye Mikoa mingine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ni suala la kisera, subiri kwenye mshahara kule. Maana yake utazungumza jumla tu. Lakini hapa tunazungumzia fedha iliyo kwenye *sub item* au *item* ndogo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2034 - *Police Tabora* ...................... Tshs. 4,329,863,100/=

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nipo kwenye kifungu kidogo cha 410500 - *Acquisition of Household and Institutional Equipments.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufafanuzi kutoka kwa Serikali, hii Shilingi milioini 12 iliyowekwa hapa ina

fungu la kukarabati nyumba ya watumishi Kituo cha Urambo ambayo paa liliezuliwa tangu mwaka 2011 mpaka leo halijarudishiwa na watumishi waliokuwa wanaishi kwenye nyumba ile familia nne zimejibanza kwenye nyumba za watumishi wenzao na hali ni mbaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

**MWENYEKITI:** Kwamba hizi fedha zinafanya kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilizotengwa katika kifungu hiki hazina uhusiano na kazi aliyoongea Mheshimiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2035 - *Police Tanga* ………………… Tshs. 5,463,886,400/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2036 - *Police Mjini Magharibi* …………Tshs. 8,541,101,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chomboh!

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua tu Jeshi letu la Polisi la Tanzania ni pamoja na Mikoa yote ya Zanzibar, lakini kwa nini kifungu cha 2036 na vingine vyote vya Mikoa ya Zanzibar havina huduma kama vifungu vingine vya Mikoa mingine yote kama vile *communications and whatsoever*? Ni vitu vinne tu pale; moja, mbili, tatu, nne, tano na sita. Hizi huduma nyingine kwa nini Mikoani kwetu hatupati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umemwelewa swali lake?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yetu ya Kipolisi yamepishana na ni vikosi vyenyewe, kwa maana ya kwamba kama ni Zanzibar Kamanda wa Polisi au Kamishna wa Zanzibar ndiye anayepanga na timu yake mahitaji yake muhimu na ndiyo yanayozingatiwa na Makao Makuu.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye *item 229900* ambayo inasema *other operating expenses* ambayo mwaka 2012 ilikuwa Sh. 161,250,000/= lakini safari hii imekuwa Shilingi milioni 12, kimepunguzwa kitu gani? Naona hiki kifungu chenyewe toka hapo ni kidogo, halafu tena hizo fedha zimepunguzwa. Sasa nataka nipate maelekezo au maelezo zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nimepapata. Mheshimiwa Waziri, kwa nini zimepungua sana?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kupungua kwa kifungu hiki ni ile ya uanzishwaji wa Mikoa mipya, lakini pia mahitaji ya wakati huu kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Umekiona kifungu chenyewe? 229900 kimetoka Sh. 161,250,000/= mpaka Shilingi milioni 12, ndiyo sababu hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo siyo matamu, lakini ndiyo hayo hayo kwamba zimepungua kutokana na mahitaji ya sasa kama yalivyoainishwa na Zanzibar yenyewe, lakini pia na kuanzishwa Mikoa mipya.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2037 - *Police Kusini Unguja* ……………Tshs. 2,539,613,400/=
Kif. 2038 - *Police Kaskazini Unguja* ……... Tshs. 2,266,152,400/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2039 - *Police Unguja Kusini Pemba*…Tshs. 2,351,428,400/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia, *microphone*.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nipo katika kifungu 220300. Hata kama majibu yatakuwa siyo matamu, lakini nitaomba Waziri aniridhishe. Kwa sababu Mkoa wa Kusini Pemba ndiyo ulio na Bandari, *Airport*; Polisi Mkoa wa Kusini wanatumika katika *escorting* na ujio wa Viongozi wetu. Ni kwa nini pesa za mafuta zimepungua hata ukilinganisha na Mikoa mingine ya Pemba ambayo wamepewa zaidi kuliko Kusini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni kuongezeka kwa Mikoa mipya, lakini itakapotokea dharura watasaidiwa kutoka Makao Makuu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2040 - *Police Kaskazini Pemba* …….. Tshs. 2,437,869,000/=

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo, kifungu hicho kwa ajili ya Kaskazini Pemba. Jibu la Mheshimiwa Waziri kuongezeka kwa Mikoa mipya; Mikoa mipya imeongezeka wapi Zanzibar? Hebu aniambie.

**MWENYEKITI:** Tupo kwenye *items*.

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Hiyo *Sub vote 2040* hiyo hiyo ya *fuels, oils, lubricants 220300*. Sasa hii kuongezeka kwa Mikoa mipya, Zanzibar kumeongezeka Mikoa gani mipya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hilo jibu ni rahisi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi lipo moja tu katika Jamhuri ya Muungano.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2041 - *Police Dodoma* ……………….. Tshs. 6,151,747,000/=

**MWENYEKITI:** Aah, mmechelewa kifungu kimeafikiwa; na wewe ni mafuta?

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni katika *sub vote number 2041 item number 220200 - utilities supplies and service*s.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimepungua karibu Shilingi milioni 30 na umuhimu wa *Police Dodoma* unajulikana. Bunge linakaa hapa miezi mitatu na *Police* wanahitajika sana katika Mkoa wa Dodoma na huduma zao.

Ninaomba kujua kwa nini zimepungua karibu Shilingi milioni 30.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaniua bure na kifungu hiki. Maelezo ni Mikoa mipya imeongezeka na inahitaji pesa.

**MWENYEKITI:** Muamini au msiamini! *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2042 - *Police Geita* …………………… Tshs. 3,711,587,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2043 - *Police Katavi* ………………….. Tshs. 2,677,669,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso. Katavi; ndiyo ninyi mliochukua fedha.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote 220300 - fuel and lubricants.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mpanda ni Wilaya ambayo imekaa katika maeneo ambayo ni mtawanyiko. Fungu hili ni dogo sana kiasi kwamba linaunganisha mpaka maeneo ya mipaka. Naomba Mheshimiwa Waziri aangalie uzito wa aina yake katika eneo hili, kwani limepakana na nchi jirani ambapo usalama wake ni mdogo.

**MWENYEKITI:** Sasa hapa tunazungumzia Mkoa wa Katavi. Ulikuwa na maana hiyo? Haya Mheshimiwa Waziri, hela ndogo naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutazingatia katika bajeti ijayo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2044 - *Police Njombe* ………………… Tshs. 2,856,176,000/=

**MWENYEKITI:** Nami mafuta na Mkoa ule ni wa milima milima. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2045 - *Police Simiyu* ………………….. Tshs. 2,796,786,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Police College Moshi* ……….. Tshs. 5,296,548,600/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mrema!

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuangalie *sub vote 3001 - Police College Moshi,* kifungu kidogo 221710 - *food suppliers and services*, yaani chakula kwa ajili ya wanafunzi, kwa ajili ya mafunzo na madai ya wazabuni ninayoyajua pale *Police College Moshi.*

Mwaka 2012 zilitengwa Shilingi bilioni moja na mwaka huu tena Shilingi bilioni moja, wakati Chuo kile kinadaiwa, kina wanafunzi wanatakiwa wale vizuri ili washibe wawe na nguvu ya kufanya kazi. Naomba Mheshimiwa Waziri hebu anieleze ni kwa nini ananyonga Chuo kile.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mrema tutaizingatia kipekee wakati muafaka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 - *Police College* ……………….. Tshs. 1,809,589,600/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwenye *sub vote ya Police College* sioni kifungu cha mafuta. Sasa sijui *Police College* wao hawana magari na hivyo hawahitaji mafuta!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la *Police College,* fedha za *operation* ndizo zitakazotumika kwenye mafuta.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Police Vehicles Maint. Unit..*….Tshs. 2,171,923,400/=

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza kwenye ile kasma ya 230400, imeongezeka ukilinganisha na mwaka 2012, lakini hii *sub vote* inahusu *maintenance* ya magari. Sasa vifungu vyote tulivyovipitia vingi vina fedha za ku-*maintain* magari, lakini kwenye Wilaya zetu huko mimi sijawahi kuona magari ya Kibondo yakija huku kufanyiwa *maintenance*. Sasa ni nini hii?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Lakini imepungua, haikuongezeka. Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia ya Jeshi la Polisi kufanya *maintenance* ya magari yake yote, lakini ni kutegemeana na fedha zinavyopatikana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *Police Medical Unit* ……..……..Tshs. 2,089,328,300/=

Kif. 6001 - *Police Building Brigade* ………. Tshs. 4,894,631,700/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7001 - *Criminal Investg. Division*..….Tshs. 21,768,087,100/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sabreena, Mheshimiwa Leticia na Mheshimiwa Suzan.

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nipo kwenye *Criminal Investigation Division* kifungu kidogo cha 220100 - *Office and General Supplies and Services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi, mwaka 2012 kifungu hiki kilikuwa kimetengewa Shilingi milioni 131 lakini mwaka huu imekuja mpaka Shilingi milioni 79 na tukiangalia kipengele hiki cha *Criminal Investigation Division*

ni kipengele muhimu sana kwa sababu watu hawa wanahitaji kufanya *investigation* na sasa hivi kuna wizi mkubwa sana umeingia *especially* wa *cyber crimes,* wanaweza ku-*cross check* kuhusu *scammers.* Sasa kwa nini fedha hii imepungua na wakati nchi yetu sasa hivi inakabiliwa na tatizo kubwa na watu hawa *Investigation Department* lazima wafanye kazi kwa sayansi na teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya kifungu hiki inapungua kutokana na mahitaji ya Mikoa mipya lakini pia na ufinyu wa bajeti tuliyopata. Kwa hiyo, kama tutapata nyongeza kutoka kwenye Kamati ya Bajeti, tutauzingatia mchango huo muhimu.

**MWENYEKITI:** Jamani Kamati ya Bajeti msije mkafikiria ndiyo jibu kwa kila kitu. Hakuna!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu cha 7001 chini ya *crimes prevention*, kwenye kasma 221600 - *printing advertising and information supplies and services.* Naona hapa imepunguzwa Shilingi milioni 50 ukizingatia kwamba *printing advertising* ni muhimu sana katika *crime prevention program.* Naomba maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wenyewe wa *crime prevention* waliona katika kupata fedha sehemu nyingine moja ya maeneo ya kupunguza ambayo hayana madhara ni hii.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma hiyo hiyo kifungu kidogo 210500 - *personal allowance in kind.* Naona mwaka 2011 ndiyo walitenga fedha, lakini mwaka 2012 na mwaka huu hakuna, kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa fedha unaokuja haikuonekana mahitaji ya fedha hizo.

**MWENYEKITI:** Hata mwaka 2012 haikuwepo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7002 - *Stock Theft Prevention Unit*......Tshs. 1,242,309,500/=

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *sub vote 7002* kifungu 220300 kinachohusu mafuta pia, nimeona kuna fedha hizi ambazo toka mwaka 2012 zinatengwa kidogo sana ukilinganisha na kazi ambazo hiki kitengo cha wizi wa mifugo ambacho kinahusika Mikoa yote ya Tanzania. Sasa inawezekana ndiyo sababu ya utengaji wa fedha kidogo, inasababisha wizi wa mifugo uendelee kuwepo katika Mikoa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi, kwa nini fedha zinatengwa kidogo kila mwaka kiasi hiki?

**MWENYEKITI:** Ahsante, mwaka huu zimeongezeka kidogo, Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana tu na ufinyu wa bajeti, lakini huko mbele tunavyokwenda tutaendelea kukipa umuhimu kipengele hiki.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 - Jeshi la Magereza**

Kif. 1001 - *Prisons Headquarters* ........... Tshs. 8,325,433,700/=

**MWENYEKITI:** Mimi sijui nani amesimama, maana wapo wengi wamesimama sasa hivi. Mheshimiwa Mngodo!

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma 410 400 - *Acquisition of specialized equipment*. Kiasi cha fedha kilichotengwa mwaka huu kiko sawa sawa na cha mwaka 2012. Sasa ningependa kujua ni *specialized equipment* za aina gani hizi?

**MWENYEKITI:** Zenye bei rahisi namna hiyo? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni vitu vidogo vidogo kwa ajili ya kufanyia kazi za kisayansi na kwa kawaida havihitaji pesa nyingi kwa *nature* yake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Unajua hii Wizara ina vifungu hivyo, tunaweza kulala humu humu kwa maswali yenu hayo. Haya tunaendelea. *(Makofi)*

*Kif. 1002 - Finance and Accounts .......... Tshs. 751,801,000/=*
*Kif. 2001 - Parole Department ................Tshs. 920,027,800/=*
*Kif. 2002 - Prisons Welf. and Rehab.......Tshs. 97,441,861,000/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *Item 221700 - food supplies and services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetengwa Shilingi bilioni 8.24, ningetaka kupata maelezo kwa sababu ni asilimia 20 tu na ni suala la chakula kwa wafungwa na mahabusu wapatao 34,000; ambapo mfungwa mmoja anatakiwa apate Shilingi 3,155 ambayo ni takribani Shilingi bilioni 39 na hapa ni Shilingi bilioni 8.2. Hapa ni suala la ubinadamu na tukitegemea kwamba, sisi sote humu ndani ni wafungwa watarajiwa. Kwa hiyo, tusije tukaenda kule hali ikawa ni mbaya zaidi. *(Makofi/ Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili pia lilijitokeza kwenye mazungumzo yaliyopita. Ni kwamba mahitaji hasa ni zaidi ya Shilingi bilioni 40, lakini tunajibana ili tuweze kuishi. Sasa kama nilivyosema mwanzoni ni kwamba tumepeleka pia maombi kwenye Kamati ya bajeti kulizingatia.

**MWENYEKITI:** Jamani bajeti msije mkaiwekea matumaini hapa. Haina fedha hizo mnazosema wala haiwezi ku-*manufacture*, ni ku-*reshuffle around.* Kama mmesha-*reshuffle so much, don't expect anything*.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *item 220200* fedha za mwaka 2012 zilikuwa Sh. 5,800,000,000/= lakini mwaka huu zimetengwa Sh. 721,283,100/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua kwanini fedha zimetolewa kiasi kidogo hivyo kwa mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakavyoona huko mbele, tumeanzisha utaratibu wa Mikoa ya ki-*prisons*. Kwa hiyo, fedha ambazo zingekuwa hapa ziko kwenye Mikoa tofauti.

**MWENYEKITI:** Aah, hukusimama kabla.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 2003 - Resettlement of Offenders ....Tshs. 2,010,104,000/=*
*Kif. 2004 - Prisons Arusha ........................Tshs. 235,060,000/=*
*Kif. 2005 - Prisons Dar es Salaam ............Tshs. 781,888,000/=*
*Kif. 2006 - Prisons Dodoma ......................Tshs. 381,793,000/=*
*Kif. 2007 - Prisons Kigoma ........................Tshs. 223,511,000/=*
*Kif. 2008 - Prisons Tanga ................. .......Tshs. 303,601,000/=*
*Kif. 2009 - Prisons Kagera ........................Tshs. 279,310,000/=*

*(Vifungu Vilichotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 2010 Prisons Mwanza ........................Tshs. 323,300,000/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wenje, ikiishatajwa Mwanza tu!

**MHE. HEZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kasma ya 230400 - *routine maintenance and repair of vehicles and transportation equipment*; katika miaka miwili mfululizo iliyopita haikutengewa fedha yoyote, lakini mwaka huu wameweka Shilingi milioni 25.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachohoji ni kwamba, hii fedha ni ndogo sana ku-*maintain* yale magari. Hii ni fedha ya tairi tu kwenye ile *bus* inayopeleka mahabusu Mahakamani kila siku. Sasa kwanini wametenga fedha kidogo kiasi hiki? Tatizo ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni ufinyu wa bajeti. *(Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 2011 - Prisons Tabora ……..……………..……Tshs. 303,084,000/=*
*Kif. 2012 - Prisons Mbeya …………….... ……Tshs. 326,720,000/=*
*Kif. 2013 - Prisons Singida …………….. ……Tshs. 278,060,000/=*
*Kif. 2014 - Prisons Coast ……………………..……Tshs. 261,270,000/=*
*Kif. 2015 - Prisons Lindi ………………………..……Tshs. 277,388,000/=*
*Kif. 2016 - Prisons Manyara ………………....Tshs. 263,970,000/=*
*Kif. 2017 - Prisons Mtwara ………….. ….…Tshs. 258,220,000/=*
*Kif. 2018 - Prisons Ruvuma ………. . ….…..Tshs. 247,890,000/=*
*Kif. 2019 - Prisons Rukwa ………….. ………Tshs. 282,050,000/=*
*Kif. 2020 - Prisons Mara ………….. .. ………Tshs. 300,440,000/=*
*Kif. 2021 - Prisons Iringa ……………….. ……Tshs. 270,170,000/=*
*Kif. 2022 - Prisons Kilimanjaro ……….. ……Tshs. 316,420,000/=*
*Kif. 2023 - Prisons Morogoro ………... …….Tshs. 387,024,900/=*
*Kif. 2028 - Prisons Shinyanga ……….. …….Tshs. 282,220,000/=*
*Kif. 3001 - Prisons Staff College …….. …Tshs. 2, 770,093,800/=*
*Kif. 3002 - Prisons Driving School………….Tshs. 407,374,200/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 3003 - Prisons Trade School ……….….Tshs. 837,362,900/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu ufafanuzi, *sub vote* 3003 hii *Prison Trade School* naomba kujua iko wapi na inafanya kazi gani.

**MWENYEKITI:** Hebu, umesema!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri au Naibu, hii *Prison Trade School* ndiyo naisikia kwa mara ya kwanza. Iko wapi na inafanya kazi gani?

**MWENYEKITI:** Yaani hii *sub vote 3003.* Haya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mbunge anauliza kwamba, hajawahi kusikia *Prison Trade School* iko wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, iko Ukonga. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Eeh, majibu mafupi la sivyo tutalala hapa hapa. *(Kicheko)*

*Kif. 3004 - Prisons College Kiwira .........T shs. 1,799,631,100/=*
*Kif.4001 - Prisons Building Brigade .......T shs. 2,147,552,900/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif.4002 - Prisons Industries...................T shs. 948,657,400/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Mbatia!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nauliza *item 230600 -routine maintenance and repair of machinery, equipment and plant.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kujua hii Shilingi milioni 55 kama ilikuwa ya mwaka 2012 kwa sababu samani zote za Serikali tumekubaliana sasa zitengenezwe na

Magereza na zinadumu na ambazo zitaokoa fedha nyingi kwa Taifa. Naomba maelezo kifungu hiki mkakati wake ukoje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili wazo limekuja wakati huu wa bajeti ambapo tulikwishatenga fedha. Hata hivyo, kama italazimika kuna *midyear review* tunaweza tukakirekebisha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif.4003 - Prisons Building Brigade ........T shs. 1,325,110,300/=*

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 403 - *prisons fund.* Kasma 220600 - *Clothing, Bedding, Footwear and Services.* Ningependa nipate maelezo hii *clothing, bedding, footwear and services* kwenye *farming* inatumika vipi kwa sababu hapa wanasema *Prison farms.* Ningependa nipate maelezo hizo nguo na kila kitu kilichotajwa vinatumika vipi kwenye *farming*.

**MWENYEKITI:** Halafu unapotaja *sub votes* zetu ni 4003, siyo 403. Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima pia wanahitaji kuvaa nguo, viatu, sare na vitu kama hivyo. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hao ni wakulima gani? *Prison farms* ni akina nani hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *prison farms* kuna mashamba yetu kwenye Magereza mbalimbali ya wafungwa. Pia kuna wafanyakazi ambao ni raia mmoja mmoja.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

*Kif.1001 - Administration and HR Mgt .....Tshs. 2,045,100,600/=*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Diana Chilolo, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango, atafuatia Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa James Lembeli. Nianze na hawa kwanza. Mheshimiwa James Lembeli.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Serikali wa kuanzisha Mikoa ya Kipolisi…

**MWENYEKITI:** Samahani kidogo, Mawaziri m-*note* watazungumza wote, halafu mtajibu. M-note kwa kuzingatia majina yao.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Uamuzi wa Serikali wa kuanzisha Mikoa ya Kipolisi lengo lake ni kusogeza huduma ya Polisi katika maeneo ambayo yana matatizo makubwa hususan ya kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kahama ni miongoni mwa Wilaya ambazo zina matatizo makubwa sana, hususan ya ujangili, ujambazi, uvamizi na utekaji nyara wa magari na mabasi, jambo ambalo ni muhimu Wilaya ya Kahama ikapewa hadhi ya Mkoa wa Kipolisi.

Sasa nilikuwa nataka kujua, pamoja na kwamba Serikali inafahamu matatizo haya, inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba Wilaya hii ya Kahama ambayo ina migodi miwili mikubwa ambayo inahamasisha watu mbalimbali kukimbilia huko na kufanya ujambazi, inakuwa mkoa wa Kipolisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanuni inasema *one item at a time*, yaani ni *issue* moja tu. Mheshimiwa Diana Chilolo!

**MHE. DIANA M. CHILOLO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa kuzungumza na kwa maandishi, niliikumbusha Serikali jinsi Magereza yetu nchini yanavyotekeleza Sera ya Kilimo Kwanza, na nikatolea mfano Gereza la Manyoni hapa. Magereza mengi nchini wanalima sana kwa jitihada zao wenyewe na wanapata shida ya vifaa; jambo ambalo wanafanya ni jema, wanasaidia sana kuokoa fedha ya Serikali. Nikawa nimeiomba Serikali ni kwanini wasiyapatie magereza haya zana za kilimo, ikiwa ni pamoja na matrekta, hasa kwa Gereza la Manyoni hapa pamoja na Magereza yote yanayojihusisha na masuala ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Wakati nachangia kwa maandishi na nimekuwa nachangia kila mwaka hapa Bungeni, niliiomba Serikali iondoe ndani ya Magereza utaratibu unaodhalilisha watu walioko Magerezani na mahabusu, wa kuwapekua kila siku. Wakati Naibu Waziri anachangia, kwanza amelidanganya Bunge kwa sababu amesema kuna chumba maalum cha kufanyia upekuzi. Yeye hajakaa Gerezani hajui. Tuliokaa Gerezani, tunajua. Wanafanya *open*, hakuna chumba maalum. Kwa hiyo, amelidanganya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri katika mchango wake wakati anajibu hoja amesema wanategemea kuandaa vyombo maalum *(detectors)* lakini iwapo uchumi utaruhusu. Uchumi utaruhusu lini wakati bajeti siku zote ni ndogo? Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iondoe ndani ya Magereza utaratibu huu unaodhalilisha wanawake, Mahabusu na watu ambao wanastahili haki. Huu ni ukiukaji wa haki za binadamu na udhalilishaji ndani ya nchi yetu. Tunaomba utaratibu huu uondoke haraka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango!

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilizungumza, tena kurasa nane. Hii shari iliyotokea Arusha ni kubwa sana. Labda watu tunaiangalia kwa juu juu, lakini ni kama watu hawa wanatu-*beep*, siku moja watatupigia simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi kubwa sana kwa Polisi wakiongozwa na Mheshimiwa Said Mwema, wanafanya kazi nzuri sana. Lakini naelewa kutakuwa na siku sita Serikali itakaa na Kamati ya Bajeti kuzungumzia na ku-*evaluate* mwenendo wote wa jinsi ambavyo bajeti imekwenda. Naiomba Serikali na niko *serious* katika hili, Mheshimiwa Waziri akisimama ajibu vizuri, Serikali ione umuhimu sasa wa kuwaongezea Polisi fedha za kutosha maana wameshatu-*beep* hawa, watatupiga! Naomba Serikali ione kuna umuhimu wa kuongeza fedha ili Polisi wafanye kazi ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anazungumza kama anatania tania, hapana. Anioneshe jitahada yake, yaani ni kiasi gani atakwenda kutafuta hizi fedha ili Polisi wapate fedha za kutosha. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze vizuri atakapojibu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Jeshi la Polisi la kisasa kwa maana ya *a Professional Police Force*, lisilokuwa linaendeshwa kisiasa siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pamoja na michango mingi ya Wabunge, Waheshimiwa Wabunge wamelalamikia sana jinsi ambavyo Jeshi la Polisi linaendeshwa kisiasa na wanasiasa wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba kisheria, chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1997, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, wana mamlaka ya kipolisi *(police powers),'* wanaweza wakaamuru watu

wakakamatwa na kuwekwa ndani. Lakini sheria yetu iko wazi na imekuwa wazi siku nyingi kwamba, Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa, hawezi akatumia mamlaka yake ya kuweka watu ndani kama mahali hapo tayari pana Polisi kwa sababu tayari Polisi wanatakiwa waone kama kosa limefanyika. Polisi wasipoona kosa maana yake ni kwamba, hakuna kosa. Hata hivyo, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, wamekuwa wanashinikiza Jeshi la Polisi wanakamata watu, wanakamata Wapinzani wa CCM, wanakamati Viongozi wa Vyama vya Upinzani, wanazuia Mikutano yao, wanawapiga watu, wanawafungulia kesi za uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hii inaonesha kwamba, Jeshi letu linaendeshwa kwa namna Kisiasa kabisa na haya siyo maneno ya kwangu tu pekee yake; Tume ya Jaji Ihema iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani mwenyewe, ilisema Muundo wa Jeshi la Polisi uangaliwe upya ili Jeshi la Polisi lisitumiwe tena na wanasiasa kunyanyasa watu, kuwanyanyasa upinzani wao wa kisiasa na tumelizungumza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri alieleza Bunge lako, wamefanyia kazi namna gani mapendekezo ya Tume ya Jaji Ihema iliyopendekeza Muundo wa Jeshi la Polisi uangaliwe upya ili haya mashinikizo ya Polisi yaondolewe; na siyo tu Tume ya Jaji Ihema pekee yake; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora vilevile mwaka 2012 imezungumzwa mambo hayo hayo kwamba Jeshi la Polisi linaonyesha upendeleo wazi kwenye Mikutano ya CCM na kwenye Mikutano ya Vyama vya Upinzani. Nataka maelezo ya kutosheleza na nitoe taarifa nitaondoa Shilingi kwenye mshahara wa Waziri ili hili suala lizungumzwe sawasawa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye mchango wangu hapa Bungeni asubuhi ya leo nimezungumzia sana suala la amani ya Taifa letu na nikasisitiza kwamba tuilinda amani ya Taifa letu kwa gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye kipengele kimoja katika suala la udini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukijitahidi kwa pamoja kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwepo kwenye hali ya amani kupitia kwenye Kituo cha Demokrasia Tanzania *(TCD)*. Tuliojifunza kutoka hasa kwenye madhehebu ya dini, ni mambo makubwa sana ya choko choko hizi ambazo zimeota au zimelelewa kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita hali inayozidi kuwa tete siku baada ya siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliiomba Serikali asubuhi ya leo kwamba jukumu letu ni kulinda Katiba. Katiba yetu Ibara ya 19 inaeleza vizuri kabisa sina haja ya kuisoma Serikali inaijua vizuri na sote tunaijua, inayoelezea suala la dini ni suala binafsi. Kwenye kati ya mambo ambayo yanaleta utata mkubwa sana leo hii hapa Tanzania ni suala la mihadhara pamoja na suala hili la imani; nani achinje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni karne ya 21 inakuwa ni fedheha kweli tukianza kupanda *bus* la nani achinje badala ya kufanya mambo ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, tunayo sheria *Animal Welfare Act,* namba 19 ya mwaka 2008 inayoeleza utaratibu wa kuchinja mifugo hawa na kuwatendea hak;i na kile kifungu 30 kinaeleza namna ya *approval of religious slaughter. "The provision of this part shall not apply, where the religious beliefs specify the mode of slaughtering and animal provided that..."* na vile vifungu vingine vinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Waziri wakati wa kujibu hili kwa sababu hakulijibu, ni suala la kuleta Watanzania kwa pamoja na amani. Ninachohitajika ni kusimamia tu zile sheria tulizojiwekea sisi wenyewe ili aweze kutoa tamko la Serikali hapa kwamba tutekeleze na tusimamie Katiba hii na sheria hii badala ya kufanya mambo tofauti. Utaratibu tuliojiwekea tusipoutekeleza itakuwa ni fujo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilikuwa naomba kauli ya Serikali na nimeishaongea na Kaimu Waziri Mkuu, analielewa vizuri hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ombi langu jioni ya leo. Kama sitapata majibu nitatangaza nia ya kutoa Shilingi. Sitaki nifike huko, naamini Serikali imenisikia. *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye mchango wangu wakati tunajadili bajeti ya Waziri Mkuu nilichangia na nikazungumzia suala la Jeshi la Polisi na Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema zile hoja ambazo hazikujibiwa pale, tulitegemea kuzipata kwenye Wizara inayohusika. Lakini cha ajabu Mheshimiwa Waziri hakuigusia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliishauri Serikali kwamba haya mambo ya kuwatangaza Jeshi Polisi kwamba ndiyo wala rushwa wakubwa katika nchi hii, suala la watu kufanya tafiti na kusema Jeshi la Polisi ndiyo namba moja kula rushwa, niliishauri Serikali kwamba hawajapambana na rushwa kikamilifu katika kuziba mianya na nikaainisha mianya ya rushwa ndani ya Jeshi la Polisi kwamba ni mshahara mdogo, posho kidogo na uduni wa makazi. Nikasema hiyo ndiyo mianya inayopelekea Polisi kuwalaumiwa kwamba wanakula rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliishauri Serikali kwamba ili kupambana na vita hii ndani ya Jeshi la Polisi, siyo kuwatumia akina Jerry Muro kumulika kamera kukamata Polisi wakipokea rushwa, isipokuwa tupambane na vita hii kwa kuanzisha Mfuko Maalum ndani ya Jeshi la Polisi ili tuweze kuboresha mishahara yao, posho zao pamoja na makazi. Nikasema, ilivyoonekana kwenye *TRA* kwamba hawakusanyi kodi kwa sababu ya rushwa, Serikali haikuwa na kigugumizi, ikaamua kupandisha mishahara na posho za *TRA* na tukaona kweli rushwa imepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa nini anakuwa na kigugumizi cha

kuanzisha Mfuko Maalum ilihali tunapopambana na umaskini akina mama tunawaanzishia Mfuko Maalum, Vijana tunawaanzishia Mfuko Maalum, na maeneo mengine tunaanzisha hata Benki za Wakulima. Sasa nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri asiwe na majibu mepesi kwenye hoja hii ya msingi. Hatuwezi kuendelea kuwalalamikia Polisi na kusingizia kwamba wanakula rushwa wakati hatupambani na rushwa kwa njia ambazo zinapunguza tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninatangaza Mheshimiwa Waziri akija na majibu mepesi juu ya jambo hili wakati linahusu rushwa, na rushwa ni adui wa haki, na rushwa ni eneo mojawapo ambalo kuhujumu uchumi, na hapa tunasema sungura mdogo. Kwa kweli hatutaelewana, na mimi nitatoa Shilingi kama majibu yatakuwa mepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**SPIKA:** Ulipewa *operation* ya kufungua mdomo lini? Maana ulishafungwa, sasa nani alikufungua mdomo? *(Kicheko)*

Naomba Mheshimiwa Waziri ujibu. *No!* Ngoja tumpe nafasi Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa kwa sababu nina dakika tatu.

**MHE. MOHAMMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina suala la kisera ambalo naomba Mheshimiwa Waziri anipatie ufafanuzi madhubuti kwamba mnamo miaka ya 1990 na kama kumbukumbu yangu ni nzuri, ni mwaka 1996; Waziri aliyekuwa na dhamana kama yako wewe wakati huo, Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, baada ya yale mambo ambayo yanaitwa kero za Muungano kwa upande wa Tanzania Bara kulalamikia kuhusu *passport,* aliondoa *passport* kwamba mtu kutoka Tanzania Bara anaweza kwenda Zanzibar bila ya kuwa na *passport*.

Baada ya mchakato huo, tumeona matendo ya uhalifu Zanzibar yakiongezeka na ya ujambazi kuanzia usiku

mpaka mchana. Wapo wataalam wanaosema moja ni chanzo cha kuondolewa *passport*, wapo wengine wanasema ni *development* ya dunia katika mambo ya utandawazi na mambo mengine. Mojawapo katika hayo yanaweza yakawa kweli au yote mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bahati nzuri Tanzania sasa hivi tuna vitambulisho vya Taifa. Kule Zanzibar kuna *ZAN ID* na Tanzania kwa ujumla tuna *TAN ID*. Vitambulisho hivi vya Taifa vinapelekea sasa Mtanzania kujulikana na kusafiri kwa uhuru zaidi. Sasa kuna tatizo ambalo limejitokeza kubwa sana; mtu anapotokea upande wa Visiwani, anapokuja upande wa Tanzania Bara, ni rahisi kumtambua aidha kwa sura au kwa mazungumzo. Lakini watu wanapotokea upande wa Tanzania Bara kwenda Tanzania Visiwani, labda wale wa Pwani Pwani, lakini wanaotokea upande wa Shinyanga huko na kwingine, huwezi kujua kwamba huyu anatokea Burundi, Rwanda, Zaire au sehemu nyingine. Kwa hiyo, imekuwa ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa kuwa tuna *ZAN ID,* Mheshimiwa Waziri anaonaje naye akatumia hiyo kauli ili kuepuka uharamia unaoendelea kuongezeka na mambo kama hayo yaliyotokea juzi Arusha na mengine ambayo yamejitokeza Zanzibar ambayo sote hatuyafurahii? Wageni wengi sana sasa hivi wanaingia Zanzibar kutoka upande wa Kenya, na kutokea pande nyingine za Bara. Sisi akiingia mtu kutoka Kongo, sisi pengine tunasema anatoka Shinyanga au anatoka Mbeya. Kumbe anatoka Kongo au Burundi. Imekuwa ni tatizo!

Mheshimiwa Waziri anaonaje sasa tukavitumia vitambulisho vyetu vya Taifa, na ile *issue* ya *passport* ikarejeshwa ili wale wageni wanaokuja kule wajulikane wanaingia kutafuta nini? Wanaondoka lini ili kupunguza wimbi kubwa la uhalifu ambalo linaendelea Zanzibar hivi sasa na kwa Tanzania kwa ujumla?

Naomba kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri ili suala hili sasa hivi kama alivyotumia nafasi hiyo mwenzake

aliyekuwa na nafasi kama yake, anaonaje; kwa kuwa sasa Watanzania wanadhani wana *ID* watatembea vizuri, kwa wale wageni ambao hatuwezi kuwajua ambao sura zinafanana wa Bara la Afrika, sasa hivi tukarejesha ile *passport* kwa upande wa Tanzania Zanzibar? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Samuel Sitta ajibu swali la Mheshimiwa James Mbatia.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa James Mbatia, anajishughulisha sana na masuala ya amani ndani ya jamii ya Watanzania. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya mwaka 2008 ya kuzuia ukatili kwa wanyama, *the Animal Welfare Act* 2008 kwa bahati mbaya haijibu moja kwa moja tatizo hili. Sheria hii ilijielekeza zaidi kuona kwamba hata katika shughuli ya kuchinja mnyama, kusiwe na ukatili. Ndiyo maana inasema kwa mfano, unapomchinja mnyama wasiwepo wanyama wengine wa aina yake wanashuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, kwa Kiingereza inasema: "*That slaughtering is performed in a way that other animals waiting for slaughter not to see the slaughtering process.*" Halafu inasema pia katika hicho hicho kifungu cha 30 kwamba, lazima mhusika awe na ujuzi unaomtosheleza kuelewa ile mishipa ya damu ambayo ikichinjwa, basi mara moja italeta kifo cha haraka bila mnyama kutapatapa. Inasema: "*Slaughtering is performed in a way that large blood* vessels *in throat area are opened with one single cut*." Kwa hiyo, kuna utaalam hapo, yaani unapokata mara moja, basi mishipa ile iwe imekatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasikitika kusema hili litakuwa ni nusu tu la jawabu. Ni kweli sheria ipo, lakini inazuia ukatili kwa wanyama wakati wa kuchinja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu mimi, tatizo limetokana na maneno, na hasa tafsiri ya neno Ibada. Baadhi ya madhehebu ya Kikristo waliposikia kwamba baadhi Waislam wamesema kwamba kuchinja ni Ibada, basi hali imegeuka katika nchi. Sasa baada ya kusikia ni ibada, baadhi ya Wakristo wametafsiri kwamba sasa kula nyama kama tulivyozoea ambavyo kuchinja Waislam walikuwa wakichinja ambayo imefanyiwa ibada ya Kiislam, ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nashauri tusiliendeleze hili kwa sasa. Ninavyofahamu, Mheshimiwa Rais ameitisha kikao cha kujumuisha Wanazuoni, Masheikh, Mapadri, Maaskofu na kadhalika ambao wataingia katika undani wa historia ya jambo hili ili tusiendelee kama Taifa kugawika kwa msingi wa nani kachinja mnyama yupi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili siyo dogo. Tukianza kubagua nani kachinja kwa maana hiyo inavyochukuliwa sasa, kama alivyosema Mheshimiwa Rais, itabidi sasa tuwe na mighawa ya aina mbili, katika Vyuo vyetu tuwe na mstari wa watu wanaokwenda kula nyama iliyochinja na dhehebu fulani na dhehebu lingine; tutaendeleza na ubaguzi sijui mwisho tutafika wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini kabisa kwamba vikao vya Mheshimiwa Rais ambavyo vitajumuisha wataalam hasa wa mambo haya kutoka pande zote, Ukristo na Uislam mimi nadhani hao watafikia jibu zuri ambalo litatuongoza kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusubiri hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka niliyonayo naomba niongeze nusu saa baada ya saa mbili kasoro. Mheshimiwa Waziri na Msaidizi wako, majibu kwa yale yaliyoulizwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na Mheshimiwa Diana Chilolo na nakubaliana naye kwamba Jeshi la Magereza ni mdau mkubwa katika Kilimo Kwanza. Siyo tu kama nilivyosema asubuhi kwamba inaweza ikatosheleza mahitaji yake, lakini pia inaweza ikasaidia upatikanaji na uhakika wa chakula hapa nchini. Kwa sasa Jeshi la Magereza linazalisha na linafidia sehemu ya mahitaji yake. Lakini pia linazalisha mbegu ambazo wanauziwa wakulima kwa ushirikiano na Makampuni mbalimbali ya mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Jeshi la Magereza lina matatizo ya vifaa na hili ni jambo ambalo kwa juhudi kubwa tunalifanyia kazi ili tuhakikishe kwamba *potential* ya Magereza inatumika *fully*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo ambayo tumeyafikiria na alitoa mfano wa kupatikana matrekta, tayari tulikuwa na mazungumzo na SUMA JKT kama watapata *consignment* nyingine, basi na Jeshi la Magereza liweze kupatiwa matrekta ambayo yatatumika kwa ajili ya kupanua na kuongeza uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilisema wakati ule kwamba tayari tunafanya mazungumzo na watu wa sekta binafsi ili wanaoweza kuchangia kile walichonacho, na sisi tuna ardhi ambazo tumezitenga katika maeneo ya Mikoa ya Magereza katika sehemu nyingi ili kwa pamoja tuweze kuhakikisha kwamba Magereza inakuwa mdau namba moja katika Kilimo Kwanza. Tuombe hili liwezekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu Magereza na upekuzi. Sidhani kwamba nimelidanganya Bunge. Suala la upekuzi kama nilivyosema, linafanywa kwa Sheria na Kanuni, na sheria hizo zinatungwa hapa Bungeni. Sidhani Bunge lingeweza likatunga sheria ambayo pengine siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupekua nilisema, utu, jinsia, na faragha vinazingatiwa na vimeonyeshwa waziwazi

kwenye hizi Sheria na Kanuni. Kinachoweza kuwa kimetokea na kama kimetokea ni bahati mbaya, ni kwamba sheria hii au taratibu hizi hazikuzingatiwa sehemu hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge aliona jambo hilo likifanywa kinyume cha utaratibu na kukosa faragha; sasa Serikali inakubali kwamba kukosea kwenye jambo hili kunaweza kukadhalilisha watu na pia kuwanyima haki zao za kibinadamu, na sidhani kama Serikali hii inaweza ikafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sasa Serikali nimesema tunaweza tukatazama uwezekano wa kuepuka haya malalamiko madogo madogo. Tumejipanga kwamba tumeshapata mafuta, tumeshapata Kilimo Kwanza, tumeishapata mambo mengi na miradi mingi ambayo tunategemea itainua uchumi, pamoja na gasi. Kwa hiyo, uborekaji wa uchumi ndiyo ambao utatufanya tutoke *level* hii ya *manual* kwenda kwenye nyingine ya vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe Mungu na tufanyie kazi kwa bidii ili tuweze kuifikia hii na kila mtu apende kupekuliwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, wengine bado hawajajibiwa. Akina Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Anne Kilango, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa na Mheshimiwa Lugola.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru waliotangulia kwa majibu yao mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze moja kwa moja na Mheshimiwa James Lembeli. Mheshimiwa James Lembeli aliongelea uzito wa eneo la Kahama na jinsi ambavyo maeneo yenye tatizo la kiusalama ambayo wakati mwingine tunalazimika kuyaundia Mikoa au Kanda Maalum. Sasa niseme tu kwamba kweli hoja yake naielewa, lakini lazima tukae tutathmini hali halisi iliyoko Kahama, tutathmini rasilimali zetu tulizonazo, uwezo wetu kwa sasa, halafu tufikie hatua ya kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutakachofanya mimi na Mkuu wa Jeshi la Polisi tutatafuta muda wa kuzungumza na Mheshimiwa Lembeli ili tuelewe vizuri *concern* yake na tuweze kufanya uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ameongea kwa uzito sana suala la Arusha na kwa kweli amesema anataka majibu *serious* sana yasioonyesha dalili ya Waziri kuchekacheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani nilikuwa naitwa *smiling boy*, lakini imekwisha kazi hii ni ngumu. Kwa hiyo, jambo lenyewe hili siyo dogo na Wizara yangu haijawahi kuchukua jambo la uhalifu lolote kirahisirahisi. Vyombo vya dola vinajua, ndiyo maana niliongea kwa kirefu sana kuhusu *IGP* wetu. Tunafanya naye kazi, saa 9.00 usiku saa 10.00 tunapigiana simu. Majambazi wamevamia sehemu. Mimi na *IGP* tunaongea kwa simu usiku saa 8.00, 9.00, 10.00, ni jambo la kawaida. Yeye hafungi simu na mimi sifungi simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ujambazi na udokozi, ule, tunahangaika nao; hatuwezi kuchukua suala la Arusha kuwa suala dogo. Ndiyo maana pamoja na kwamba bajeti tumeianza jana, juzi tumepata taarifa ya tukio la Arusha, Naibu Waziri pamoja na *IGP* wakaondoka mara moja. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye ali-*facilitate* safari hiyo ya Waziri na *IGP* kwa kasi iliyohitajika na waliweza kufanya kazi iliyokusudiwa. Kwa hiyo, niseme tu kwamba suala la mashambulizi ya kuvizia watu, kuua watu ni jambo lisilokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie wewe na Waheshimiwa Wabunge na nilihakikishe Taifa kwamba tutapambana nalo kwa nguvu zetu zote. Hatutapumzika mpaka watu walioanzisha utaratibu huu watakapojua kwamba nchi yetu, Watanzania hawataki na Serikali haitaki mambo ya hovyo ya kuvizia roho za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo amesema Mheshimiwa Anne Kilango, kwa vyovyote vile unapoanza

kulijadili jambo kubwa kama hili huwezi kusema utatumia nguvu wakati huna fedha. Ni lazima uwe na fedha za kutosha. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais ametuita mimi na wenzangu tukazungumze kuhusu tatizo hili. Moja ya agenda ni tunawezaje kuisimamia vita hii na kuishinda. Maana vita hii ni kuianzisha na kuishinda. Hamna ushindi wa katikati lazima tushinde ifike mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Anne Kilango kwamba tumechukua kwa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye suala la Mheshimiwa Tundu Lissu. Rafiki yangu huyu ni mchokozi sana; urafiki, gharama!

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwanza kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba Jeshi la Polisi haliendeshwi kisiasa. Linaendeshwa kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni za nchi yetu. Wakati wote Askari wote ambao wamewahi kujaribu kuendesha nje ya utaratibu walichukuliwa hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme vilevile kwamba maoni na mapendekezo ya Kamati mbalimbali yanategemea timu inayofanya uchunguzi imekutana na mazingira ya namna gani. Ukimwuliza mtu ambaye ametoka tu kupishana na Trafiki aliyemwomba rushwa; vipi unafahamu nini kuhusu Trafiki? Atakuambia hakuna watu wabaya kama Trafiki. Ni wala rushwa! Lakini ukikutana na mtu ambaye ametoka kupata ajali ya gari, amevunjika mguu, hana wa kumchukua, Trafiki ndiye aliyekuja kumchukua, ukimwuliza; vipi kuhusu Trafiki? Atakwambia hakuna watu wazuri kama Trafiki. Wameokoa maisha yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unapopokea taarifa ya uchunguzi wowote, lazima wewe sasa usimame katikati, usikae sehemu ya mtu aliyeathirika. Ukifanya hivyo, utatoa uamuzi ambao siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile alijenga hoja ya Ma-*RC* na Ma-*DC* kutumika huwalazimisha Polisi. Kwanza niiweke kwenye rekodi kwamba katika nchi yetu Ma-*RC* na Ma-*DC* ambao ndio Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa wanafanya kazi nzuri sana.

Watu wote ambao wana mapenzi mema na nchi yetu, wanaridhika na kazi inayofanywa na Ma-*RC* na Ma-*DC*. Ila watu wote wanaoishi kwa ujanja ujanja, wanapata taabu sana na kazi zinazofanywa na Ma-*RC* na Ma-*DC*. Ndiyo maana yuko msanii mmoja alisema: *"Courage, brother, do not stumble, Though thy path be dark as night; And its end far out of sight, Foot it bravely; strong or weary, some will love thee, some will hate thee, some will flatter, some will slight; cease from man, and look above thee: Perish policy and perish cunning, perish all that fears the light! Whether winning, whether losing, trust in God and do the right. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokusudia msanii huyo ni kwamba watu wasifanye mambo ya ujanja ujanja, wasifanye mambo wanayoogopa mwanga. Muda wote wafanye mambo ya haki bila ya kujali wanashinda au wanashindwa. Wamwamini Mungu na watende ya haki. Salaam hizi zinamfaa sana Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyowekwa mezani ni ya Mheshimiwa Lugola. Amejenga hoja ya kuwekwa Mfuko Maalum kwa ajili ya Jeshi la Polisi. Naomba nikiri kwamba maswali mengi tuliyopewa hata yale ambayo ni ya leo tu hatukuyamaliza kutokana na muda kuwa mdogo. Lakini niseme kwamba hoja yake ya kuwa na Mfuko Maalum ni hoja njema, inahitaji kufanyiwa utafiti na kuamriwa kwa maslahi ya Jeshi la Polisi, lakini pia kwa nchi yetu. Ni kweli kwamba kiwango cha fedha hakitoshi, lakini lazima kila siku tuendelee kutafakari tunafanyaje kupata fedha zaidi, na mtu yoyote ambaye anakuonyesha namna ya kupata fedha anakusaidia.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Lugola tunautambua mchango wako, tutalifanyia kazi wazo lako, tupate uamuzi

sahihi wa namna ya kulimaliza tatizo la fedha kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niseme pamoja na hoja zile za mshahara mdogo, makazi yasiyofaa, posho kidogo, bado hakuna kinachohalalisha kula rushwa, kwa sababu hao unaowalia rushwa hawana huo mshahara mkubwa, hawana hiyo posho kubwa.

Kwa hiyo, nasema Askari wetu tunatambua matatizo ya fedha, matatizo ya mishahara yao, matatizo ya posho yao. Lakini watambue dhamana yao kwa Taifa, hakuna kisingizio cha kuwaruhusu kula rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mnyaa, anasema tunaonaje kama tukirudisha *passport,* uhalifu Zanzibar umeongezeka na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka yalipotokea mauaji ya Padri pale Zanzibar zilizunguka *message* nyingi na vilipotokea vitisho, kuna makaratasi yalisambazwa ya kusema kwamba siku ya Pasaka hakutakalika. *Message* zikaanza kusambaa upande wa Bara. Wanasema kuna Wazanzibar 1,000 wako na majambia wameshapanda jahazi sijui wako wapi, sijui nini.

Sasa siku moja tuliongea na viongozi wenzangu *IGP* na wenzangu tukasema haya siyo mambo ya kuendekeza. Kwa sababu wanasema kaeni mpakani kaeni bahari yote; ina maana sasa tukiruhusu maneno ya namna hii, tunachowaambia, tunasema watu wa Zanzibar waone kwamba tatizo ni watu wa Bara na watu wa Bara waseme tatizo ni watu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno namna hii kama viongozi, lazima tufanye kila njia kuyakwepa. Sisi kama Serikali tutafanya kila njia kuimarisha usalama. Lakini Tanzania ni moja na italindwa yote na Mtanzania ana haki ya kuishi popote bila ya kubaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa taarifa kwamba nitatoa hoja ya kuondoa Shilingi kwenye mshahara wa Waziri. Sasa naomba nitangaze rasmi kwamba natoa hoja ya kuondoa Shilingi kwenye mshahara wa Waziri na naomba suala hili lijadiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema...

**MWENYEKITI:** Sasa tuwe *very specific* kwa sababu sisi itabidi tufanye nini? Tufanye maamuzi, maana ikiwa *so broadly* na nini; basi tuendelee.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siko *so broadly* hata kidogo!

**MWENYEKITI:** Nasema hivyo! Nasema tuwe *specific* katika suala la kujadili hoja. Tumeelewana! Endelea sasa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala la Polisi kutumiwa na wanasiasa wa CCM kwa manufaa ya CCM ni tatizo kubwa sana na linaumiza watu wengi sana. Sisi ambao tumekutana na tatizo hili, ni tatizo kubwa sana. Nafikiri ni bahati mbaya sana kwa Waziri kusema kwamba tunaishi kijanja kijanja. Kwa mtu ambaye ameanza kujiita *Doctor* kabla hajapata *Ph.D* kwa kuhubiria wengine kwamba wasiishi kijanja kijanja ni kitu cha ajabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli sheria ya nchi hii inasema, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ana mamlaka ya kuamuru watu wakamatwe na ni kweli vilevile kwamba Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ni Wajumbe wa Vikao vyote Vikuu vya Chama cha Mapinduzi katika Mikoa na Wilaya. Ni ukweli usiopingika kwamba watu hawa vilevile ni Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama wa Mikoa na Wilaya. Ni ukweli usiopingika vilevile kwamba watu hawa wametumia nafasi zao kukandamiza Wapinzani wa CCM,

kuwazuia Wabunge kufanya Mikutano kwenye Majimbo yao. Mimi nimezuiliwa kufanya Mkutano na watu walionichagua siku tatu baada ya Mkuu wa Mkoa ambaye hajachaguliwa na mtu yeyote kufanya Mkutano kwenye Jimbo langu. Lakini mimi ambaye nimechaguliwa, naambiwa na *OCD* kwamba Mkuu wa Mkoa amekataza. Haya mambo ndiyo yanayosababisha vurugu kwa kweli. Kama hatutendewi haki, inatengeneza mbegu za chuki, inatengeneza mbegu za vurugu. Sasa kuyajibu kirahisirahisi hivi, haitatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba hizi taarifa, nimesema taarifa ya Kamati aliyoiunda yeye, Kamati ya Jaji Ihema imesema mfumo wa Jeshi la Polisi uangaliwe upya ili Jeshi la Polisi lisitumiwe na Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa manufaa ya kisiasa ya CCM. Halafu hapa anasema inategemea aliyeandika hivyo ameathirikaje. Jaji Ihema na Wajumbe wenzake aliowateua Mheshimiwa Waziri waliathirikaje mpaka wakapendekeza hili? Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliyoteuliwa na Mheshimiwa Rais imesema hivi hivi; Jeshi la Polisi linafanya upendeleo kwa Vyama vya Upinzani, inaviumiza; CCM hawana shida. Hawa wameathirika namna gani na matendo ya Polisi mpaka Waziri mzima aseme kwamba inategemea huyo aliyeandika ameathirikaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la ukiukwaji wa sheria, ni suala la matumizi mabaya ya madaraka. Tunataka hoja hii ijadiliwe ili Waheshimiwa Wabunge waridhike kwamba Jeshi la Polisi linalotumia fedha za walipa kodi wote, wanachama wa CCM na wasio wanachama wa CCM linatumika kwa ajili ya shughuli ambazo ziko wazi kisheria, lisitumike kukandamiza Wapinzani wa CCM. Kuna watu wengi wamekamatwa kwa sababu za ajabu ajabu, za kutunga tu. Tunataka Jeshi la Polisi liwe *professional,* lisiegemee upande wowote wa kisiasa, litutendee haki wote. Haya majibu ya Waziri kwa kweli ni bahati mbaya sana kwamba maneno ya aina hii yametoka kwenye mdomo wa Mheshimiwa Waziri. Naomba Waheshimiwa Wabunge walijadili suala hili na tupate muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na natoa hoja kwamba suala hili lijadiliwe na kama halitapatiwa majibu ya sawasawa, basi hiyo Shilingi kwenye mshahara wa Waziri iondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Yaani kile kitendo cha kuondoa Shilingi ndiyo hoja yenyewe.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri yuko sahihi sana kwamba Jeshi la Polisi halitumiki kisiasa, Jeshi la Polisi linaongozwa na kanuni, taratibu na sheria ambazo Bunge hili lenyewe limetunga na ukiwa Mbunge, ukilaumu Jeshi la Polisi kutenda kazi kwa sheria ambazo zimetungwa na Bunge, maana yake Mbunge mwenyewe hujitendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wapo kwa mujibu wa Katiba iliyopo sasa. Mtoa hoja anataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya wasitoe, kwa sababu Chama chao hakitaki Wakuu wa Mikoa na Wilaya wawepo. Lakini kimsingi Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanafanya kazi vizuri na wala hawaongozwi na utashi wa Chama chochote cha siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba Jeshi la Polisi kwa kuonyesha kwamba halibagui, tuna Mbunge mwenzetu sisi hapa ambaye anatoka Mbeya, Mheshimiwa Kilufi kuna wakati pia naye kama Kiongozi amewahi kukamatwa na Jeshi la Polisi. Alikamatwa, huyu ni Mwana-CCM, ni Kiongozi. Alikamatwa kwa nini? Kwa sababu alikuwa na jambo ambalo Polisi walifikiri ni vizuri angetoa maelezo. Kwa hiyo, kwa kuonyesha kwamba kuna ubaguzi siyo sahihi hata kidogo. Mimi kama tulivyozungumza huko nyuma, tuliombe Jeshi la Polisi liendelee kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu zilizopo bila kuhofia haya ambayo yanayozungumzwa na wenzetu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi, Adolf Hitler alikuwa ni mzungumzaji mzuri sana. Wakati huo hajawa Kiongozi wa Ujerumani, alikuwa ni mzungumzaji mzuri kiasi kwamba akiwa kwenye jukwaa, wazungumzaji wengine ambao walikuwepo pale walikuwa hawaonekani kuwa na maana. Kwa hiyo, wananchi ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya ni dakika tatu tatu kwa nyie wote mnaochangia hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naungana na yale anayosema Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni jambo ambalo linasitisha sana, kama watu tunasimama na tunaeleza mambo ambayo yanafanyika, halafu Mheshimiwa Waziri anajibu kwa mzaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi hapa nina *message* zaidi ya 40 zinazouliza hivi kweli Mheshimiwa Lukuvi kama Kiongozi wa ... *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ehee!!!!

**MHE. CHIKU A. ABWAO**: Ndiyo kuhusu usalama huo huo!

**MWENYEKITI:** Nitakuzuia sasa. Tunajadili hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. ALI KESSY MOHAMED:** Onyesha hizo *message! (Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Tunajadili hoja ya Mheshimiwa Tundu lissu. Naomba ujielekeze huko au sivyo, hatuna muda huo, ni dakika tatu.

**MHE. CHIKU A. ABWAO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja kwamba ni kweli kabisa Viongozi wa Serikali wanalitumia vibaya Jeshi la Polisi. Hii ndiyo hoja ambayo Mheshimiwa mtoa hoja bado analalamikia, kwamba Serikali bado inatumia vibaya Jeshi la Polisi.

Tunapozungumzia kwamba Serikali inatumia Jeshi vibaya kisiasa, hatuna maana kwamba Polisi ndio wanaofanya vibaya. Polisi ni watu ambao wanafanya kazi kwa utii. Wao hawana hapana na kila siku wanasema wao ni ndio, *okay*, sawa; hakuna kukataa. Kwa hiyo, wanapoagizwa na Serikali ambayo imewapa ajira, lazima inawatii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka, Serikali iache kutumia vibaya Jeshi la Polisi, kitu ambacho inabidi wakubaliane na sisi kwa sababu ni ukweli kabisa na tuna ushahidi mbalimbali ambao tunaweza tukauwasilisha hapa Bungeni.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naungana na maneno ya Mheshimiwa Waziri, na natuombe sana wenzangu upande wa pili na nimesema asubuhi kwamba Jeshi la Polisi litafanya kazi yake kwa misingi ya kisheria, kanuni na taratibu zake. Tukianza maneno hapa sasa hivi ya kubeza Jeshi la Polisi tutakuwa hatuwatendei haki Polisi wetu, lakini sisi wenyewe tutakuwa hatujitendei haki. Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri sana na utaratibu umewekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Wenyeviti wa Kamati ya Usalama kule kwenye Majimbo yetu, Wilayani, Mikoani. Wasimamizi hao ni Wakuu wa Mikoa pamoja na Ma-DC wetu. Sasa leo mkisema kwamba Jeshi la Polisi linatumika vibaya, naomba tusiogope vivuli vyetu. Tukitenda haki nina uhakika Polisi hawatamwonea mtu. Polisi siku zote hawaonei mtu, ila sisi wenyewe tunapotosha maneno mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Waziri kwa kauli yake. *(Makofi)*

**MHE MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Naungana na Mheshimiwa Waziri kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi ipasavyo. Ma-*DC* na Ma-*RC* wanafanya kazi ipasavyo. Hawa wenzetu wana *allergy* ya Ma-*DC* na Ma-*RC*. Kule Igunga waliwahi kumpiga *DC* wetu. Tuna uhakika na hilo, tunalijua hilo hatutawasikiliza hata kidogo. Polisi wanafanya kazi sawasawa. Juzi tu walikuwa Tabora walifanya Mkutano wao mpaka saa 1.00 usiku wanahutubia Mkutano. *DC* walikuwepo Polisi walikuwepo hawakukamatwa. Lakini wangekuwa wamefanya CCM, wangesema Polisi wanaipendelea CCM.

Kwa hiyo, hivi vitu vidogo vidogo ambavyo havifuati Sheria wanakuja kuvileta hapa ambavyo wao wanavunja Sheria, wanapiga mpaka Ma-*DC*, wanafanya Mikutano mpaka saa 1.00 usiku; kwa hiyo, mimi nasema siyo kweli. Jeshi letu la Polisi linafanya kazi vizuri, inabidi tuli-*support*. Wanatukana watu huko kwenye Mikutano, Jeshi la Polisi linawaangalia hivi halijawafanya chochote. Wanatukana watu na *message*, Jeshi la Polisi lipo linawaangalia. Ingekuwa mwana-CCM wangesema wanapendelea. Kwa sababu Jeshi la Polisi linafanya kazi vizuri sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hili jambo siyo tu kwamba namuunga mkono Mheshimiwa Tundu Lissu, siyo tu kwamba linawaonea Wapinzani lakini pia linainyima fursa Jeshi la Polisi kuwakama wana-CCM ambao wanafanya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtu mmoja wa watu ambao nimeshawaripoti wana-CCM Kibondo ambao wanafanya uvamizi, wanahujumu mali zali za umma. Nimewashtaki Polisi. *DC* anakwenda kuitisha Mkutano wa hadhara, anasema nitafanya uchunguzi, hafanyi na wale watu hawakamatwi. Kwa hiyo, haya mambo tunayoyasema siyo tu kwamba yanatuumiza na kuonewa sisi Wapinzani, bali yanawafanya hata Polisi wasiwakamate. Ma-*DC* na Ma-*RC*

wanaagiza wana-CCM wanaofanya uhalifu wasikamatwe. Nimeripoti na ushahidi upo. Hawakamatwi.

**MBUNGE FULANI:** Uwongo!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, *DC* wa Kasulu ameagiza Viongozi wa NCCR-Mageuzi wakamatwe bila makosa kule kanda ya Kagera. Anaagiza tu, kila mahali wanaagiza tu kwa sababu ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Sasa jambo hili ambalo limejadiliwa vizuri, badala ya watu twende vizuri, tubadilishe mfumo huu, watu wanaleta ushabiki. Hivi nyie mnaleta ushabiki hamwoni? Mimi nimeripoti Polisi watu wanaofanya uhalifu, halafu mnashabikiashabikia hapa. Mbona hawakukamatwa? Hawa watu vipi hawa? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya, kengelea imeshalia. Namwita Mheshimiwa Waziri Kiongozi. Akisimama Waziri Kiongozi ndiyo basi. Kwa sababu muda hauniruhusu. Mheshimiwa Sitta.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa, kwanza nashukuru kwa nafasi hii. Pili nadhani sisi kama Wabunge kuna haja ya kuwatendea Watanzania haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna tuhuma nzito sana dhidi ya Jeshi la Polisi, dhidi ya Serikali ya CCM na zinatolewa na watu tunaowaheshimu sana wenzetu Wabunge wa Upinzani. Nataka kushauri kwamba Kanuni ya 103 siyo mahali pale kuzungumza jambo zito namna hii. Kwa sababu inahitaji hoja ikae vizuri, iwe na ushahidi, majibu yawepo.

Sasa wakati wa kuondoa Shilingi tuzungumzie suala la Polisi kutumika na Wanasiasa na pande zote mbili ziweze kupeana taarifa na kujibu; pengine na upande wa Serikali wana mambo nao ya kusema. Tunakerwa sana na baadhi ya Wanasiasa wa Vyama vingine wanaotoa eti saa 24 fulani aondoke, huu siyo utaratibu pia. Kwa sababu kama kuna Serikali na baadhi ya Wanasiasa wanataka Serikali ionekane

goigoi, haifai; kila mtu anasimama tu, tunatoa wiki moja Waziri Mkuu afanye hiki; tunatoa siku tatu, *DC* ahame. Hatuendi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya yote ukiyachanganya, ni furushi kubwa la kuzungumza vizuri ili tuje tuwasaidie watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemshauri Mheshimiwa Tundu Lissu atumie Kanuni nadhani ya 53 apewe nafasi kwenye Mkutano ujaom elete hoja binafsi kwa mujibu wa Kanunim tuwe na muda wa kutosha labda siku moja au siku mbili tuzungumze hoja binafsi ya Mheshimiwa Tundu Lissu kuhusu suala hili. Tutapeana mifano vizuri na mwisho tunaweza tukafikia muafaka. Lakini kwenye Shilingi hapa, kila mtu atasimama; itakuwa ndiyo ile hadithi ya mnyama ndovu na vipofu. Sisemu tunaitana vipofu, lakini natoa mfano tu. Aliyegusa mkia atasema ndovu ni kama mkuki; aliyegusa masikio, anasema ndovu ni kama ungo; aliyegusa mbavu anasema lake. Sasa hatuwezi kufika pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusihi tuishie hapo tuendelee na mambo mengine tupitishe makadirio haya, halafu mwenzetu alete hoja binafsi kwenye Mkutano ujao halafu tutaijadili kikamilifu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni, zikibaki dakika kumi ni *guillotine*. Sasa nikiruhusu tuendelee kujadili hapa, *guillotine* tunafanyaje? Kwa hiyo mimi nadhani kama Mheshimiwa Tundu Lissu atakubali, tutaiweka vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa. Maana sasa hivi nitakachofanya, ukisema wewe, nitahoji. Hata muda huo wa kuhoji sitakuwa nao kwa sababu tutakuwa tumefikia kipingi cha *guillotine*. Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hoja zilizotolewa halafu kama *guillotine* itafuata, ifuate. Lakini hatuwezi tukaacha hoja zilizotolewa hapa bila kujibiwa.

**MWENYEKITI:** Ninakupa dakika tatu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika tano kwa mujibu wa Kanuni.

**MWENYEKITI:** Sina muda, *guillotine* imefika *my brother*. Naweza nikaingia kwenye *guillotine* bila wewe kujibu. Nakupa dakika tatu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** *I hope* umekubali hili la hoja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu ametambua uzito wa suala hili na nimefurahi kwamba ameingilia na hajatoa majibu rahisirahisi ambayo yamekuwa yanatolewa. Lakini kilicho muhimu ni kwamba kitu ambacho nimekisema kimesemwa na Tume iliyoundwa na Waziri mwenyewe. Tume ya Serikali ndiyo inayosema muundo wa Jeshi wa Polisi uangaliwe ili Jeshi la Polisi lisitumiwe na wanasiasa wa CCM.

Pili, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Wajumbe wake na Makamishna wake ni wateuliwa wa Mheshimiwa Rais, imesema Jeshi la Polisi linatumiwa vibaya. Huyo Kamuhanda wanayesema hajafanya makosa, taarifa ya Haki ya Tume za Binadamu na Utawala Bora, imemtaja kwamba ni mkiuka Sheria. Kwa hiyo, tunachosema, siyo kitu cha kuokoteza. Hili ni tatizo ambalo linahitaji lijadiliwe kwa mapana na marefu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wa Waziri Sitta kwamba lipatiwe fursa nzuri zaidi na nitafanya kama alivyoshauri. Lakini ni tatizo ambalo halihitaji majibu ya kuokotezaokoteza ambayo tumeyasikia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda wa *guillotine* umefika. Haya tunaendelea kwa *guillotine*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ............ .Shs 204,469,400/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ..................Shs 322,963,600/=
Kif. 1004 - *Probation and Comm. Serv div*.....Shs 751,719,000/=
Kif. 1005 - *Government Comm. Unit* .......... Shs 162,519,500/=
Kif. 1006 - *Mgt Info Sys Unit* .........................Shs 111,945,100/=
Kif. 1007 - *Internal Audit Unit* .....................Shs 118,315,900/=
Kif. 1008 - *Procurement Management* .......Shs 172,729,800/=
Kif. 1009 - *Complaints Div*.........................Shs 163,188,000/=
Kif. 1010 - *Legal Service Div* ...................... Shs 261,231,200/=
Kif. 4001 - *Refugees Unit* ..........................Shs 504,797,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Uhamiaji**

Kif. 2001 - *Immigration Zanzibar* .............. Shs 5,160,238,500/=
Kif. 2002 - *Immigration Mainland* ...........Shs 49,315,866,500/=
Kif. 2003 - *Regional Immigration offices* ...Shs15,528,288,000/=
Kif. 2004 - *Tz Regional Immig. Train. Acd*.....Shs 1,506,675,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Mpango wa Maendeleo**

**Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

Kif. 2001 - *Police Main force* .................. Shs 5,980,451,000/=
Kif. 2005 - *Police Zanzibar* ........................Shs 450,000,000/=
Kif. 2017 - *Police Iringa* ............................Shs 300,000,000/=
Kif. 2020 - *Police Kagera* ..........................Shs 500,000,000/=
Kif. 2022 - *Police Mwanza* ........................Shs 600,000,000/=
Kif. 2023 - *Police Mara* .............................Shs 600,000,000/=

Kif. 2041 - *Police Dodoma* ……………………Shs 550,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

Kif. 1001 - *Prisons Headquarter* ……………..….. Shs 300,000,000/=
Kif. 2002 - *Prisons Welfare and Rehab*…..… Shs 1,352,066,000/=
Kif. 4001 - *Prison Building Bridge* ..…………..…Shs 400,000,000/=
Kif. 4002 - *Prison Industries* ……………………Shs 300,000,000/=
Kif. 4003 - *Prison Farms* ………………………Shs 314,500,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Kif. 2002 - *Immigration Mainland* ……. Shs 151,200,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liyakubali rasmi makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Haja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, Wizara kama tulivyosema, naona nyie mmetegemea sana *Budget Committee. Budget Committee* siyo kwamba yenyewe inaweza ku-*produce money*. *Budget Committee* inaweza ku-*juggle around figures* huku. Shilingi bilioni 183 iliyopatikana msidhani kama ni rahisi hivyo. Lakini kwa sababu *budget cycle* yenyewe tumeanzia katikati; kama tukianza mwanzoni hiyo itatupa nafasi zaidi ya kuangalia kwa undani, lakini hii ya katikati siyo rahisi sana. Kwa hiyo, naomba Wizara hela mlizopewa kidogo kidogo kila mahali zitumike vizuri kusudi ziweze kutuvusha tufike kipindi ambacho tunaweza kuiangalia Wizara vizuri zaidi.

Kwa hiyo, tunakupongeza Waziri, tunawapongeza Majeshi yote kwa kazi nzuri wanazozifanya na tunaomba waendelee. Sisi wajibu wetu ni kusema, lakini siyo kuwakatisha tamaa. Mwendelee kufanya kazi kwa kadri Sheria zinavyowaruhusu kusudi tuweze kujenga nchi yenye amani na upendo kati yetu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, nina tangazo. Kwanza, nina tangazo la Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama - Mheshimiwa Anna Abdallah anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati kuwa leo sasa hivi baada ya kuahirisha kikao hiki, wakutane Ukumbi Na. 231. Hivi sasa tukitoka hapa wenzetu wa Kamati hiyo, waende wakutane katika Ukumbi Na. 231.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, napenda kuahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 8.10 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 8 Mei, 2013 saa Tatu Asubuhi)*